| | | mafuta, zilizopo mipakani na nchi jirani pamoja na wilaya zilizokuwa na kambi za wakimbizi;<br>• Kufanya tathmini ya hali ya uharibifu wa mazingira katika wilaya 3 zilizokuwa na kambi tatu (3) za wakimbizi katika ukanda wa Magharibi mwa nchi;<br>• Kupanga matumizi ya ardhi ya wilaya 38 zinazopitiwa na bomba la mafuta, zilizopo mipakani na nchi jirani pamoja na wilaya zilizokuwa na kambi za wakimbizi; na<br>• Kutoa mafunzo kwa Timu za Usimamizi wa Matumizi ya Ardhi za Wilaya 38 zinazopitiwa na bomba la mafuta, zilizopo mipakani na nchi jirani pamoja na wilaya zilizokuwa na kambi za wakimbizi. | | | Singida na Bukombe) zinazopitiwa na Mradi wa Bomba la Mafuta imeandaliwa;<br>• Magari 2 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi yamenunuliwa (Landcruiser Hardtop na Landcruiser GXR V8);<br>• GPS (Handheld) 10, Kompyuta 4 na Laptop 3 zimenunuliwa kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi;<br>• Tathmini ya matumizi ya ardhi na hali ya mazingira imefanyika katika Mikoa ya Tabora na Katavi kwa kushirikiana na sekta husika;<br>• Maandalizi ya mpango wa matumizi ya ardhi wa kanda ya mkuza wa bomba kiwilaya yamefanyika kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC);<br>• Mafunzo ya timu za usimamizi wa matumizi ya ardhi za wilaya 13 za za Misenyi, Muleba, Bukoba, Bukombe, Mbogwe, Chato, Chemba, Iramba, na Kiteto, Handeni na Singida yametolewa; na<br>• Elimu kwa umma imetolewa kupitia makala 8 kwa kushirikiana na |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | vyombo vya habari vya TBC, CLOUDS TV, DIRA TV na ITV. |
| **JUMLA NDOGO** | | | **19,842,539,069.8** | **27,484,624,616** | |
| **OFISI YA MAKAMU WA RAIS** | | | | | |
| 157. | Mradi wa Kuhimili Athari ya Mabadiliko ya Tabia nchi Kupitia Mifumo ya Ikolojia | Mradi huu unatekelezwa kwa kipindi cha miaka 5 (2018 hadi 2022). Lengo la mradi ni Kuongeza uvumilivu wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi katika jamii za vijijini za Tanzania kwa kuimarisha mifumo ikolojia katika Wilaya za Mvomero (Morogoro), Simanjiro (Manyara), Kishapu (Shinyanga), Mpwapwa (Dodoma) na Kaskazini A, (Unguja). | | 2,440,794,454.00 | Shughuli zilizofanyika katika mradi huu ni pamoja na;<br>• Mradi ulizinduliwa tarehe 29 Juni, 2018;<br>• Vikao vya Kamati ya Uongozi wa mradi vimefanyika tarehe 24 Agosti, 2018 na tarehe 22 Februari, 2019;<br>• Kufanyika kwa Tathimini ya Hali Halisi (Baseline Study) ya Ikolojia katika maeneo ya mradi iliyokamilika Oktoba, 2019;<br>• Kuendelea na Maandalizi ya Muundo wa Mfumo wa kimtandao katika Usimamizi wa Maarifa ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi (Adaptation Knowledge Management System - AKMS). Kazi ilianza Julai, 2019;<br>• Kukamilika kwa Tathmini ya Athari na hatari ya Mabadiliko ya Tabianchi (Vulnerability and Impact Assessment - VIA) kwenye maeneo |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | yote ya mradi. Tathmini hii ilifanyika tarehe 10 - 22 Novemba, 2019 na rasimu ya taarifa imeandaliwa na kuwasilishwa kwenye Kamati ya Ushauri wa Mradi;<br>• Kutolewa kwa mafunzo kwa Wataalam na Viongozi (Training of Trainers - ToT) kuhusu namna ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi kwa kutumia Mifumo Ikolojia (EbA approaches). Mafunzo hayo yalifanyika 18-20 Desemba, 2019 kwa kushirikisha Wizara, Mashirika na Taasisi za Serikali na Zisizokuwa za Serikali;<br>• Mkataba wa Makubaliano (MoU) kati ya Ofisi ya Makamu wa Rais na Wizara ya Kilimo ulikamilka Mei, 2019 ili kutekeleza eneo la Kilimo Rafiki kwa mazingira kinachozingatia hali ya mabadiliko ya tabianchi (Climate Smart Agriculure - CSA); na Kuboresha uwezo wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi kwa kuanzisha shughuli mbalimbali za kuingiza kipato kwa vikundi vya |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | wahanga wa mabadiliko ya tabianchi hususan wanawake, watoto, wazee na wenye ulemavu;<br>• Kuandaliwa Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathimini (Monitoring and Evaluation Strategy) ya utekelezaji wa mradi. Rasimu ya Mkakati huo imeandaliwa Desemba, 2019;<br>• Wilaya zinazotekeleza mradi zinakamilisha mchakato wa kupata NGO kwa ajili ya kufanya kazi ya kuanzisha na kuhamasisha utengenezaji na matumizi ya majiko banifu na sanifu, tekinolojia bora ya uzalishaji mkaa ili kupunguza matumizi makubwa ya rasilimali za misitu. |
| 158. | Mradi wa kusaidia kujenga uwezo wa taasisi na jamii kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi kwenye maeneo ya kaskazini mwa nchi | Mradi huu unatekelezwa kwa kipindi cha miaka 2 (2018 hadi 2020). Lengo la mradi ni;<br>• Kujenga uwezo wa jamii kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi kwenye maeneo kame ya wilaya za Same na | | 230,165,952.84 | Shughuli zilizofanyika katika mradi huu ni pamoja na:<br>• Mkataba wa makubaliano kati ya Serikali na AfDB kuhusu utekelezaji wa Mradi umesainiwa tarehe 05 Aprili, 2018;<br>• Kujenga uwezo na uelewa wa viongozi wa halmashauri na wataalam wasimamizi wa mradi |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | Mwanga.<br>• Kujenga uwezo wa Mamlaka ya Hali ya Hewa nchini katika kukusanya, kuchakata na kusambaza taarifa za hali ya hewa kwa halmashauri za wilaya ya Same na Mwanga | | | katika hamashauri za Mwanga na Same;<br>• Taratibu za manunuzi ya wakandarasi wa Ujenzi wa skimu mbili za usambazaji wa maji kwenye vijiji viwili; (Makuyuni na Jipe) wilaya ya Mwanga; na Kukarabati mita 1800 za njia ya jadi za umwagiliaji katika kijiji cha Mabilioni Wilaya ya Same zinaendelea;<br>• Kutolewa kwa mafunzo kwa vikundi vya wakulima kuhusu uendeshaji endelevu wa mradi katika kilimo cha umwagiliaji katika kijiji cha Mabilioni Wilaya ya Same. Mafunzo hayo yalitolewa kwa wanakijiji 30 Septemba, 2019;<br>• Kutolewa kwa mafunzo kwa vikundi vya watumia maji kuhusu matumizi endelevu ya maji katika vijiji vya Jipe, Makuyuni na Kambi ya Simba. Mafunzo hayo yalitolewa kwa wanakijiji 30 Septemba, 2019;<br>• Taratibu za manunuzi ya huduma za wataalam elekezi (Consultancy) wa Kufanya utafiti wa awali kuhusu uwezekano wa kupata athari za mabadiliko ya tabianchi zinaendelea; na |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | • Kuandaliwa kwa Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini wa utekelezaji wa mradi mwezi Julai, 2019. |
| 159. | Mradi wa Kurejesha Ardhi Iliyoharibika na Kuongeza Usalama wa Chakula Katika Maeneo Kame Tanzania | Mradi huu unatekelezwa katika kipindi cha miaka 5 (2017 hadi 2022). Lengo la mradi ni Kuboresha mifumo ya ikolojia ya kilimo ambayo itawezesha kuongeza uzalishaji wa chakula na kuchangia moja kwa moja kuboresha mazingira katika wilaya husika. Maeneo hayo yana changamoto kubwa sana za uharibifu wa mazingira hasa mmomonyoko wa udongo, kupungua kwa rutuba ya udongo na uharibifu wa vyanzo vya maji na misitu. | | 1,625,768,356.00 | Shughuli zilizofanyika katika mradi huu ni pamoja na;<br>• Uzinduzi wa rasmi wa Mradi ulifanyika tarehe 23 Machi, 2018;<br>• Ununuzi wa vitendea kazi vya mradi umefanyika yakiwemo magari mawili, pikipiki tano, laptops nane, photocopy machine moja, printer moja na scanner moja (Agosti, 2018 na Machi, 2019);<br>• Mafunzo kwa maafisa manunuzi yalitolewa kwa watendaji wa Ofisi ya Makamu wa Rais na Halmashauri za Magu, Nzega, Mkalama, Kondoa na Micheweni (Mei, 2018);<br>• Kuunda na kujenga uwezo wa Usimamizi wa Maliasili na Mazingira kwa Kamati za Usimamizi wa Maliasili na Mazingira za vijiji 24; Kamati za Matumizi Bora ya Ardhi kwa Vijiji 17; Kamati za Shirikishi za pamoja za Maliasili na Mazingira 8; Kamati za Shirikishi za pamoja za Matumizi Bora Bora ya Ardhi 5 zimeundwa Aprili, 2019; |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | • Mwezi Juni, 2019 Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi ya vijiji (Vijiji 17 Tanzania Bara) umeandaliwa katika Wilaya za Magu, Mkalama, Nzega na Kondoa;<br>• Aidha kwa upande wa Zanzibar Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi kwa Shehia 8 zilizopo Wilaya ya Micheweni, Pemba zipo katika hatua za mwisho za ukamilishaji 2019/2020;<br>• Hati miliki za kimila kwa kaya 880 katika Halmashauri Magu, kaya 600 katika Halmashauri ya Nzega na katika halmashauri ya Mkalama kaya 600 zilitolewa Agosti, 2019;<br>• Aprili, 2019 Sheria ndogo za Usimamizi wa Mpango Bora ya Matumizi ya Ardhi kwa vijiji 17 vinavyotekeleza mradi zilikamilishwa;<br>• Tathmini ya kutambua vyanzo vya maji na teknolojia zitakazotumika kupata maji kwa ajili ya matumizi ya binadamu, kilimo, mifugo imefanyika katika vijiji 17 vya wilaya za Mkalama, Nzega, Magu na |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | Kondoa mwezi Juni, 2019;<br>• Utafiti wa taarifa za awali kuhusu hali ya uchumi na kijamii (Social Economic Baseline Survey) katika maeneo ya mradi umekamilishwa Agosti, 2019;<br>• Kuandaa Hadidu za Rejea na Hati ya Makubaliano na kusaini hati hiyo kati ya Ofisi ya Makamu wa Rais na (International Centre for Agroforestry Research - ICRAF) kwa ajili ya kufanya utafiti wa taarifa za msingi na tathmini kuhusu hali ya bioanuai, ubora wa udongo, upatikanaji wa maji, uharibifu wa udongo na faida ya hewa ukaa (bio-physical assessment) katika maeneo ya mradi mwezi Julai, 2019;<br>• Kuandaa na Kukamilisha Hadidu za Rejea na Hati ya Makubaliano (MoU) kati ya Ofisi ya Makamu wa Rais na Kituo cha Taifa cha Ufuatiliaji wa Kaboni kwa ajili ya kufanya kufanya ufuatiliaji wa Kaboni katika maeneo ya mradi mwezi Machi, 2019; |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | • Mwezi Septemba, 2018 ziara za kikazi kwa Viongozi wa Ofisi ili kutambulisha mradi katika maeneo yote ya mradi;<br>• Kuratibu na kufanya vikao vinne vya Kamati ya Uongozi (Steering Committee) Juni 2018, Julai, 2018, Agosti, 2018 na Septemba, 2019 na vikao viwili vya Kamati ya Ushauri wa kitaalam (Technical Advisory Committee) Februari 2019 na Mei 2019; na<br>• Kutoa mafunzo msasa (refresher training) ya wawezeshaji wa mashamba darasa. Julai, 2019 jumla ya washirki 38 wamepata mafunzo kuhusu maeneo yafuatayo;<br>a) Kanuni na sifa za mashamba darasa,<br>b) Kilimo hifadhi,<br>c) Kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabia nchi,<br>d) Uvunaji wa maji ya mvua,<br>e) Utunzaji wa vitalu vya miti, upandaji na usimamizi wa miti, na |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | f) Upandaji na usimamizi wa nyanda za malisho.<br><br>Mradi umekamilika kwa asilimia 50 |
| 160. | Mradi wa kukabiliana na changamoto za kimazingira katika Pwani ya Dar es salaam kutokana na athari za Mabadiliko ya Tabianchi. | Mradi huu unatekelezwa kwa kipindi cha miaka 5. (2012 hadi 2019). Lengo la mradi ni Kukabiliana na changamoto za kimazingira katika pwani ya Dar es salaam kutokana na athari za mabadiliko ya tabianchi. | | 11,156,927,584.00 | Shughuli zilizofanyika katika mradi huu ni pamoja na:<br>• Ujenzi wa ukuta Barabara ya Obama ulikamilika mwaka 2018;<br>• Ujenzi wa ukuta Kigamboni ulikamilika mwaka 2018;<br>• Ujenzi wa mfereji wa Ilala ulikamilika mwaka 2018;<br>• Ujenzi wa mfereji wa Mtoni umekamilika mwaka 2019;<br>• Kazi ya kugawa majiko ilikamilika mwaka 2016 na majiko 2999 yaligawiwa kwa Halmshauri husika;<br>• Upandaji wa matumbawe ulikamilika mwaka 2016;<br>• Upandaji wa mikoko umekamilika mwaka 2019 na ufuatiliaji wa maendeleo ya mikoko iliyopandwa Kigamboni na Mbweni unaendelea na ripoti zimeandaliwa; na<br>• Mradi umekamilika kwa asilimia 98 |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| 161. | Mradi wa Kujenga Uwezo Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi katika maeneo ya Pwani | Mradi huu umetekelezwa kwa kipindi cha miaka 6 (2012 hadi 2019). Lengo la mradi ni Kukabiliana na kuhimili ongezeko la kina cha maji ya bahari katika ukanda wa pwani ya Tanzania. | | 7,487,905,300.00 | Shughuli zilizofanyika katika mradi huu ni pamoja na:<br>• Ujenzi wa ukuta wa Pangani eneo la urefu wa mita 950 umekamilika;<br>• Ujenzi wa Makinga bahari (Groynes) matano (5) ya wastani wa mita 100 katika eneo la Kilimani Zanzibar umekamilika mwaka 2017;<br>• Ujenzi wa mfumo wa kuvuna maji ya mvua katika Shule za sekondari Matipwili na Kingani Bagamoyo umekamilika mwaka 2019;<br>• Uchimbaji wa visima vya maji 10 na ujenzi wa matanki 10 ya kuhifadhi maji ya visima Bagamoyo umekamilika mwaka 2019;<br>• Upandaji wa Mikoko hekta 1000 katika Delta ya Rufiji umekamilika mwaka 2018;<br>• Upandaji wa Mikoko Hekta 240 Zanzibar umekamilika 2018; na<br>• Mradi umekamilika kwa asilimia 98. |
| 162. | Mradi wa Kuwezesha Mfuko wa Mazingira | Kuhamasisha ukusanyaji wa rasilimali kwa ajili ya kugharamia mikakati ya | | | Shughuli zilizofanyika katika mradi huu ni pamoja na:<br>• Rasimu ya Waraka wa BLM |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | uhifadhi na usimamizi wa mazingira | | | kurekebisha Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 ili kuwezesha Mfuko wa Mazingira kufanya kazi kwa ufanisi imeandaliwa na ipo katika ngazi ya maamuzi; na<br>• Kukamilika kuainisha na kupendekeza vyanzo vya mapato kwa ajili ya uendeshaji wa Mfuko. Mapendekezo hayo yaliwasilishwa kwenye *Tax Task Force* Desemba, 2019. |
| 163. | Usimamizi endelevu wa Ardhi ya Bonde la Ziwa Nyasa. | Mradi huu unatekelezwa kwa kipindi cha miaka 3 (2018 hadi 2021). Lengo la mradi ni;<br>i) kukuza uwezo wa usimamizi na matumizi endelevu wa Ardhi ya Bonde la ziwa Nyasa.<br>ii) Kuwezesha kuwapo na utaratibu wa kusimamia matumizi endelevu ya ardhi ya bonde la Ziwa Nyasa na kuimarisha ustawi wa jamii ya wakulima wadogo katika | | 992,209,866.58 | Shughuli zilizofanyika katika mradi huu ni pamoja na;<br>• Kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi ya Vijiji 3 katika kila halmashauri za wilaya kama ifuatavyo:- Makete (Kisasatu, Ugabwa, Utengule), Ludewa (Mkongobaki, Ntumbati, Kipangala), Nyasa (Kihuru, Lundo, Mtupale), Kyela (Itete, Kasumulu, Lugombo); na Mbinga (Ntuwaro, Paradiso, Ruanda) katika mwaka 2019;<br>• Kuandaa sheria ndogo za vijiji hivyo 15 kwa ajili ya kusimamia |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | halmashauri za Mbinga, Kyela, Nyasa, Makete na Ludewa.<br>iii) Kupunguza uharibifu wa ardhi unaochangia kuongezeka kwa hali ya ukame na jangwa. | | | mpango wa matumizi bora ya ardhi kwa katika vijiji vitatu kutoka katika kila halmashauri za wilaya za Mbinga, Ludewa, Kyela, Nyasa, na Makete; katika mwaka 2019;<br>• Kukamilika zoezi la kuhamasisha na kuelimisha jamii kuhusu usimamizi na matumizi endelevu ya ardhi katika halmashauri za Wilaya za Ludewa, Makete, Nyasa, Mbinga na Kyela ambapo katika mwaka 2018 Vijiji kumi na vitano (15) vimefanyiwa mpango bora wa matumizi ya Ardhi;<br>• Kuanziasha makundi matatu (3) ya wakulima kwa kila halmashauri za Wilaya za Mbinga, Kyela, Nyasa, Makete. na Ludewa katika mwaka 2018;<br>• Kufundisha na kuwapa mafunzo wawezeshaji 20 kwa Wilaya za makete, Mbinga, Ludewa Nyasa, na Kyela katika mwaka 2018;<br>• Kuandaa mashamba darasa ya kilimo cha mpunga na vitalu vya miche pamoja na kutengeneza |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | mizinga ya nyuki katika vijiji vya Itete, Matema, Ruanda, Ntunduwaro, Paradiso, Mkongobaki, Kipangala na Lupingu katika mwaka 2018;<br>• Kuendesha Warsha ya kukuza uelewa wa usimamizi endelevu wa ardhi ya Bonde la Ziwa Nyasa kwa wataalam 20 kwa Wilaya zote zinazotekeleza Mradi. Warsha hii ilifanyika Agosti, 2019;<br>• Mafunzo ya kuhusu uanzishaji wa vitalu vya miche ya miti kuhusu matumizi mbalimbali kwa wanavikundi kutoka Halmashauri za Makete, Mbinga, Ludewa, Kyela na Nyasa zinazotekeleza mradi kwenda Morogoro Chuo cha kilimo cha Sokoine pamoja na Wakala wa Mbegu za Miti yalifanyika mwaka 2018;<br>• Kuanzisha vitalu vya miche ya miti ya aina mbalimbali katika halmashauri za Mbinga, Ludewa, Nyasa, Kyela and Makete. Vitalu hivi vilianzishwa mwaka 2018; |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | • Kukuza uelewa kwa halmashauri za vijiji juu ya hifadhi ya ardhi, misitu, na maji kwa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo katika halmashauri za Mbinga, Makete, Kyela, Ludewa na Nyasa mwaka 2018;<br>• Kupanda miti 5,540 (Miti 2,300 ilipandwa eneo la Lunyere- Nyasa na miti 3,240 imepandwa katika kijiji cha Amani- Ludewa) kwenye maeneo yaliyoharibiwa kutokana na shughuli za kibinadamu zisizo endelevu katika maeneo yanayotekeleza Mradi. Upandaji huo ulifanyika Oktoba – Desemba, 2019;<br>• Kuendesha Mafunzo kwa vikundi 14 (Nyasa 6 na Ludewa 8) vya wakulima kuhusu kuhifadhi misitu kama shughuli ya kiuchumi. Mafunzo yalitolewa Agosti, 2019;<br>• Kuandaa mfumo shirikishi wa ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa usimamizi endelevu wa ardhi katika halmashauri za |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | Mbinga, Makete, Kyela, Ludewa na Nyasa. Mfumo huu uliandaliwa mwaka 2019; na<br>• Mradi umekamilika kwa asilimia 60. |
| 164. | Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kutekeleza Mkataba wa Montreal Kuhusu Upunguzaji wa Kemikali Zinazomong'onyoa Ukanda wa Ozone | Mradi huu utatekelezwa kwa kipindi cha miaka 2 (2017 hadi 2019). Lengo la Mradi ni;<br>• Kusaidia katika utekelezaji wa Itifaki ya Montreal kuhusu udhibiti wa kemikali zinazoharibu tabaka la ozoni angani.<br>• Utoaji mafunzo kwa wadau katika kutekeleza Programu ya Kitaifa ili kuondosha matumizi ya kemikali na teknolojia zinazotumia kemikali zinazoharibu tabaka la ozoni. | | 256,450,000.00 | Shughuli zilizofanyika katika mradi huu ni pamoja na:<br>• Takwimu za uingizaji nchini kemikali zinazomong'onyoa tabaka la Ozoni zimekusanywa kwa kipindi cha Januari hadi Septemba kila mwaka;<br>• Usajili wa waingizaji na wasafirishaji nje ya nchi kemikali jamii ya HCFCS umefanyika kwa mwaka 2017, 2018 na 2019;<br>• Kuendesha mafunzo kwa maafisa forodha 31 na wasimamizi watano (5) wa sheria kutoka Mamlaka za Serikali za Udhibiti wa uingizwaji wa Kemikali zinazodhibitiwa chini ya Itifaki ya Montreal;<br>• Mafunzo kwa Mafundi Mchundo wa Majokofu, Viyoyozi na Mitambo ya Kupozea kuhusu tekinolojia mpya na njia sahihi za kuhudumia vifaa hivyo yamefanyika kila mwaka. |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | (Novemba, 2017, Mei 2018 na Agosti, 2019);<br>• Kuadhimisha siku ya kimataifa ya hifadhi ya Tabaka la Ozone ambayo hufanyika tarehe 16 Septemba kila mwaka;<br>• Tathmini ya mfumo wa kisheria uliopo na kuendesha mkutano wa wadau mbalimbali kupitia taarifa ya tathmini ya kisheria kuhusiana na kemikali zinazodhibitiwa chini ya Itifaki ya Montreal ilifanyika tarehe 6 – 13 Juni, 2019;<br>• Kuwezesha Serikali kuridhia Marekebisho ya Kigali kwenye Itifaki ya Montreal kuhusu kupunguza matumizi ya kemikali aina ya Hydrofluorocarbons (HFCs) ambazo zimegundulika kuwa zinachangia kwenye mabadiliko ya tabianchi Novemba, 2019; na<br>Mradi umekamilika kwa asilimia 80 |
| 165. | Mradi wa kutekeleza Mpango wa Dunia wa Ufuatiliaji wa Taka Zinazodumu | Mradi huu unatekelezwa kwa kipindi cha miaka 4 (2017 hadi 2020). Lengo la mradi ni kuendeleza mbinu | | 162,495,000.00 | Shughuli zilizofanyika katika mradi huu ni pamoja na:<br>• Kikao kazi kwa ajili ya kujadili mpango wa utekelezaji wa mradi |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | katika Mazingira kwa muda mrefu | zilizopo na bora za usimamizi wa mazingira katika kupunguza uzalishaji taka zinazodumu katika mazingira kwa muda mrefu utokanao na uchomaji taka usiorafiki wa mazingira. | | | pamoja na mgawanyo wa fedha za bajeti kati ya OMR, TBS na GCLA kilifanyika Novemba, 2017;<br>• Uwekaji wa mitambo na ukusanyaji wa sampuli katika shamba la Vikuge Mkoani Pwani kwa ajili kunasa hewa ili kubaini kiwango cha kemikali zinazodumu katika mazingira kwa muda mrefu (POPs) umefanyika Mwezi Machi, 2018;<br>• Kukamilisha zoezi ukusanyaji wa Sampuli za mafuta kwenye transfoma 553 zinazokisiwa kuwa na kemikali aina ya Polychlorinated Biphenyls (PCBs) Agosti, 2019 na kupelekwa Afrika ya Kusini ili kufanyiwa uchunguzi wa kimaabara. Sampuli hizi zilichukuliwa Tanzaia Bara;<br>• Kuendesha mafunzo mahsusi ya namna bora ya kudhibiti kemikali aina ya PCBs kwa wafanyakazi wa TANESCO katika mikoa ya Dodoma, Singida, Mwanza, Kilimanjaro, Arusha, Tanga, Pwani, Dar es Salaam na Mororgoro. |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | Mafunzo yalifanyika Desemba, 2019;<br>• Maeneo ya ukusanyaji sampuli kwa ajili ya uchunguzi yameainishwa na ukusanyaji wa sampuli umefanyika kuanzia Machi 2018 hadi Juni, 2019;<br>• Kuchukua sampuli katika maziwa ya wamama wanaonyonyesha na kutumwa nchini Ujerumani kwa ajili ya uchunguzi wa kimaabara ili kubaini kiwango cha kemikali zinazodumu katika mazingira kwa muda mrefu. Sampuli 55 zilichukuliwa mwezi Agosti, 2029 katika mikoa ya Mbeya, Pwani, Arusha, Mwanza na Dodoma; na<br>• Mradi umekamilika kwa asilimia 85. |
| 166. | Utekelezaji wa Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kitasisi wa Kusimamia Kemikali na Taka Nchini | Mradi huu unatekelezwa kwa kipindi cha miaka 2 (2017 hadi 2019). Lengo la mradi ni Kuwezesha na kuendeleza mfumo wa Sera na udhibiti wa kemikali na taka nchini; | | 257,223,812.00 | Shughuli zilizofanyika katika mradi huu ni pamoja na:<br>• Utengenezaji wa Kanzidata (database) ya kemikali na taka unaendelea. Rasimu ya awali imeshapitiwa na kuboreshwa Agosti, 2019;<br>• Kuandaliwa kwa taarifa ya tathmini ya Uwezo wa Kitaasisi katika Kusimamia Kemikali na Taka |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | Hatarishi Nchini iliyokamilika Novemba 2019;<br>• Mafuzo katika mamlaka zinazosimamia mafuta na gesi kahusu udhibiti wa taka yamefanyika mwezi Agosti, 2018 na Novemba, 2018;<br>• Kuandaliwa kwa kanuni za udhibiti wa Zebaki Desemba 2019;<br>• Mafunzo kwa maafisa kilimo kahusu udhibiti wa taka na kemikali yamefanyika mwezi Agosti, 2018 na Januari, 2019;.<br>• Kukamilishwa kwa Mpango Kazi wa mwaka 2020/21 wa Utekelezaji wa Mradi wa Udhibiti wa Kemikali na Taka Hatarishi (Integrated Health and Environment Observatories and Legal and Institutional Strengthening for the Sound Management of Chemicals in Africa (African ChemObs) Novemba 2019; na<br>• Mradi umekamilika kwa asilimia 80 |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| 167. | Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Makazi na Ofisi ya Makamu wa Rais | Kuwa na mazingira bora na wezeshi ya ofisi na Makazi ya Mheshimiwa Makamu wa Rais na wasaidizi wake | 538,000,000 | | Shughuli zilizofanyika katika mradi huu ni pamoja na kukamilika kwa hatua ya kwanza ya Ukarabati wa Ofisi na Makazi ya Ofisi ya Mheshimiwa Makamu wa Rais Tunguu Zanzibar. Fedha hizi zilitolewa katika mwaka wa fedha 2018/19. |
| **JUMLA NDOGO** | | | 538,000,000.00 | 24,609,940,325.42 | |
| **WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** | | | | | |
| 168. | Upanuzi wa Usikivu wa Shirika la Habari Tanzania (TBC). | • Kuboresha usikivu wa TBC katika maeneo mbalimbali yenye usikivu hafifu hususan mipakani;<br>• Kuanza ujenzi wa jengo jipya la Makao Makuu ya TBC Jijini Dodoma litakalotosheleza mahitaji ya shughuli za utangazaji na utawala;<br>• Kuanzisha Chaneli ya Utalii kwa ajili ya kutangaza maliasili nchini;<br>• Kununua magari 11 ya utangazaji, utafutaji na | 6,644,777,679.00 | | • Michoro ya jengo la Makao Makuu mapya ya TBC Jijini Dodoma imekamilika na kuidhinishwa na Bodi ya Wakurugenzi wa TBC. Aidha, TBC inakamilisha taratibu za kumilikishwa eneo lililopo Mtumba, kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu katika Kipindi cha Mwaka wa Fedha 2019/20;<br>• Chaneli ya Utalii Tanzania (Tanzania Safari Channel) ilizinduliwa na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 15 Desemba, 2018. Aidha, kufuatia jitihada za Serikali kuhakikisha Chaneli |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | uandishi wa habari;<br>• Ukarabati wa studio za redio na televisheni makao makuu ya TBC Jijini Dodoma na kuimarisha mfumo wa usambazaji umeme kwenye studio na urushaji wa matangazo;<br>• Kuendelea na upanuzi wa usikivu katika Mikoa ya Songwe, Simiyu, Njombe, pamoja na Zanzibar (Unguja na Pemba); na<br>• Ununuzi wa vifaa vya utangazaji pamoja na mitambo ya kurushia matangazo mubashara. | | | inafikia wananchi na walengwa wengi zaidi, tarehe 11 Januari, 2019 Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ilibadilisha leseni ya Chaneli ya Utalii kuwa ya Chombo cha Utangazaji cha Umma (Public Service Broadcaster - Must Carry) na hivyo kuiwezesha kurusha matangazo yake kupitia visimbuzi vyote nchini pamoja na majukwaa mengine kama vile mitandao ya kijamii ambapo kwa sasa, Chaneli hii inaonekana katika visimbusi vyote vilivyopo nchini pamoja na katika mitandao ya kijamii. Aidha, Chaneli hii inaonekana kupitia DSTV katika nchi za Burundi, Djibouti, Eritrea, Ethiopia, Kenya, Rwanda, Sudan Kusini, Somalia, Malawi, Congo, Zambia na Uganda; kupitia ZUKU katika nchi za Zambia, Uganda, Kenya na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na kupitia AZAM TV katika nchi zote za Afrika Mashariki; |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | • Ajira mpya 28 zimezalishwa baada ya kuanzishwa kwa Chaneli ya Utalii;<br>• Magari 22 yatakayotumika katika shughuli za ukusanyaji habari na shughuli nyingine za utangazaji yamenunuliwa;<br>• Kukamilika kwa mfumo wa kupooza mitambo katika studio tano (5) za redio zilizopo katika Barabara ya Nyerere;<br>• Kukamilika kwa ufungaji wa mitambo ya redio ya kuwezesha usikivu wa matangazo ya FM kwenye masafa ya 87.7MHz-TBC Taifa na 89.7MHz-TBCFM mkoani Geita;<br>• Kukamilika kwa uwekaji mitambo ya kurushia matangazo ya redio ya FM katika maeneo ya mipakani ikiwemo Rombo, Namanga, Tarime, Kibondo na Mbamba Bay ili kuongeza usikivu wa redio ($TBC_{Taifa}$ na $TBC_{FM}$). Mradi huu uligharimu Shilingi Bilioni 1.;<br>• Kuboreshwa kwa mifumo ya |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | urushaji matangazo kwa njia ya kidigitali baada ya kununua mtambo wa Satelaiti (*Satelite Uplink*) na kuufunga katika studio za TBC Mikocheni;<br>• Kununua mitambo ya kidigitali ya mfumo wa studio za televisheni $TBC_1$ na $TBC_2$ (*Server based system*) kwa thamani ya Shilingi bilioni 1.595. Mitambo ilifungwa studio za Mikocheni na kuendesha mafunzo kwa wafanyakazi wanaotumia mfumo huu;<br>• Kuboreshwa kwa urushaji wa matangazo ya televisheni kwa njia ya digitali (*Server Based System*). Hii imewezesha mifumo ya studio zote za TBC kufanya kazi kwa kuwasiliana, na hivyo kuongeza ufanisi na ubora wa picha na sauti;<br>• Ununuzi wa vitendea kazi vya kisasa vikiwemo Kamera aina ya *drone* inayowezesha urushaji wa matangazo ya moja kwa moja kutoka maeneo yasiyofikika kirahisi, pamoja na Live-U |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | equipment nne (4) kwa ajili ya kurushia matangazo ya moja kwa moja kwa njia ya intaneti; na kifaa kimoja cha kurushia matangazo ya moja kwa moja kwa njia ya Satelaiti (*FLY AWAY*) kutokea sehemu ya tukio;<br>• Kufungwa kwa mtambo wa Redio wa kurushia matangazo Wilayani Lushoto mwezi Mei, 2018;<br>• Studio za kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere zilikarabatiwa kwa lengo la kuwezesha sauti kutoka katika mfumo wa analojia kwenda katika mfumo wa kidijitali;<br>• Mradi wa studio za Kumbukumbu ya Mwl. Nyerere ya Ukombozi wa Bara la Afrika ulikamilika na kuwezesha Sehemu ya jengo la Utangazaji, ambamo studio zake zilitumika kwa ajili ya matangazo ya wapigania uhuru wa Kusini mwa Afrika kukarabatiwa na kazi ya kuhamisha kumbukumbu kwenda mfumo wa Kidijiti kuanza kutekelezwa; |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | • Ukarabati wa Mtambo wa Redio Wilayani Nachingwea ili kuongeza nguvu ya kurusha matangazo kutoka Watt 100 (TBC $_{FM}$) hadi Watt 1,000 na TBC$_{Taifa}$ kutoka watt 250 hadi watt 1,000. Hatua hii imewezesha maeneo ya Nachingwea, Ruangwa na sehemu za Wilaya ya Masasi kupata usikivu wa TBC. Aidha, Mradi wa ujenzi wa mitambo ya TBC$_{FM}$ katika Kituo cha Mtwara ulikamilika Machi 30, 2018;<br>• Ujenzi wa mitambo ya kurushia matangazo ya Redio katika maeneo mbalimbali kumesababisha kuongezeka kwa usikivu wa Redio kutoka Wilaya 87 mwaka 2017/18 (asilimia 54) hadi Wilaya 95 mwaka 2018/19 (asilimia 59) ya wilaya 161. Hadi sasa Wilaya 102 (asilimia 63) zimefikiwa na matangazo ya Redio.<br>• Vifaa kwa ajili ya mfumo wa TEHAMA vilipokelewa tarehe 31 |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | Julai, 2019. Kazi ya kufunga vifaa hivyo ilikamilika Novemba, 2019;<br>• Ukarabati wa jengo la studio umekamilika;<br>• Vifaa na mitambo ya studio za redio vimenunuliwa na TBC Januari, 2020; na<br>• Mfumo mpya wa uandaaji na urushaji wa taarifa ya habari kwa dakika mia na ishirini (120) iliyo sheheni uchambuzi wa kina uitwao ARIDHIO ulizinduliwa Machi 30, 2020. |
| 169. | Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika. | • Kuratibu utekelezaji wa Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika;<br>• Kukarabati majengo yaliyokuwa yakitumiwa na Kamati ya Ukombozi Kusini mwa Afrika;<br>• Kufanya utafiti na kuhifadhi kumbukumbu kidijitali kuhusu harakati za ukombozi Bara la Afrika; | 1,055,009,667.00 | | • Ukarabati wa jengo lililokuwa likitumiwa na Kamati ya Ukombozi wa nchi za Kusini mwa Bara la Afrika lililopo jijini Dar es Salaam unaendelea. Aidha, katika kipindi hiki ukarabati wa mfumo wa maji taka na maji safi kwa jengo dogo umekamilika;<br>• Tovuti kwa ajili ya kutoa taarifa/elimu kuhusu harakati za ukombozi wa Bara la Afrika inaandaliwa kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali Mtandao |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | • Kuandaa sheria na kanuni za kulinda kumbukumbu za harakati za ukombozi Bara la Afrika;<br>• Kuandaa tovuti ya programu ya urithi wa ukombozi wa Bara la Afrika kwa ajili ya kuwezesha upatikanaji wa taarifa mbalimbali kuhusu programu hiyo;<br>• Kuandaa mpango wa kikanda na Mpango wa kitaifa wa utekelezaji wa Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika; na<br>• Kujenga kituo cha Kikanda cha Programu ya urithi wa ukombozi wa Bara la Afrika jijini Dar es Salaam. | | | (eGA);<br>• Mpango wa Kikanda wa utekelezaji wa programu na Mpango wa Kitaifa wa utekelezajiuimeandaliwa na kuwasilishwa kwa wadau wa ndani na nje ya nchi kwa utekelezaji. Aidha, Mpango wa Kitaifa umejadiliwa na Menejimenti ya Wizara na kuboreshwa kwa mujibu wa maoni yaliyotolewa;<br>• Kufanyika kwa mahojiano na Wazee 227 walioshiriki au kushuhudia harakati za ukombozi wa Bara la Afrika katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, Kilimanjaro, Lindi, Mbeya, Morogoro, Mtwara, Pwani, Ruvuma, Singida na Tabora;<br>• Kuratibiwa kwa Maonesho ya Harakati za Ukombozi wa Afrika katika Makumbusho ya Taifa tarehe 27 Oktoba hadi 20 Novemba, 2017;<br>• Kufanyika kwa Mkutano wa Mashauriano baina ya Jamhuri ya |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Afrika Kusini kwa lengo la kuimarisha ushirikiano katika uhifadhi wa Urithi wa Ukombozi wa Afrika. Mkutano huo ulifanyika Mwezi Septemba, 2017 Jijini Dodoma;<br>• Kuratibiwa kwa Mkutano wa Mawaziri wa Utamaduni wa nchi za SADC kwa kushirikiana na Jamhuri ya Afrika Kusini kwa lengo la kuimarisha ushirikiano katika kutekeleza Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Afrika. Mkutano huo ulifanyika mwezi Machi, 2018 nchini Afrika Kusini na kumalizika kwa kusaini *Joint Communique*.<br>• Ununuzi wa Magari matatu kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji wa kazi za Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Afrika;<br>• Kubainishwa na kukusanywa kwa taarifa mbalimbali zikiwemo nyaraka, nyimbo, mashairi, orodha ya maeneo, na vitu halisi |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | mbalimbali vilivyotumika wakati wa harakati za ukombozi wa Bara la Afrika kutoka Tawala za Mikoa, Watu binafsi, Maktaba, Wizara na Taasisi zinazohusika na ukombozi wa Afrika;<br>• Rasimu ya Makala Bainifu ya Sheria ya Kuhifadhi na Kulinda Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika uliopo Tanzania ilikamilishwa na Mtaalam Mwelekezi na kuwasilishwa Wizarani na kufanyiwa maboresho kwa kuzingatia maoni yaliyotolewa na Wizara; na<br>• Eneo kwa ajili ya ujenzi wa Miundombinu ya Kituo cha Makao Makuu ya Kikanda ya Programu limepatikana na lipo Mabwepande Manispaa ya Kinondoni Jijini Dar es Salaam. Hati Miliki ya eneo hilo imeshapatikana. |
| 170. | Habari kwa Umma. | • Kukusanya, kuandaa na kusambaza habari kwa umma kuhusu utekelezaji wa kazi za Serikali | 673,028,188.00 | | • Taarifa na vielelezo kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo pamoja na Ilani ya CCM (2015 – 2020) katika mikoa ishirini na tatu |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | ikiwemo Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2015- 2020), miradi na programu mbalimbali za maendeleo nchini;<br>• Ununuzi wa magari mawili na vitendea kazi vya ofisi ya Idara ya Habari – MAELEZO kwa ajili ya shughuli za kukusanya na kusambaza habari kwa umma; na<br>• Kutoa machapisho mbalimbali pamoja na picha za viongozi. | | | (23) zimekusanywa. Mikoa hiyo ni pamoja na Arusha, Dar es salaam, Iringa, Kagera, Katavi, Kigoma, Kilimanjaro, Lindi, Manyara, Mara, Mbeya, Mwanza, Morogoro, Mtwara, Njombe, Pwani, Rukwa, Ruvuma, Shinyanga, Simiyu, Songwe, Tabora na Tanga. Taarifa zilizokusanywa ziliandaliwa na kutolewa kwa Wananchi kupitia vyombo mbalimbali vya habari vikiwemo TBC na Channel Ten na Mitandao ya Kijamii (You tube);<br>• Magari 2 kwa ajili ya kuimarisha shughuli za ukusanyaji na utoaji habari kwa wananchi yamenunuliwa; na<br>• Nakala 5000 za Jarida maalum la Nchi Yetu kuhusu Miaka Minne (4) ya Serikali ya Awamu ya Tano zilichapishwa. Majarida hayo yalisambazwa Ofisi ya Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Wizara, Mikoa, Wilaya, Ofisi za Balozi za ndani na nje ya nchi, na Taasisi mbalimbali. |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| 171. | Ukarabati wa Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo. | • Kuboresha Miundombinu ya kufundishia;<br>• Kukarabati studio ya kisasa ya muziki na uzalishaji wa sauti; na<br>• Kukarabati miundombinu mingine ya Taasisi (mabweni, madarasa na ofisi). | 300,000,000.00 | | • Ukarabati wa kugawanya/kutenganisha vyumba vya studio, kuzuia utokaji wa sauti nje na kuzuia mwangwi katika studio umefanyika;<br>• Uwekaji wa viyoyozi na utandazaji wa nyaya za umeme na za sauti umefanyika; na<br>• Kununuliwa, kufungwa na kuanza kutumika kwa vifaa vya studio vikiwemo vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika teknolojia ya sauti, muziki, ubunifu, pamoja na uzalishaji wa picha jongefu. |
| 172. | Ujenzi wa Eneo Changamani la Michezo. | • Kukarabati miundombinu ya Uwanja wa Taifa na Uwanja wa Uhuru kwa ajili ya maandalizi ya mashindano ya mpira wa miguu ya vijana wa chini ya umri wa miaka 17 (AFCON-Under 17);<br>• Kuendelea na ujenzi wa Eneo Changamani la Michezo Dodoma; na<br>• Kuendelea na Ujenzi wa | 2,031,808,612.00 | | • Ukarabati wa Uwanja wa Taifa umefanyika katika vyumba vya kubadilishia nguo wachezaji, chumba cha wanahabari, na paa (*shadow*) la jukwaa la VIP limejengwa;<br>• Kuunganishwa kwa huduma za intaneti katika vyumba vyote vya Uwanja wa Taifa;<br>• Kununuliwa kwa viyoyozi viwili vya kusimama (stand Air Condition) na kufungwa katika |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | Awamu ya Tatu ya Eneo Changamani la Michezo Dar es Salaam. | | | chumba cha VIP na uboreshaji wa bustani za Uwanja wa Taifa umefanyika;<br>• Uwanja wa Uhuru umewekwa nyasi bandia na kwa sasa unatumika; na<br>• Maandalizi ya ujenzi wa Uwanja wa Michezo wa Dodoma yameendelea kufanyika ambapo mipaka ya uwanja na barabara zimebainishwa kwa kuwekwa vibao na nguzo za tahadhari dhidi ya wavamizi. Aidha, upembuzi yakinifu, tathmini ya mazingira, maandalizi ya mchoro wa uwanja, "geotechnical Survey na topographical Survey vimefanyika". |
| 173. | Ujenzi wa Chuo cha Michezo cha Malya. | • Kuchimba kisima cha maji safi pamoja na kujenga mifumo yake;<br>• Kukarabati viwanja vitatu vya kufundishia michezo ya Mpira wa kikapu, miguu, riadha na netibali; na<br>• Kukarabati mabweni | 143, 835,000.00 | | • Ukarabati wa nyumba mbili ili kukidhi mahitaji ya mabweni kutokana na kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi umefanyika;<br>• Matanki sita (6) ya kuhifadhia maji yenye ujazo wa lita 5,000 kila moja yamenunuliwa; na<br>• Ukarabati wa viwanja viwili vya |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | mawili (2) ya wanafunzi, Bwalo la Chakula, na Madarasa mawili (2). | | | michezo ambavyo ni Kiwanja cha Mpira wa Kikapu na Kiwanja cha Mpira wa Mikono umefanyika. |
| **JUMLA NDOGO** | | | **10,704,624,146.00** | **0** | |
| **WIZARA YA MAJI** | | | | | |
| 174. | Kuendeleza na kusimamia Rasilimali za Maji. | Kulipa fidia kwa maeneo yanayowekewa mipaka na kutangazwa kuwa maeneo tengefu ya vyanzo vya maji na kujenga Ofisi za Mabonde ya Maji. | 9,841,835,362.00 | 2,219,223,842.00 | • Vituo 55 vya kupima mwenendo wa maji vilifanyiwa ukarabati na vyanzo 35 vimetangazwa kuwa maeneo tengefu ya vyanzo vya maji na taratibu za kutangaza maeneo zaidi zinaendelea;<br>• kupandwa kwa miche 16,400 ya miti rafiki ya maji na kuundwa kwa jumuiya 13 za Watumia Maji;<br>• Kuanza maandalizi ya ujenzi wa bwawa la Farkwa ambapo wananchi 2,612 kati ya 2,868 wanaostahili fidia wamelipwa; na<br>• Kuendelea kujenga na kukarabati Ofisi za Maji za Mabonde na Maabara za Maji katika Mabonde mbalimbali ambapo hatua zilizofikiwa ni: Ruvuma na Pwani ya Kusini (asilimia 90), Ziwa Nyasa (asilimia 50), Rufiji (asilimia 65 |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | Mkoji na Kimani), Ziwa Rukwa (asilimia 65) na Bonde la Kanda ya Kati (asilimia 95).<br>• Kukarabatiwa kwa vituo 53 vya kukusanyia takwimu za rasilimali za maji. |
| 175. | Ujenzi, ukarabati, na upanuzi wa Miradi ya maji katika miji mikuu ya mikoa. | Kugharamia miradi ya maji katika miji ya Kigoma, Lindi, Babati, Mwanza, Misungwi, Geita, Morogoro, Arusha, Dodoma, Tanga, Mtwara na Shinyanga | 56,059,213,175.00 | 39,914,114,277.00 | • Kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu ya maji safi na usafi wa mazingira katika miji ya Sumbawanga na Musoma;<br>• Kukamilika kwa ujenzi wa mradi wa maji katika Mji wa Geita;<br>• Kuendelea na ujenzi wa mradi wa majisafi na usafi wa mazingira katika Jiji la Arusha ambapo umefikia (asilimia 44.3), Lindi (asilimia 92.3) Kigoma (asilimia 93), Mwanza (asilimia 50), Njombe (asilimia 95), Songwe (asilimia 95) Morogoro (Upembuzi yakinifu wa mradi mkubwa umekamilika na taratibu za kumpata Mataalam Mshauri wa kufanya usanifu wa kina zinaendelea), Dodoma (Mtaalam Mshauri wa kusanifu miundombinu ya kuboresha huduma ya maji katika |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | Jiji la Dodoma na Chamwino anaendelea na amewasilisha rasimu ya usanifu wa kina na utekelezaji wa mradi wa usambazaji wa maji katika mji wa Serikali umekamilika);<br>• Mradi wa kuboresha huduma katika mji wa Shinyanga uko katika hatua za kumpata Mtaalam Mshauri wa kufanya mapitio ya usanifu; na<br>• Mradi wa kuboresha huduma ya maji katika mji wa Mtwara, Mtaalam Mshauri anaendelea na usanifu wa kina wa mradi. |
| 176. | Ujenzi, ukarabati, na upanuzi wa miradi ya maji katika miji mikuu ya wilaya, miji midogo na miradi ya kitaifa. | Kuboresha huduma za maji katika miji ya Orkesumet, Bunda, Itumba/Isongole, Mbinga, Makete, Kisarawe, Ruangwa, Liwale, Kibaya, Mbulu, Misungwi, Lamadi, Magu, Sengerema, Nansio-Ukerewe na miradi ya maji ya kitaifa ya Chalinze (Phase III), Mugango – Kiabakari na Butiama. | 46,542,583,231.00 | 12,267,734,913.00 | • Utekelezaji wa miradi ya maji katika Mji ya Longido umefikia wastani wa asilimia 100, na Orkesumet unaendelea na umefikia wastani wa asilimia 68 na miradi ya matokeo ya haraka katika miji 57 imekamilika katika miji ya Kyela, Tukuyu, Turiani, Mahenge, Mvomero, Kilindi, Katesh na Mererani. Aidha, utekelezaji unaendelea katika miji mingine iliyobaki na upo katika hatua mbalimbali;<br>• Miradi ya maji katika miji ya |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | Sengerema na Nansio-Ukerewe imekamilika;<br>• Ujenzi wa mradi wa maji Chalinze (Phase III) unaendelea na umefikia asilimia 79.5;<br>• Usanifu wa ujenzi wa mradi wa maji wa Mugango - Kiabakari na Butiama umekamilika. Mkandarasi wa ujenzi amepatikana na ameanza kazi; na<br>• Utekelezaji wa miradi ya maji katika miji ya Misungwi, Lamadi, Magu umefikia asilimia 96. |
| 177. | Kuboresha upatikanaji wa maji katika Makao Makuu ya Mikoa mipya. | Kuboresha huduma za maji katika miji mikuu ya Mikoa mipya ya Geita, Simiyu, Njombe, Katavi na Songwe. | 5,931,301,950.00 | | Kuendelea na ujenzi wa miradi ya maji katika miji mikuu ya mikoa mipya kama ifuatavyo: Njombe (umekamilika), Songwe - Mlowo (umekamilka) na Vwawa (asilimia 90). Utekelezaji wa miradi ya muda mfupi kwa ajili ya kuboresha huduma za maji katika miji ya mkoa wa Geita umekamilika. Aidha, utekelezaji katika miji ya mikoa ya Katavi – Mpanda na Simiyu – Bariadi unaendelea. |
| 178. | Mradi wa Maji wa Masasi/Nachingwea. | • Kukamilisha ujenzi wa mradi wa maji wa Masasi - Nachingwea pamoja na | 1,000,000,000.00 | | • Kukamilika kwa ukarabati wa mradi ambapo wananchi 24,077 wanapata huduma ya maji; na |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | uunganishaji wa wateja<br>• Ujenzi wa mtambo wa kutibu maji.<br>• Kujenga chujio la maji na kujenga vituo vya kuchotea maji | | | • Kukamilika kwa taarifa ya upembuzi yakinifu na usanifu kwa ajili ya ujenzi wa mtambo wa kutibu na kusafisha maji. |
| 179. | Mradi wa Maji Kahama, Nzega na Tabora. | • Kutekeleza mradi wa kutoa maji kutoka Ziwa Victoria kwenda kwenye Miji ya Tinde, Nzega, Igunga, Uyui, Tabora na Sikonge pamoja na Vijiji vilivyopo kando kando ya bomba kuu.<br>• Kupeleka maji katika vijiji 33 vya nyongeza | 3,095,144,000.00 | 147,356,000,000.00 | • Ujenzi wa miundombinu ya maji katika miji ya Tabora, Igunga, Nzega na vijiji 89 vilivyo pembezoni mwa bomba kuu umefika asilimia 82;<br>• Usanifu kwa ajili ya vijiji 33 vya nyongeza umekamilika;<br>• Kukamilika kwa ulazaji wa mabomba makubwa ya kusafirisha maji kutoka Kijiji cha Solwa kwenda Nzega, Nzega – Tabora na Nzega – Igunga kwa umbali wa kilomita 290.7;<br>• Kukamilika kwa ujenzi wa matanki 17;<br>• Ulazaji wa mabomba ya usambazaji wa maji mijini na vijijini umefikia asilimia 98.6; na<br>• Ulazaji wa mabomba ya matawi umefikia asilimia 86. |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| 180. | Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria - Kahama Shinyanga. | Kutekeleza miradi inayolenga kuboresha huduma ya maji katika miji ya Kagongwa, Isaka, Magu, Sumve, Malya, Lagangabilili, Busega, Bariadi, Mwanhuzi, Kolandoto na Maganzo | 15,111,095,272.00 | | • Kukamilika kwa ulazaji wa bomba la kusambazia maji katika miji ya Isaka, Tinde na Kagongwa;<br>• Miradi katika miji ya Mwadui, Mhunze (Kishapu), Kolandoto na Maganzo imekamilika; na<br>• Kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu ya kupeleka maji katika vijiji vya Mwasekagi na Mwakatola. |
| 181. | Kuboresha Huduma za Maji katika Jiji la Dar es Salaam. | • Ukarabati wa miundombinu ya usambazaji maji ili kupunguza upotevu wa maji;<br>• Ujenzi, ukarabati na upanuzi wa mfumo wa usambazaji wa majisafi;<br>• Ujenzi wa mfumo wa maji kutoka Kibamba hadi Kisarawe;<br>• Kukamilisha malipo ya mradi wa maji wa Ruvu Chini;<br>• Kuanza mradi wa ukarabati na upanuzi wa | 59,227,223,644.00 | 17,443,581,636.00 | • Kuendelea na usambazaji wa maji kutoka mitambo ya Ruvu Juu na Ruvu Chini katika jiji la Dar es Salaam na maeneo ya Bagamoyo, Kibaha na Mlandizi;<br>• Ufungaji wa mita mpya 8,022 na mita 5,231 zimefanyiwa matengenezo, kubadilisha mabomba ya zamani kilomita 62 na kuongeza mtandao wa usambazaji kwa umbali wa kilomita 4.5 katika maeneo ya Kiwalani, Kigamboni mjini – Navy, Segerea, Kinyerezi, Bonyokwa, Mivumoni, Madale, Salasala na Goba;<br>• Kuunganisha maji kwa wateja wapya |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | mfumo wa majitaka katika Jiji la Dar es Salaam<br>• Upanuzi wa mtambo, ulazaji wa bomba kuu la kusambaza maji, ujenzi wa matanki na kulipa fidia kwa wananchi; na<br>• Kujenga miundombinu ya mfumo wa majitaka na kulipa fidia Kurasini. | | | 27,000;<br>• Ujenzi wa bomba la maji kutoka Kibamba kwenda Kisarawe ambapo utekelezaji umekamilika;<br>• Ujenzi wa matanki matano (5), vituo vinne vya kusukuma maji, pamoja na ulazaji wa mabomba kilomita 511.6 umekamilika katika maeneo ya Bagamoyo, Tegeta-Salasala, Bunju Wazo, Changanyikeni, Goba, Mlandizi na Mbezi;<br>• Mtaalam Mshauri atakayesimamia mradi wa Majitaka katika eneo la Jangwani amepatikana na ameanza kazi ya mapitio ya usanifu wa kina na kuandaa makabrasha ya zabuni na unatarajiwa kunufaisha maeneo ya Kinondoni na kuboresha mfumo wa zamani; na<br>• Kupatikana kwa mkandarasi kwa ajili ya ununuzi na ufungaji wa dira za maji pamoja na vifaa vya uboreshaji wa huduma za maji. |
| 182. | Mradi wa ujenzi wa Bwawa la Kidunda. | • Kukamilisha ulipaji wa fidia, ujenzi wa shule, zahanati na huduma za | 6,002,079,861.00 | | • Ulipaji wa fidia umekamilika; na<br>• Usanifu wa bwawa umekamilika. |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | maji kwenye maeneo wanakohamishiwa wananchi wanaopisha mradi wa bwawa la Kidunda. | | | |
| 183. | Mradi wa Maji wa Kimbiji/Mpera. | Kukamilisha uchimbaji wa visima 20 vya Kimbiji na Mpera na kuendelea na utafiti wa maji chini ya ardhi katika maeneo ya Kimbiji na Mpera. | 5,434,618,409.00 | 275,000,000.00 | • Kukamilika kwa visima 19 kati ya 20 vilivyopangwa kuchimbwa katika eneo la Kimbiji na Mpera;<br>• Uchimbaji wa kisima kimoja kilichobaki unaendelea;<br>• Kuanza maandalizi ya ujenzi wa miundombinu ya kusambaza huduma ya maji kwa wananchi kutoka katika visima vitano (5) vya awali vya Kimbiji; na<br>• Kwa ujumla utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 95. |
| 184. | Kupanua na kukarabati miradi ya maji vijijini ambayo inaendelea. | Kuboresha huduma za maji katika vijiji karibu na bomba kuu la KASHWASA, HTM, Chiwambo, Ntomoko na Makonde pamoja na miradi mingine ya maji vijijini. | 152,772,577.00 | | • Ujenzi wa miradi ya maji kutoka mradi wa KASHWASA kwenda vijiji vya Runele, Gatuli, Nyashimbi, Magobeko, Kakulu, Butegwa, Nyang'homango, Ng'homango, Jimondoli, Kadoto, Lyabusalu, Mwajiji, Ichongo na Bukamba umekamilika; utekelezaji wa mradi katika vijiji vya Mwasekagi na |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | Mwakatola umefikia asilimia 100; Mwakuzukana na Kabondo ambapo utekelezaji umefikia asilimia 60; vijiji vya Izuga, Isesa, Igenge na Mbarika, utekelezaji umefikia asilimia 55; na<br>• Mkataba wa kukamilisha ujenzi wa mradi wa maji wa Ntomoko umesainiwa. |
| 185. | Uchimbaji wa Visima na Ujenzi wa Mabwawa. | Kukarabati mabwawa na malambo, upanuzi wa miundombinu ya maji kutoka kwenye mabwawa ya Mwanjoro, Nanja, Masuguru, Matwiga, na Bulenga. | | | • Ujenzi wa Bwawa la Mwanjoro umekamilika na kuhudumia wananchi 13,859 wa vijiji vitatu vya Mwanjoro, Jinamo na Mbushi vilivyopo katika Halmashauri ya Meatu ; na<br>• Uimarishaji wa bwawa la Matwiga umefanyika. Taratibu za kumpata Mtaalam Mshauri wa kufanya usanifu wa miundombinu ya usambazaji maji zinaendelea. |
| 186. | Uboreshaji wa huduma za majisafi na usafi wa mazingira vijijini. | Kukamilisha ujenzi wa miradi inayoendelea; pamoja na kukarabati miradi ya maji na kujenga vituo vipya vya kuchotea maji vijijini katika kila Halmashauri. | 266,096,695,057.00 | 4,225,000,000.00 | • Miradi 75 imekamilika na imeanza kutoa huduma za maji hivyo kufanya jumla ya miradi yote iliyokamilika kufikia 1,268 ambapo vituo vya kuchotea maji vimeongezeka kufikia 131,370 na kuhudumia wananchi 25,359,290; na |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | • Kuendelea na utekelezaji wa miradi 802 ya huduma za maji. |
| 187. | Mradi wa maji Same/ Mwanga/Korogwe | Kuboresha huduma ya maji katika miji ya Same na Mwanga, pamoja na baadhi ya vijiji vya Wilaya za Mwanga, Same na Korogwe | 10,938,367,228.00 | 5,777,615,872.00 | • Kuendelea kwa ujenzi wa miundombinu ya usambazaji wa maji ambapo katika miji ya Same utekelezaji umefikia asilimia 73 na Mwanga asilimia 38; na<br>• Ujenzi wa mtambo wa kusafisha maji umefikia asilimia 81. |
| 188. | Miradi ya maji katika miji 28 itakayotekelezwa kupitia fedha za mkopo kutoka India | Kuboresha huduma ya maji katika Miji na Miradi ya Kitaifa ya Makonde, Handeni (HTM), Kaliua/Urambo, Muheza, Kayanga, Chunya, Manyoni, Wangin'gombe, Songea, Sikonge, Kasulu, Nanyumbu, Kilwa – Masoko, Rujewa, Mugumu, Geita, Chato, Singida, Kiomboi, Mpanda, Chemba, Mafinga, Pangani, Ifakara, Rorya/Tarime na Chamwino | | | Taratibu za kuwapata Wataalam Mshauri wa kuandaa taarifa ya usanifu *Detailed Project Report* (DPR) zimefanyika. Taratibu za kuandaa *Tender Document* zinaendelea. |
| 189. | Kuimarisha Huduma za Ubora wa Maji | Kuwezesha maabara 16 kufanya kazi kwa kununua | | | • Kuendelea na ukarabati, ujenzi na uimarishaji wa ofisi za maji za |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | kemikali na kutekeleza mkakati wa teknolojia ya kutoa madini ya fluoride kwenye maji | | | mabonde na maabara za maji ikijumuisha Bonde la Kati (asilimia 99), Ruvuma na Pwani ya Kusini (asilimia 95), Ziwa Rukwa (asilimia 70), Ziwa Nyasa (asilimia 65), Rufiji Makao Makuu (asilimia 30), Rufiji Kimani na Mkoji (asilimia 85) na Wami-Ruvu (asilimia 65);<br>• Kukusanywa na kuhakikiwa usalama kwa sampuli za maji 2,667 ambapo asilimia 95.8 zilikidhi viwango vinavyokubalika;<br>• kusambazwa kwa mitambo 200 ya kuondoa madini ya *Fluoride* katika maji ya kunywa na kupikia kwa kutumia chengachenga za mkaa wa mifupa ya Ng'ombe katika Mkoa wa Manyara maeneo ya Minjingu na Olasiti itakayonufaisha wananchi wapatao 1,600. |
| **JUMLA NDOGO** | | | **485,432,929,766.00** | **229,478,270,540.00** | |
| **WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI** | | | | | |
| 190. | Ukarabati na Upanuzi wa Huduma za Zimamoto | Kununua Magari matano (5) ya Kuzima Moto na kununua vifaa vya kuzima moto na kufanya Maokozi | 3,000,000,000 | | • Vifaa vya kuzima moto na uokoaji vimeshanunuliwa na kupokelewa na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji mwezi Juni, 2019. |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | • Taratibu za ununuzi wa magari matano (5) ya kuzima moto zinaendelea. Magari hayo yatanunuliwa kutoka Shirika la Nyumbu (TATC) linalomilikiwa na Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania.<br>• Taratibu za ununuzi wa vifaa ya uokoaji zinaendelea ambapo kibali cha ununuzi wa boti mbili (2) za uokoaji unaendelea.<br>• Kuendelea na Ujenzi wa kituo cha Zimamoto na Uokoaji Wilayani Chato (Geita) |
| 191. | Kuendeleza Mashamba ya Jeshi la Magereza | • Kumalizia ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika Gereza Idete<br>• Ununuzi wa zana za kilimo.<br>• Ununuzi wa pembejeo za kilimo. | 3,113,389,304.95 | | • Ujenzi wa banio, mfereji mkuu pamoja na baadhi ya mifereji midogo umefanyika.<br>• Matrekta 18 yamenunuliwa na kusambazwa katika magereza yafuatayo: Mollo (2), Kitai (2), Kitengule (2), Songwe (2), Ludewa (1), Pawaga (1), Kitetengasi (1), Kalila Mkulukulu (1), Ilalagala (1), Kiambatari (1), Ubena (1), Idete (1), Kibrege (1) na Arusha (1). |
| 192. | Ukamilishaji wa | • Ujenzi wa maghorofa 12 | 13,000,000,000 | | • Kuendelea na ujenzi wa majengo 12 |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | nyumba za maafisa na askari | yenye uwezo wa kuchukua familia 322 | | | hadi ghorofa ya pili au ya tatu yenye uwezo wa kuchukua familia 172 |
| 193. | Ukamilishaji wa Magereza | • Kukamilisha ujenzi wa magereza ya wilaya ya Chato na Ruangwa | 3,000,000,000 | | • Awamu ya kwanza ya ujenzi imekamilika kwa kujenga mabweni ya wafungwa wa kiume, ofisi na baadhi ya nyumba za maafisa na askari. |
| 194. | Uendelezaji wa Viwanda vya Magereza | Ujenzi wa kiwanda cha Seremala Gereza Msalato - Dodoma | | | • Andiko la mradi limekamilika.<br>• Eneo la mradi limesafishwa.<br>• Michoro ya jengo la Kiwanda imekamilika.<br>• Makadirio ya mahitaji (BOQ) yameandaliwa na kukamilika. |
| 195. | Ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji Makao Makuu Dodoma | Kuanza Ujenzi wa Makao Makuu ya Uhamiaji Jijini Dodoma | 3,048,182,000 | | • .Ujenzi umefikia asilimia 21 ambapo shughuli zinazoendelea ni kukamilika kwa umwagaji wa jamvi la ghorofa ya kwanza na uwekaji wa nguzo kwa ajili ya ghorofa ya pili. |
| | | • Kuendelea na mradi wa ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Lindi | 856,512,424.39 | | • Mradi umefikia asilimia 53. |
| | | • Kukamilisha ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Geita | | | Mradi umefikia asilimia 60 |
| | | • Kuendelea na ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa | | | Mradi umefikia asilimia 21 |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | Mtwara | | | |
| | | Kukamilisha ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Manyara | 326,147,589.50 | | Mradi umefikia asilimia 65 |
| | | Kumalizia kazi za nje katika mradi wa ujenzi wa nyumba ya Makazi ya Afisa Uhamiaji Mkoa wa Mwanza | | | Mradi umefikia asilimia 98 |
| | | Kumalizia ujenzi wa nyumba ya Kamishna Jenerali wa Uhamiaji Masaki – Dar es Salaam | | | Mradi umefikia asilimia 75 |
| | | Kukamilisha ukarabati wa Nyumba za Makazi ya Watumishi zilizopo Ibinzamata Shinyanga | | | Mradi umefikia asilimia 85 |
| 196. | Chuo cha Upelelezi wa Makosa ya Jinai Dodoma | Ujenzi wa Jengo la Utawala | 1,239,424,306.50 | | • Utekelezaji umefikia asilimia 63. |
| 197. | Technical Equipment (Radios and access) | Ununuzi na ufungaji wa vifaa vya kuratibu taarifa za wahalifu Offenders Management System | 2,890,627,757.20 | | Mradi huu umekamilika na vituo vyote 30 vimeunganishwa kwenye Mkongo wa Taifa. |
| 198. | Mpango wa Ulinzi wa Haki za Mtoto na Ushirikishwaji | Kuelimisha jamii juu ya haki za mtoto, kuwakinga watoto dhidi ya ukatili na | | | Elimu juu ya Haki za Mtoto ilitolewa kwa Maafisa wa Polisi na Jamii kupitia madarasa maalum. Vile vile, Jamii |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | unyanyasaji wa kijinsia | | | ilielimishwa juu ya kuwalinda watoto dhidi ya aina yoyote ya ukatiri na unyanyasaji wa kijinsia. |
| 199. | Mradi wa kuzuia uhalifu unaotokana na Imani kali za Kihafidhina | • Kuelimisha Jamii juu ya Matukio ya Kihalifu na Wahalifu wenye mwelekeo wa Kigaidi<br>• Kutoa Elimu kwa jamii kutokujihusisha na Makundi yenye Imani kali na yale ambayo yana mtazamo wa kuhamasisha uhalifu | | 271,031,500. | • Jumla ya Watumishi wa Serikali 207 wamepata mafunzo katika Wilaya za Lushoto na Tanga Mjini. Kati ya hao wanaume 137 na wanawake 70.<br>• Jumla ya vijana 100 wa Zanzibar wamepata elimu juu ya namna ya kutambua na kuzuia kuenea kwa itikadi kali za kihafidhina.<br>• Maafisa 25 wa magereza walipata mafunzo ili kuwafundisha wengine namna ya kutambua na kuzuia kuenea kwa itikadi kali magerezani.<br>• Kazi ya kukusanya taarifa magerezani katika Mikoa ya Mwanza, Tanga, Zanzibar, Pwani, Lindi na Mtwara imekamilika na taarifa zake zitatumika katika kuandika Mkakati wa Kitaifa wa kuzuia kuenea kwa Itikadi kali za kihafidhina.<br>• Hatua za awali za uandishi wa mkakati zimeanza ambapo Mtaalamu Mwelekezi (Consultant) kutoka Chuo Kikuu Dar-es-Salaam |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | amepatika.<br>• Mafunzo ya kuwajengea uwezo maafisa wa NCT katika kuzuia kuenea kwa itikadi kali yalifanyika mkoani Mwanza.<br>• Vitabu vya kufundishia kwa ajili ya Watumishi wa Serikali na Taasisi za Kijamii zinazoshughulikia masuala ya wanawake vimeandaliwa.<br>• Majaribio ya kitini yamefanyika kwa kuwafundisha Watumishi wa Serikali 25 kutoka Wizara mbalimbali.<br>• Vijana 60 walihudhuria mafunzo ya ufundi stadi katika vyuo vya SUZA; VETA; TALIRI; na SIDO vilivyopo Zanzibar, Mwanza na Tanga. |
| 200. | Ujenzi wa Ofisi na Nyumba za Makazi Tanzania | Ujenzi wa Kituo cha Polisi Mkokotoni Zanzibar | 50,797,753.00 | | • Ujenzi wa jengo la Kituo umekamilika kwa asilimia 60. |
| | | Ujenzi wa Ofisi na Nyumba za Makazi – Byekera Kagera | 415,775,671.00 | | • Ujenzi wa jengo la ghorofa tatu unaendelea ambapo ghorofa ya chini na ya kwanza zimejengwa.<br>• Utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 25. |
| | | • Ujenzi wa nyumba za makazi, Mabatini - Mwanza | 2,245,983,717.00 | | • Utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 80. |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | • Kazi ya ufungaji wa mifumo ya maji na umeme inaendelea. |
| | | • Ujenzi wa nyumba za makazi, Musoma -Mara. | 2,811,830,317.00 | | • Utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 95. |
| | | Ujenzi wa nyumba za makazi, Ludewa - Njombe | 445,174,187.00 | | Ujenzi umetekelezwa kwa asilimia 65. |
| | | Ujenzi wa Ofisi ya RPC – Manyara. | 5,813,303.93 | | Utekelezaji unaendelea. |
| | | Ujenzi wa Kituo cha Polisi daraja A - Ludewa. | 199,350,073.17 | | Ujenzi umetekelezwa kwa asilimia 60. |
| | | Ujenzi wa nyumba za makazi kwa ajili ya kuishi Askari Wilayani Meatu - Simiyu | | | Mradi umeanza kutekelezwa kwa nguvu ya wananchi. Hatua iliyofikiwa ni ya umaliziaji. |
| | | Ujenzi wa Kituo cha Polisi Mbalizi - Mbeya | | | Ujenzi unaendelea kwa nguvu ya wananchi. |
| 201. | Mradi wa Vitambulisho vya Taifa | • Kusajili, kutoa namba ya utambulisho na vitambulisho vya taifa kwa wananchi, wageni wakaazi na wakimbizi waliofikia umri wa miaka 18 na kuendelea. Mradi wa ujenzi ofisi za wilaya kwa kupitia fedha za mkopo wa masharti nafuu kutoka Serikali ya Jamhuri ya | 7,774,272 | 40,924,728 | • Ujenzi wa kanzi data (Data Centre) na Kituo cha Uokozi umekamilika na tayari vituo vyote viwili vinafanya kazi.<br>• Ujenzi wa vituo 13 vya usajili katika Wilaya za Temeke, Kinondoni, Ilala, Arumeru, Arusha Mjini, Ilemela, Nyamagana, Kwimba, Magu, Sengerema, Morogoro Mjini, Longido na Dunga umekamilika. |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | Korea. | | | |
| | | • Upembuzi yakinifu wa Miradi ya ujenzi wa IOC (Intergrated Operating Centre) mjini Dodoma, Ujenzi wa Ghala la kuhifadhia vifaa na nyaraka mbalimbali za Mamlaka, na Ujenzi wa vituo vya utambuzi na usajili katika Wilaya 31 Tanzania bara na Zanzibar. Vituo hivyo vitajengwa katika Wilaya za Kigamboni, Ubungo, Bagamoyo, Tanga Mjini, Kongwa, Singida Manispaa, Rombo, Babati, Geita, Chato, Bukoba Mjini, Musoma, Kahama, Shinyanga, Bariadi, Tabora Mjini, Kasulu, Sumbawanga, Mpanda, Kyela, Mbarali, Momba, Iringa Manispaa, Njombe Mjini, Mtwara Manispaa, Lindi Manispaa, Ruangwa, | 15,142,569 | 70,519,017 | • Mradi upo katika hatua za mwisho za upembuzi yakinifu |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | Songea Mjini, Mjini Magharibi 'A', Kaskazini 'A' na Micheweni | | | |
| **JUMLA NDOGO** | | | **36,671,925,245.64** | **111,443,745.00** | |
| **WIZARA YA KATIBA NA SHERIA** | | | | | |
| 202. | UNICEF *Multisectoral Support* | • Kuandaa mipango ya maendeleo inayojumuisha haki ya motto.<br>• Kusajili Vizazi kwa Watoto wote wa Umri wa chini ya Miaka Mitano Nchini (Tanzania Bara). | | 169,0008,000.00 | • Kukamilika kwa tathmini ya utekelezaji wa Mpango Mkakati wa haki ya Mtoto mwaka 2013 – 2017; na<br>• Kukamilika kwa maandalizi ya Mpango wa Mkakati wa pili wa utekelezaji wa haki mtoto (2019 – 2024) ambapo na masuala mengine yatakayozingatiwa ni unyanyasaji dhidi ya watoto.<br>• Kusajili Vizazi 4,257,705 vya Watoto wa umri wa chini ya miaka 5 katika mikoa ya Mwanza, Mbeya, Songwe, Iringa, Njombe, Shinyanga, Geita, Lindi, Mtwara, Mara, Simiyu, Dodoma na Singida, Morogoro, Pwani ambapo usajili wa watoto wa umri wa chini ya miaka mitano umeongezeka kutoka asilimia 38 (2018) hadi asilimia 45 (2019). |
| 203. | *Strengthening the* | Kuzuia Vitendo Vya ukatili | | 380,587,770.28.28 | • Kuandaa na kuwasilisha taarifa ya |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | *Capacity of The Ministry of Constitutional and Legal Affairs for Women's Rights Legal Review and Institutionalize Response to Violence against Women in the Legal Sector* | dhidi ya Wanawake na Watoto | | | robo ya mwaka ya utekelezaji wa mpango kazi wa Taifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto (2017/17 – 2021/22);<br>• Kuandaliwa kwa mapendekezo ya kuimarisha mifumo ya ulinzi wa haki za wanawake na watoto yatakayohaulishwa kwenye mpango kazi mpya wa kitaifa wa Haki za Binadamu 2018/19 – 2023/24);<br>• Kuandaliwa kwa kanuni za kutekeleza Sheria ya Huduma ya Msaada wa Kisheria ikiwa ni moja ya hatua za Serikali za kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto na kujenga jamii iliyozingatia misingi ya kutoa haki kwa wote na usawa wa Jinsia;<br>• Uchambuzi wa sheria mbalimbali zinazosimamia masuala ya wanawake na watoto wa kike na kutoa mapendekezo ya hatua za kurekebisha mapungufu yaliyopo;<br>• Kuandaliwa kwa taarifa ya tathmini ya mahitaji ya maafisa wa taasisi za utoaji |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | haki (Mahakimu, mawakili wa Serikali, maafisa wa Ustawi wa jamii na maafisa wa polisi) wanaoshughulikia masuala ya ukatili wa kijinsia; na<br>• Kukamilika kwa mapitio ya Sheria, Kanuni na miongozo mbalimbali inayosamia masuala ya wanawake na kutoa maoni kuhusu upungufu uliopo. |
| 204. | Kuimarisha Utoaji wa Haki na Ulinzi wa Haki za Binadamu. | Kuwa na mifumo ya utoaji wa haki na ulinzi wa haki za binadamu kwa wanawake na makundi maalum. | | 228,239,698.40 | • Kutengeneza mfumo jumuishi wa kukusanya, kuchambua na kuhifadhi takwimu na taarifa muhimu zinazohusu sekta ya haki jinai. Mfumo huo umetolewa maoni na wadau mbalimbali na upo katika majaribio;<br>• Kusambaza mapendekezo yaliyokubaliwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye kikao cha 33 cha Baraza la haki za binadamu, chini ya mfumo wa umoja wa mataifa wa mapitio kwa kipindi maalum;<br>• Kupitia rasimu ya taarifa ya nchi ya mkataba wa umoja wa mataifa wa |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | Haki za watu wenye ulemavu wa mwaka 2006;<br>• Kuandaliwa kwa mwongozo wa utoaji huduma ya msaada wa kisheria kwa wafungwa na watu waliopo kizuizini;<br>• Kuandaliwa kwa mpango wa miaka mitano wa utekelezaji wa Sheria ya Huduma ya Msaada wa Kisheria (2017) pamoja na kanuni zake za mwaka 2018;<br>• Kutolewa mafunzo elekezi kwa wasajili wasaidizi wa huduma ya msaada kisheria 139 kutoka katika mikoa 8 ambayo ni Mbeya, Singida, Mwanza, Simiyu, Arusha, Tanga , Lindi na Kigoma;<br>• Kusimika kwa mfumo wa kimtandao wa usajili wa watoa huduma ya msaada kisheria pamoja na kufuatilia utendaji wao; na<br>• Wananchi 50,000 walipewa huduma ya msaada kisheria kwenye siku ya maadhimisho ya wiki ya huduma ya msaada wa kisheria. |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| 205. | *National Human Rights Action Plan - NHRAP* 2018-2022. | Kuweka mfumo wa ufuatiliaji wa taarifa kuhusu Haki za Binadamu na ukusanyaji wa takwimu. | | 514,480,000.00 | • Maandalizi ya Mpango kazi wa pili wa Kitaifa wa Haki za Binadamu (2018 – 2022) yanaendelea kwa kushirikiana na na washauri elekezi; na<br>• Kufanyika kwa ufuatiliaji wa hali ya haki za binadamu nchini katika mikoa nane ya Tanzania Bara na Zanzibar ikiwa ni sehemu ya kupata maoni ya wadau kwa ajili ya kuboresha mpango huo. |
| 206. | *E-JUSTICE* | Kutumia TEHAMA kuimarisha mifumo ya Utoaji Haki ili kuharakisha huduma za utoaji Haki nchini. | 605,441,000.00 | | Kuanzishwa kwa kanzidata ya wanasheria wote walio katika utumishi wa umma;<br>• Kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya TEHAMA ya Ofisi ya makao makuu ya Wizara; na<br>• Kuendelea kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za kisheria kwa kuboresha wa mfumo wa ukusanyaji wa takwimu *(Judicial Statistical Dashbord System)*. |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| 207. | *Building Sustainable Anti-Corruption Action in Tanzania (BSAAT).* | Kuondoa mianya ya rushwa kwenye Mifumo ya Haki-Jinai ambayo ni kikwazo katika kupiga vita dhidi ya Umasikini. | | 572,653,607 | ▪ Kufanya uchambuzi wa mifumo ya Haki-Jinai iliyopo na kutathmini mapungufu yake katika mwenendo wa utoaji Haki na mchango wake katika kuzalisha mianya ya rushwa inayosababisha umasikini nchini;<br>▪ Kuandaa rasimu ya mapendekezo ya kuweka mifumo ya Haki Jinai inayokidhi mahitaji ya sasa na baadaye na isiyo na mianya ya rushwa |
| 208. | Ujenzi wa Hosteli za Kiume katika Chuo cha Mahakama (IJA). | Kiumarisha malazi ya wanachuo na kuinua Taaluma | 1,300,086,777.52 | | Kuendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa hosteli katika Chuo cha Mahakama - Lushoto |
| 209. | Usajili wa watoto walio na umri chini ya miaka mitano. | Kusajili vizazi vyote vya watoto walio na umri chini ya miaka mitano nchini (Tanzania Bara). | 79,302,000.00 | | • Kusajiliwa kwa jumla ya Vizazi 5,665,411 katika mikoa ya Mwanza, Mbeya, Songwe, Iringa, Njombe, Shinyanga, Geita, Lindi, Mtwara, Mara na Simiyu; na<br>• Kupanda kwa kiwango cha usajili kwa watoto wa kundi husika kutoka asilimia 13 (sensa 2012) hadi kufikia asilimia 38 (makadirio mwaka 2018). |
| 210. | Mpango wa Usajili wa Wanafunzi Shuleni Walio na | Kusajili Vizazi vya watoto walio mashuleni ambavyo havijasajiliwa. | 709,482,000.00 | | • Kutolewa elimu kwa umma, semina elekezi na mafunzo ya usajili kwa viongozi wa wilaya za Bariadi, |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | Umri wa Miaka Mitano (5) hadi Kumi na Saba (17). | | | | Tarime, Singida, Ilala, Kinondoni, Temeke, Ubungo, Kigamboni, Iringa Mjini, Kilindi, Ludewa, Njombe, Makete, Wang'ingombe na Musoma<br>• Kusajiliwa kwa jumla ya Vizazi 320,208,011 katika wilaya tajwa hapo juu; na<br>• Ununuzi wa vifaa vya usajili (fomu na vyeti) pamoja na kulipia gharama za kituo cha kudurufu vyeti. |
| 211. | Mfumo wa Usajili wa Uzazi na Vifo kwa Kutumia TEHAMA. | Kuboresha usajili wa vizazi na vifo kwa kutumia mfumo wa TEHAMA | 220,871,920.00 | 14,561,638,189.00 | • Kuzinduliwa kwa mfumo mpya wa kieletroniki wa usajili wa vizazi na vifo;<br>• Kufungwa na kuanza kutekelezwa kwa mfumo huu mpya katika vituo 150;<br>• Kuzinduliwa kwa Mfumo wa kutafuta na kuhifadhi taarifa na takribani rekodi milioni moja ambazo awali zilikuwa kwenye makaratasi zimehifadhiwa na kurahisisha upatikanaji wake kwa matumizi mbalimbali;<br>• Usajili wa jumla ya vizazi 142,617 na vifo 4,962;<br>• Kuimarishwa kwa kanzidata ya usajili |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | ya RITA makao makuu na kituo cha kutunzia taarifa cha Serikali Mtandao;<br>• Wakala umenzisha mazungumzo kuhusu maombi ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, Mamlaka ya Udhibiti wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na Mfuko wa Maendelo ya Jamii *(TASAF)* kuhusu kuunganishwa kwa mifumo yao kwenye mfumo mpya wa usajili wa vizazi wa RITA. Hatua ya kubadilishana taarifa zimeanza kufanyiwa majaribio; na<br>• Wakala umetoa namba kwa ajili ya zoezi la usajili na kuhuisha daftari la mpiga Kura kwa Tume ya taifa ya uchaguzi (NEC), zoezi hili ni mahsusi kwa wale waliotimiza miaka 18 na kwa ambao hawakuwa na kadi ya kupiga kura kwa ajili ya kujiandaa na uchaguzi 2020. |
| 212. | Mpango wa Majaribio ya Usajili wa Matukio ya Vifo. | Kusajili matukio ya vifo na kutoa vyeti vya vifo katika Hospitali na Kata. | | 371,266,000.00 | • Kufanyika kwa mafunzo elekezi ya usajili wa matukio ya vifo kwa wenyeviti wa vijiji katika mkoa wa Iringa, mafunzo elekezi ya usajili wa matukio ya vifo kwa wasajili wasaidizi |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | pamoja na elimu kwa umma na ufuatiliaji wa mwenendo wa usajili; na<br>• Jumla ya vifo 696 vimesajiliwa katika mkoa wa Iringa sawa na asilimia 18.1 ya matukio ya vifo 3,848 yaliyotarajiwa kusajiliwa katika mkoa huo. |
| 213. | Ukaguzi wa Vizuizi vya Watoto Waliokinzana na Sheria | Kupunguza idadi ya watoto walio katika mgogoro na sheria za nchi. | | 85,994,382.00 | Maandalizi ya awali ya Utelekezaji Mpango huu yameanza. |
| 214. | Kuimarisha Upatikanaji Haki za Kisheria na Ulinzi wa Haki za Binadamu Tanzania. | Kuimarisha upatikanaji haki na ulinzi wa haki za binadamu nchini. | | 199,880,908.00 | • Kukamilishwa kwa uandaaji wa Mpango Mkakati wa miaka mitano wa Tume 2018/19 – 2022/23, (CHRAGG Strategic Plan), *Stakeholders Engagement Strategy, Communication and Visibility Strategy*, na *Training plan;*<br>• Kukamilisha makubaliano ya Ushirikiano baina ya Tume na AZAKI katika kufuatilia na kutoa taarifa kuhusu utekelezaji wa masuala ya haki za binadamu;<br>• Tume imesuluhisha migogoro ya ardhi katika wilaya za Same, Liwale na Handeni na kuimarisha maelewano |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | (peace and harmony) kati ya wawekezaji, wananchi na Serikali. |
| 215. | Kuimarisha Misingi ya Ufikiwaji ya Haki Kisheria na Upatikanaji wa Haki za Binadamu kwa Wananchi katika Ngazi za Chini hasa kwa Wanawake. | Kuongeza fursa za upatikanaji wa haki za kisheria na utetezi wa haki za binadamu katika jamii hasa kwa wanawake katika ngazi za chini. | | 442,635,000.00 | • Kutekelezwa kwa mradi kwenye Halmashauri 39 za Mikoa mitano (5) (Mtwara, Mara, Shinyanga, Mbeya na Manyara); na<br>• Kujenga uwezo wa watumishi 870 wa Halmshauri hizo katika ngazi za wilaya na kata katika masuala ya upatikanaji wa haki kisheria na utetezi wa haki za binadamu kwa lengo la kutoa elimu hiyo kwa watendaji katika ngazi ya vijiji na kwa wanachi wote. |
| 216. | Utekelezaji wa Haki za Watu Wanaoishi Maisha ya Asili. | Kutoa elimu na kufuatilia hakiza watu wanaoishi katika mazingira na maisha ya asili. | | | • Kutolewa elimu kwa watumishi 200 wa idara za umma, na elimu kwa wananchi 200, asasi za kiraia 50; na<br>• Kutoa mapendekezo kwa mamlaka kuhusu namna bora ya kushugulikia haki za watu wanaoishi maisha ya asili. |
| 217. | Mpango wa Maboresho Huduma za Mahakama | Kuboresha miundombinu ya mahakama katika ngazi mbalimbali | 28,582,181,424 | | • Kukamilika kwa ujenzi mahakama za wilaya za Bagamaoyo, Ilala, Kigamboni na Mkuranga ambapo ujenzi wa mahakama kuu katika mkoa wa Kigoma unaendelea na ujenzi wa mahakama ya Mara umekamilika. Pia |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | ujenzi wa mahakama za hakimu mkazi katika mikoa ya geita, Njombe, Katavi, Simiyu na Lindi pamoja na mahakama za wilaya 16 unaendelea na ujenzi wa Mahakama za mwanzo 8 umekamilika. |
| 218. | Ujenzi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali – Mtumba, Dodoma | Kujenga Ofisi za Mwanasheria Mkuu wa serikali Dodoma ili kupunguza gharama za pango | 1,000,000,000 | | Jengo limekamilika. |
| **JUMLA NDOGO** | | | **32,497,365,121.52** | **18,666,795,784.40** | |
| **WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** | | | | | |
| 219. | Ujenzi, Ununuzi na Ukarabati wa Majengo ya Ofisi na Makazi Balozini. | Kuwezesha Serikali kumiliki majengo ya ofisi na makazi balozini kuipunguzia Serikali gharama za kulipa pango la majengo ya ofisi na makazi ya watumishi Balozini | 7,397,416,651.40 | | • Ukarabati wa jengo la ubalozi – Maputo, Msumbiji umefikia asilimia 96;<br>• Ujenzi wa uzio katika kiwanja kilichopo Nairobi Kenya;<br>• Kuendelea na ukarabati wa makazi ya balozi na nyumba za watumishi wa ubalozi wa Tanzania Stockholm, Sweden;<br>• Kuendelea na ukarabati majengo ya ubalozi wa Tanzania Kampala;<br>• Kuanza kwa kazi za ukarabati wa majengo ya ubalozi wa Tanzania |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | Kinshasa, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo;<br>• Kuendelea na ukarabati wa makazi ya balozi wa Tanzania Brussels, Ubelgiji;<br>• Kuendelea na ukarabati wa makazi ya Balozi wa Tanzania Ottawa, Canada;<br>• Kuendelea na ujenzi wa vyumba vya mihadhara katika Chuo cha Diplomasia; na<br>• Kukamilika kwa ujenzi wa majengo ya ofisi Mtumba |
| **JUMLA NDOGO** | | | **7,397,416,651.40** | **-** | |
| **WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** | | | | | |
| 220. | Mradi wa Kupunguza Vifo vya akina Mama Vinavyotokana na Uzazi | Kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi kwa kuimarisha miundombinu ya kutolea huduma za afya na kuvijengea uwezo wa kutoa huduma ya dharura na upasuaji wa kutoa mtoto tumboni | 38,900,617,000.00 | 260,805,052,941.00 | • Kukamilika kwa ujenzi na ukarabati wa vituo 487 vya kutolea huduma za afya nchini kuanzia 2016/17 hadi Desemba 2019. Aidha, ujenzi na ukarabati wa vituo hivi vilizalisha jumla ya ajira 68,992 zikijumuisha ajira za kudumu na ajira za mkataba;<br>• Jumla ya magari 117 ya kubebea wagonjwa yamenunuliwa ambapo kati ya hayo 67 yameshasambazwa katika Mikoa mitano ya Mwanza, Kigoma, Mara, Dodoma na Mtwara |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | ili kuimarisha huduma za Rufaa kwa Wajawazito.<br>• Vifaa tiba (mashine za Cryotherapy 97, mashine za 15 na Electrosurgical Excision Procedure mashine 9 na mitungi ya Gesi ya Carbon Dioxide) kwa ajili ya matibabu ya mabadiliko ya awali ya saratani ya mlango wa kizazi vilisambazwa katika Mikoa ya Dodoma, Singida, Mara, Ruvuma. |
| 221. | Ujenzi na ukarabati wa Hospitali za Rufaa za Mikoa | Kujenga hospitali 5 za Rufaa za Mikoa mipya ya Njombe, Songwe, Katavi, Simiyu, na Geita | 30,000,000,000.00 | 10,320,228,634.00 | • Hatua iliyofikiwa katika na ujenzi wa hospitali 5 za rufaa za mikoa hadi Februari 2020 ni: Njombe (50%), Songwe (25%), Katavi (25%), Geita (88%) na Simiyu (97%) ambapo kwa mikoa ya Njombe, Geita na Simiyu huduma zimeanza kutolewa. Aidha, jumla ya ajira 3,504 za kudumu na za mkataba zilizalishwa kutokana na ujenzi wa hospitali za rufaa za mikoa mipya;<br>• Kuboreshwa kwa miundombinu ya TEHAMA katika Hospitali Sita ambazo ni Temeke, Geita, Njombe, Dodoma, Bombo na Mbeya; na<br>• Kuendelea na ujenzi wa majengo |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | mapya na ukarabati wa miundombinu ya kutolea huduma za afya katika hospitali za mikoa ya Mara (Kwangwa), Mwanza (Sekou Toure), Mbeya, Ruvuma (Songea), Lindi (Sokoine), Mtwara (Ligula), Kilimanjaro (Mawenzi), Arusha (Mount Meru), Manyara, Tabora (Kitete), Pwani (Tumbi), Singida, Shinyanga na Dar es Salaam (Mwananyamala). |
| 222. | | Kukarabati na kufunga vifaa katika hospitali 21 za rufaa za mikoa | 30,000,000,000.00 | 3,000,000,000.00 | |
| 223. | Ujenzi wa Hospitali za Wilaya na vituo vya Afya | Kujenga hospitali za Wilaya 71 na vituo vya Afya nchini | | | Hatua iliyofikiwa ni: kuendelea na ujenzi wa Hospitali mpya za Wilaya 71 zikijumuisha hospitali tatu za Uhuru (Dodoma), Mji wa Tunduma (Songwe) na Manispaa ya Ubungo (Dar es Salaam) ambapo utekelezaji katika baadhi ya hospitali umefikia asilimia kati ya 50 hadi 90, baadhi ya halmashauri ujenzi upo katika hatua ya ukamilishaji ikijumuisha kupaka rangi, kuunganisha umeme, maji na kuweka milango na madirisha. |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | |
| 224. | Ujenzi wa Hospitali za Kanda | Kujenga hospitali 3 za kanda ya Kusini - Mtwara, Magharibi - Tabora, Kanda ya Ziwa – Burigi | 12,940,427,476.00 | | • Ujenzi wa hospitali ya Kanda ya Kusini Mtwara unaendelea ambapo jengo la wagonjwa wa nje (OPD) limefikia asilimia 45; na<br>• Ujenzi wa hospitali ya Kanda ya Ziwa Burigi unaendelea ambapo majengo ya huduma za; wagonjwa wa nje (OPD), famasia, maabara, Dharura (Emergency) na huduma za uangalizi wa karibu (ICU) yapo katika hatua mbalimbali za ujenzi. Kwa ujumla, mradi huu umefikia asilimia 89 ambapo majengo yote yapo katika hatua ya kupaka rangi na uwekaji wa marumaru, miundombinu ya umeme, majitaka na mifumo ya TEHAMA. |
| 225. | | Kujenga jengo la ghorofa mbili la huduma za uchunguzi wa mionzi (Radiolojia) na ujenzi wa jengo la wazazi katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Nyanda za juu Kusini-Mbeya | 5,200,000,000.00 | | • Kukamilika kwa jengo la ghorofa mbili la huduma za uchunguzi wa mionzi (Radiolojia) na kuwezesha kuanza kutolewa kwa huduma za uchunguzi wa mionzi (X–Ray Building na CT Scan);<br>• Kuendelea Ujenzi wa jengo la wazazi katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | ya Nyanda za Juu Kusini-Mbeya na hatua iliyofikiwa ni umiminaji wa sakafu ya tatu wa jengo hilo sawa na asilimia 50 ya utekelezaji; na<br>• Kuendelea na ukarabati wa jengo la wodi ya daraja la kwanza ambapo utekelezaji umefikia asilimia 85. Aidha, kukamilika kwa mradi huu kutaongeza idadi ya vitanda kutoka 553 vya sasa kuwa 603. |
| 226. | Kuboresha huduma za uchunguzi wa magonjwa. | Kuwezesha vifaa na vifaa tiba vya kisasa katika hospitali za rufaa, maalum na hospitali za Taifa kupitia mradi wa ORIO | 30,000,000,000.00 | 30,000,000,000.00 | Kukamilika kwa awamu ya kwanza ya kuweka vifaa tiba vya kisasa katika hospitali 5 za Tumbi, Mkuranga, Mwananyamala, Amana na Temeke. |
| 227. | | Kuwezesha upatikanaji wa vifaa, vifaa tiba vya kisasa na kuboresha miundombinu ya kutolea huduma za afya katika Hospitali za Rufaa, maalum na hospitali za Taifa | 78,833,132,300.00 | 2,500,000,000.00 | **Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI)**<br>• Ukamilishaji wa Jengo la MOI awamu ya tatu na ununuzi wa mitambo na vifaa tiba umefanyika na huduma zinatolewa;<br>• Wagonjwa 400 wamepatiwa huduma za kibingwa za upasuaji magoti kwa matundu;<br>• Hadubini ya kisasa kwa ajili ya kufanya upasuaji wa mishipa ya |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | fahamu na ubongo (*Neurosurgeries*) imenunuliwa na imewezesha kwa mara ya kwanza kufanya upasuaji wa kutoa vivimbe vya mishipa ya damu kwenye ubongo (cerebral aneurysm) na kuimarisha upasuaji wa mgongo kwa tundu dogo (*minimum invasive spine surgery);*<br>• Wagonjwa 6,899 walifanyiwa huduma za upasuaji ikiwa ni pamoja na upasuaji wa mifupa, upasuaji wa nyonga, upasuaji wa goti, upasuaji wa mfupa wa paja, upasuaji wa uti wa mgongo, upasuaji wa saratani ya ubongo na vichwa vikubwa na migongo wazi. Huduma hizi zimesaidia kupunguza idadi ya wagonjwa wanaopewa rufaa za matibabu nje ya nchi kwa asilimia 95 na hivyo, kupunguza gharama kwa Serikali;<br>• Kukamilika kwa vyumba vya wagonjwa wenye uangalizi maalum na kuweka vitanda vipya na vya kisasa 16 na monita zake na chumba cha wagonjwa mahututi (ICU) |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | chenye vitanda 18;<br>• Kufungwa kwa vifaa vya kisasa kwa kiwango cha kimataifa katika kitengo cha wagonjwa mahututi;<br>• Kuendelea na ujenzi wa chumba maalum cha kisasa kwa ajili ya kufanya matibabu ya ubongo kupitia mishipa ya damu (Angio Suite) na kununua mitambo ya kisasa; na kupelekwa kwa madaktari watatu (3) na wauguzi wawili (2) kupata mafunzo maalum ya kutumia mitambo na teknolojia ya *Angio Suite* nchini China; na<br>• Kwa mara ya kwanza Taasisi imeweza kutoa matibabu ya Kifafa kwa njia ya upasuaji. |
| 228. | | | | | **Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI)**<br>• Wagonjwa zaidi ya 1,000 walifanyiwa upasuaji wa moyo kwa mwaka 2015 hadi Juni 2019 ambapo hatua hii imeokoa takribani shilingi bilioni 20 ambazo zingetumika kuwapeleka wagonjwa wa moyo nje ya nchi;<br>• Mitambo ya kisasa ya kufanya |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | upasuaji imenunuliwa "cath lab";<br>• Ununuzi wa CT Scan na MRI umefanyika kwa ajili ya uchunguzi wa magonjwa;<br>• Wagonjwa 1,882 walipatiwa matibabu kwa njia ya tundu dogo (catheterization lab) bila kufungua kifua;<br>• Upasuaji wa moyo kwa kufungua kifua na upasuaji wa mishipa ya damu kwa wagonjwa 289, ambapo 140 walikuwa watu wazima na 149 watoto kwa kipindi cha kuanzia June hadi Desemba 2019;<br>• Vile vile, upembuzi yakinifu wa mradi wa kupanua eneo la Mlongazila awamu ya pili kwa ajili ya wagonjwa wa moyo nchini umeanza; na<br>• Zaidi ya asilimia 90 ya wagonjwa wa moyo wanapatiwa matibabu nchini. |
| 229. | | | | | **Taasisi ya Saratani Ocean Road**<br>• Wagonjwa 741 wamepatiwa matibabu ya Saratani baada ya Mashine 2 mpya za kisasa za mionzi za LINAC kununuliwa; |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | • Kuimarika kwa upatikanaji wa dawa kutoka asilimia 4 mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 85 mwaka 2019;<br>• Mtambo wa PET/CT Scan umenunuliwa na hatua za ufungwaji zinaendelea<br>• Wagonjwa 108 kutoka nje ya nchi walipatiwa huduma za tiba ya Saratani Mwaka 2018/19. Kati ya hao, 51 walitoka Kenya, 34 Malawi, 15 Comoro, 5 DRC, 2 Musumbiji na 1 Zimbabwe;<br>• Vipimo vya radiolojia 9,897 vilitolewa katika kipindi cha mwaka 2019/20;<br>• Kufanyika kwa uchunguzi na tiba za dawa ya nyuklia kwa kutumia mashine za Gamma Camera;<br>• Kuendelea na ukarabati wa miundombinu ikiwemo mfumo wa majitaka ya jengo la wodi, stoo ya dawa maalum, dawa za tiba ya Saratani katika wodi ya tiba kemia; uwekaji wa milango na madirisha ya chuma ili kuimarisha usalama katika wodi za tibakemia; na |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | • Kutoa mafunzo kwa Wanafunzi 52 kwa ngazi ya Shahada ya kwanza ya Tiba ya Mionzi. |
| 230. | | | | | **Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Ziwa Bugando**.<br>• Kukamilika kwa awamu ya kwanza ya ujenzi wa jengo la kufunga Mashine za LINAC za tiba ya mionzi katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Ziwa Bugando;<br>• Kuendelea na awamu ya pili ya mradi wa Saratani kwa kujenga wodi ya kulaza wagonjwa wa Saratani ambapo mkandarasi ameanza maandalizi ya kupeleka vifaa eneo la mradi (mobilization);<br>• Kuzalisha chupa 38,000 za maji tiba ya aina tisa tofauti za ujazo wa nusu lita kwa kila moja; na<br>• Kuzalisha mitungi 11,098 ya oxgen kupitia mitambo miwili iliyosimikwa hospitalini. |
| 231. | Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya kutolea huduma za Afya | Kujenga wodi mpya, na kukarabati majengo yaliyopo katika Taasisi ya Magonjwa ya Kuambukiza ya | 128,000,000.00 | 2,183,000,000.00 | • Kukamilika kwa ujenzi wodi mpya, na ukarabati wa majengo yaliyopo katika Taasisi ya Magonjwa ya Kuambukiza ya Kibongóto na |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | Kibongóto na ujenzi wa maabara ya kisasa | | | majengo hayo kuanza kutumika. Aidha, ujenzi wa maabara ya kisasa kwa awamu ya kwanza umefikia asilimia 65 na awamu ya pili upo katika hatua za ununuzi;<br>• Kukamilika kwa michoro ya eneo itakapowekwa mashine ya CT - Scan na taratibu za ununuzi zinaendelea;<br>• Kununuliwa kwa mashine nne (4) za uchunguzi wa madhara yatokanayo na dawa na mashine 1 ya ultrasound kwa ajili ya uchunguzi wa magonjwa;<br>• Kutolewa mafunzo ya kudhibiti magonjwa ambata ya Kifua Kikuu na Kisukari kwa wataalam 89 katika mikoa mitatu ya Iringa, Dar es salaam na Kilimanjaro; na<br>• Kukabidhi mashine 27 aina ya HbA1c Analyser kwa vituo vya afya 27 kwa ajili ya kutoa huduma kwa wagonjwa wenye magonjwa ambata ya Kifua Kikuu na Kisukari. |
| 232. | | Kujenga na kukarabati miundombinu katika Hospitali ya Rufaa ya Afya ya Akili-Mirembe na Taasisi | 900,000,000.00 | | **Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe**<br>• Ukarabati wa wodi 10, jengo la x-ray pamoja na jengo la *community* |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | ya Isanga | | | *psychiatric;*<br>• Jumla ya wagonjwa 171,721 walihudumiwa, kati yao 91,854 ni wagonjwa wa nje (OPD), ambapo 33,675 ni wagonjwa wa kawaida na 58,179 ni wagonjwa wa akili na wagonjwa 79,867 wa ndani waliopatiwa huduma za afya ya akili kwa kipindi cha kuanzia June hadi Desemba 2019;<br>• Kuimarika kwa Hali ya upatikanaji wa dawa za wagonjwa wa akili kwa asilimia 86 na dawa za magonjwa mengine ya kawaida kwa zaidi ya asilimia 80;<br>• Jumla ya wagonjwa 390, walipata huduma za kibingwa za Neuro-recognative na dementia wagonjwa 165 walipewa huduma za Saikolojia na wagonjwa 76 walifanyiwa uchunguzi na kuandikiwa taarifa za kisheria. Aidha katika kliniki ya afya ya akili kwa watoto na vijana wagonjwa 1,740 walihudumiwa; na<br>• Jumla ya wagonjwa 45,122 wenye matatizo ya utumiaji wa madawa ya |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | kulevya wamepatiwa huduma kati yao wapya walikuwa 132. |
| 233. | | Kujenga Maabara Kuu ya Afya ya Taifa-Mabibo, DSM | | 8,478,796,926.38 | • Ujenzi wa Maabara Kuu ya Afya ya Taifa-Mabibo, DSM umefikia asilimia 98 ambapo hatua za kufunga mabenchi unaendelea. Mkandarasi anatarajia kukabidhi jengo mwezi Machi 2020. |
| 234. | Ujenzi wa Kiwanda cha dawa za asili | Ununuzi na ufungaji wa mitambo ya kuzalisha dawa katika Kiwanda na Maabara ya Dawa za Asili NIMR - Mabibo | 1,200,000,000.00 | | Ujenzi na ununuzi wa mitambo umekamilika. Aidha, taratibu za ufungaji zinaendelea wakati mitambo inasubiriwa kuwasili mwezi Machi, 2020. Vile vile uzalishaji wa dawa unategemewa kuanza mwezi Julai 2020. |
| 235. | Upatikanaji wa Huduma ya Damu salama | Kujenga vituo 5 vya Damu Salama katika mikoa ya Kigoma, Rukwa, Njombe, Tanga na Katavi na kununua vifaa vya kupimia makundi ya damu kwa ajili ya kanda ya ziwa Mwanza, Kanda ya magharibi Tabora, Mbeya, Mtwara na Dar es Salaam | | 17,548,000,000.00 | • Ujenzi wa kituo cha Damu Salama katika Mkoa wa Njombe unaendelea kutekelezwa na hatua za kuwapata wakandarasi kwa ajili ya kujenga mradi kama huo katika mikoa ya Kigoma, Rukwa, Tanga na Katavi zinaendelea;<br>• Mashine za kisasa za kupima makundi ya damu na maambukizi kwenye damu zimenunuliwa na kusimikwa katika kanda ya ziwa |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | Mwanza, Kanda ya magharibi Tabora, Mbeya, Mtwara na Dar es Salaam.<br>• Kukamilika kwa ujenzi wa kituo cha Damu salama katika hospitali ya Benjamini Mkapa; na<br>• Katika kipindi cha Julai hadi Desemba, 2019 jumla ya chupa za damu salama 165,897 zilikusanywa sawa na asilimia 88 ya lengo la kukusanya chupa za damu 187,500 kwa nusu mwaka. Chupa zote 165,897 zilizokusanywa zilipimwa makundi ya damu pamoja na magonjwa makuu manne ambayo ni Ukimwi (HIV,) Homa ya Ini B na C (HBV, HCV) na Kaswende (Syphilis). Jumla ya chupa 150,284 sawa na asilimia 90 zilikuwa salama na kusambazwa katika hospitali kwa ajili ya wagonjwa wenye uhitaji wa damu. |
| 236. | Kuimarisha Upatikanaji wa Chanjo Nchini. | Kuhakikisha watoto wote wenye umri chini ya mwaka mmoja na mama wajawazito wanapatiwa | 50, 654,000,000.00 | 23,349,293,131.00 | • Kiwango cha chanjo kimeongezeka kutoka asilimia 97 (2016/17) hadi asilimia 99 robo ya kwanza (2019/20); |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | chanjo ili kuwakinga na magonjwa yanayozuilika kwa chanjo. | | | • Kutokomezwa kwa ugonjwa wa Polio nchini na kuifanya Tanzania kuwa na hati ya kutokomeza ugonjwa wa polio;<br>• Maghala 2 ya kutunzia Chanjo yamekarabatiwa na vifaa vya kuzalisha ubaridi (Cooling System) vimefungwa katika vyumba nane (8) kwa ajili ya kuhifadhi Chanjo;<br>• Magari 74, Fork lift 3, na Jenereta 1 zilinunuliwa kwa ajili ya huduma za Chanjo. Kati ya magari hayo, magari 61 aina ya Toyota pick up yalipelekwa katika Halmashauri kwa ajili ya kusambaza Chanjo;<br>• Majokofu 1,385 kwa ajili ya kutunzia Chanjo yalinunuliwa na kusambazwa kwenye Halmashauri zote nchini;<br>• Vishikwambi (tablets) 1,249 kwa ajili ya kukusanyia taarifa za Chanjo vilinunuliwa na kusambazwa kwenye Halmashauri;<br>• Ununuzi na usambazaji wa chanjo na vifaa vya kutolea huduma za chanjo nchini kwa ajili ya kuwakinga watoto dhidi ya magonjwa |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | kuambukiza kama vile surua, dondakoo, ugonjwa wa kupooza; kutolewa chanjo ya kukinga ugonjwa wa Polio na chanjo ya PENTA-3 inayozuia magonjwa ya Dondakoo, Kifaduro, Pepopunda, homa ya ini na homa ya uti wa mgongo kwa watoto 1,027,566 wenye umri chini ya mwaka mmoja, sawa na asilimia 98 ya lengo; watoto 8,082,861 walipata chanjo ya kuzuia ugonjwa wa surua na rubella sawa na asilimia 112 na watoto 4,040,654 sawa na asilimia 114 wamepatiwa chanjo ya kuzuia ugonjwa wa kupooza kwa nchi nzima kupitia kampeni ya chanjo ya kuzuia surua na ugonjwa wa kupooza kwa kipindi cha kuanzia Julai hadi Desemba 2019; |
| 237. | Mapambano dhidi ya Maambukizi ya Malaria. | Kupunguza maambukizi ya ugonjwa wa malaria kutoka asilimia 14 mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 1 ifikapo 2020 | 56,749,289,000.00 | 229,042,566,155.90 | • Vitendanishi (*MRDT*) vipimo 21,664,450, dawa mseto ya Malaria (*ALU*) dozi 3,982,740 na vidonge vya *SP* dozi 4,457,433 kwa ajili ya kuwakinga wajawazito dhidi ya madhara ya Malaria vilinunuliwa na kusambazwa katika mikoa yote; |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | • Upuliziaji wa dawa ya ukoko katika kuta za ndani ya nyumba umefanyika katika mikoa minne ya Kanda ya Ziwa (Kagera, Mwanza, Mara na Geita);<br>• Vyandarua 31,916,335 vyenye dawa vimesambazwa kwa wananchi mikoa yote bila malipo;<br>• Maambukizi ya malaria yamepungua kutoka asilimia 14 mwaka 2015 hadi asilimia 7.3 mwaka 2017;<br>• Kiwango cha maambukizi ya Malaria kwa akina mama wajawazito kimepungua kutoka asilimia 6.8 mwaka 2015 hadi asilimia 1 mwaka 2017; na<br>• Kupungua kwa maambukizi ya Malaria kwa watoto wenye umri wa chini ya miaka 5 kutoka asilimia 7.3 mwaka 2015 hadi asilimia 1 mwaka 2017. |
| 238. | Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI (*NACP*). | Kutekeleza na kufikia malengo ya 90 tatu ambapo (i) asilimia 90 ya watu wanaoishi na VVU kutambua hali zao za | | 63,466,288,248.43 (CDC na GF) | • Hadi kufikia Mwezi Desemba 2019 watu 1,282,277 sawa na asilimia 80.1 ya watu wanaokadiriwa kuishi na VVU 1,600,000 walipimwa na kutambuliwa kuishi na VVU; |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | maabukizi,<br>(ii) asilimia 90 ya waliogundulika kuwa na maambukizi ya VVU wanatumia dawa za kufubaza makali ya VVU(ARV) na<br>(iii) Asilimia 90 ya wanaotumia dawa za ARV wanakuwa na kiwango cha chini cha VVU. | | | • Watu 1,266,521 sawa na asilimia 98.8 ya wanaoishi na VVU 1,282,277 walianzishiwa tiba ya ARV;<br>• Asilimia 92 ya watu wanaotumia dawa za ART, kiwango cha maambukizi kiko chini, hivyo kuwawezesha kuishi bila magonjwa nyemerezi;<br>• Maambukizi mapya ya VVU yameendelea kupungua kutoka 80,000 mwaka 2016 hadi 72,000 mwaka 2018;<br>• Kiwango cha maambukizi ya VVU kimepungua kutoka asilimia 7 mwaka 2003/04 hadi asilimia 4.7 mwaka 2016/17;<br>• Maambukizi mapya kwa vijana yamepungua kutoka asilimia 3.2 mwaka 2011/2012 hadi asilimia 2.2 mwaka 2016/2017;<br>• Kuongeza idadi ya mashine za kupimia wingi wa virusi vya UKIMWI kutoka mashine 17 mwaka 2015 mpaka mashine 40 mwaka 2019; na<br>• Kuongeza idadi ya vituo vinavyotoa |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | huduma na Tiba ya UKIMWI ambapo mpaka kufikia mwezi Desemba 2019 vimefikia vituo 6,529 kutoka Vituo 5,555 mwaka 2015. |
| 239. | Mapambano Dhidi ya TB. | Kuboresha huduma za kudhibiti Kifua kikuu ili kupunguza maambukizi mapya. | 33,301,648,000.00 | 93,788,226,104.35 | • Vituo 284 vya kutolea huduma za afya vimekarabatiwa, hivyo kufanya idadi ya vituo vyenye uwezo wa kutoa huduma za uchunguzi wa Kifua kikuu kuwa 1,200 mwezi Machi 2019/2020;<br>• Jumla ya wagonjwa 40,072 wa Kifua kikuu waligunduliwa ikiwa ni ongezeko la asilimia 6% ukilinganisha na wagonjwa 37,924 waliogunduliwa kipindi kama hiki mwaka 2018;<br>• Kueendelea kuimarisha huduma za ugunduzi wa maambukizi ya ugonjwa wa kifua kikuu ambapo Mashine 16 zaidi za *Gen Xpert* zimeongezwa katika mikoa ya Pwani, Singida, Mbeya, Songwe, Dodoma na Manyara na hivyo kufikisha jumla ya mashine 238 kutoka mashine 210 mwaka 2018;<br>• Halmashauri takriban 115 kwa sasa |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | zina mashine hizi na Serikali imejipanga ifikapo Desemba 2020 Halmashauri zote zipatiwe mashine hizi;<br>• Vioo vya hadubini (glass films) 671 vilinunuliwa na kugawiwa kwa maabara 5 mkoani Dar es Salaam.<br>• Karatasi za mashine za X-ray (X-ray films and processors) zilinunuliwa na kugawiwa kwa vituo vya afya 30 vyenye mashine hizi katika mikoa ya Morogoro, Mtwara, Lindi, Njombe na Iringa; na<br>• Kampeni ya uchunguzi ilifanyika katika halmashauri za Ifakara na Kilombero kwa wananchi wa vijiji vya Msagati, Taweta na Mlimba na kufuatilia kaya hatarishi 80 ambapo watu 1,432 walifanyiwa uchunguzi na kati yao 1,307 sawa na asilimia 91 walipewa kinga tiba na wagonjwa wapya 28 kuibuliwa na kuanza matibabu. |
| 240. | Utekelezaji wa Kampeni ya Usichukulie Poa | Kuimarisha Huduma bora za Hali ya Afya na Usafi wa Mazingira kwa jamii ili | | 14,289,557,076 | Kaya zenye vyoo bora zimeongezeka kutoka asilimia 46 Julai, 2016 hadi asilimia 63.4 Desemba, 2019, na kaya |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | Nyumba Ni Choo ili kupunguza kaya zisizokuwa na vyoo nchini. | kupunguza kiwango cha kaya, taasisi na maeneo ya jumuiya zisizokuwa na vyoo nchini kwa kuhimiza ujenzi na matumizi bora ya vyoo katika jamii, taasisi na maeneo yenye mikusanyiko. | | | zisizokuwa na vyoo imepungua kutoka asilimia 7.5 hadi asilimia 1.9 Desemba, 2019. |
| 241. | Mapambano dhidi ugonjwa wa dengue na magonjwa yaenezwayo na wadudu dhurifu | | | 120,000,000 | Ununuzi wa Fogging Machine 4 na dawa za udhibiti wa Malaria, Dengue na magonjwa yaenezwayo na wadudu dhurifu ulifanyika ambapo fogging mashine 2 ziligawiwa kwa Mkoa wa Dar es Salaam, Tanga mashine 1 na Dodoma mashine 1. Aidha, ugonjwa wa Dengue umepungua kutoka wagonjwa 700 mwezi Julai hadi wagonjwa wanne Mwezi wa Septemba 2019 na kuanzia mwezi Oktoba 2019 hadi Desemba 2019 hakuna tukio lolote la ugonjwa wa Dengue liliotolewa taarifa hapa nchini. |
| 242. | Kupunguza pengo kati ya mahitaji na watumishi waliopo katika Sekta ya Afya. | Kuajiri wataalamu zaidi wa afya kutoka ndani na nje ya nchi pamoja na kuboresha mazingira ya kazi kwa lengo | 664,454,000,000 | | Idadi ya Watumishi walioajiriwa imeongezeka kutoka 9,345 mwaka 2014 hadi 12,160 mwaka 2019 sawa na ongezeko la asilimia 30. |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | la kuongeza ubora wa huduma za afya | | | |
| 243. | Huduma za Dawa, Vifaa, Vifaa Tiba na Vitendanishi. | • Kuimarisha upatikanaji wa Dawa, Vifaa, Vifaa Tiba na Vitendanishi<br>• Bohari ya Dawa itakamilisha ujenzi wa maghala ya kisasa ya kuhifadhia dawa katika mikoa ya Tanga, Tabora, Mtwara na Dar es Salaam. | 440,000,000,000.00 | 1,381,945,415,641.00 | • Ongezeko la bajeti ya dawa la shilingi bilioni 239 kutoka bilioni 31 mwaka 2015/16, hadi kufikia bilioni 270 mwaka 2018/19;<br>• Ongezeko la upatikanaji wa dawa muhimu katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini kufikia asilimia 94.4 mwaka 2018/19 kutoka asilimia 36 mwaka 2015/16.<br>• Upatikanaji wa dawa za UKIMWI (ARVs) zinapatikana kwa asilimia 89, dawa za Kifua Kikuu (TB na Leprosy) asilimia 62, Chanjo na Malaria (ALU) zinapatikana kwa asilimia 100 ndani ya maghala ya Bohari ya Dawa (MSD) na katika vituo vya kutolea huduma za afya;<br>• Jumla ya magari 181 yalinunuliwa na Serikali kwa ajili ya usambazaji wa dawa nchini;<br>• Bohari ya Dawa (MSD) imekamilisha ujenzi wa maghala ya kisasa ya kuhifadhia dawa katika mikoa ya Tanga, Tabora, Mtwara na |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | Dar es Salaam;<br>• Kuimarika kiutendaji kwa Bohari ya Dawa na kuweza kudhaminiwa na nchi za SADC kununua dawa kwa niaba yao;<br>• Kusambazwa katika Halmashauri zote nchini lita 239,020 za viuadudu (biolarvicides) vya kuangamiza viluwiluwi vya mbu katika maeneo ya mazalia;<br>• Kununuliwa mashine za X-ray 11 za kidigitali ambazo zimesambazwa katika hospitali za Ruvuma, Chato, Morogoro, Simiyu, Magu, Singida, Nzega, Njombe, Bukoba, Amana na Katavi;<br>• Mikoa yote nchini inatekeleza ununuzi wa dawa, vifaa na vifaa tiba kwa mfumo wa Mshitiri (Prime Vendor); na<br>• .Hadi Desemba 2019, Bohari ya Dawa imesambaza dawa, vifaa tiba na vitendanishi vya maabara ambapo asilimia 99 ya vituo vyote vya umma vya kutolea huduma za Afya vimesambaziwa dawa na vifaa tiba |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | muhimu kwa kutumia Mfumo wa ugavi ujulikanao kama Ugavi Shirikishi. |
| 244. | | Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba itaimarika kiutendaji na kuhakikisha dawa na vifaa tiba vyenye Ubora vinapatikana | | | • Kuimarika kiutendaji kwa Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba na kufikia ngazi ya tatu kiukomavu (maturity level three) na kuwa taasisi pekee Barani Afrika kufikia ngazi hiyo. |
| 245. | | Serikali itaendelea kushirikisha Sekta Binafsi kuwezesha upatikanaji wa dawa pale zinapokosekana katika Bohari ya Dawa | | | • Bohari ya Dawa kuingia mikataba ya moja kwa moja na wazalishaji wa dawa ambapo mpaka mwishoni mwa mwezi Juni, 2019, Bohari ya Dawa ilikuwa imeingia mikataba ya muda mrefu (Framework Agreement) na jumla ya wazalishaji 128, kati yao 17 wakiwa ni wazalishaji wa ndani. Hii imewezesha kushuka kwa bei za baadhi ya dawa kwa asilimia 40. |
| 246. | Kuimarisha Vyuo vya Mafunzo ya Afya. | Kuendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya vyuo vya afya vilivyo chini ya Wizara ya Afya | 1,600,000,000.00 | 0 | Kumalizia ujenzi wa chuo kipya cha afya mkoani Tabora ambacho kwa mwaka wa masomo 2019/2020 kimeanza kudahili wanafunzi. |
| 247. | Kuongeza udahili katika vyuo vya mafunzo ya Afya | Kuongeza udahili katika vyuo vya afya kufikia idadi wanafunzi | | | Kuimarika kwa ushirikiano kati ya Serikali na Sekta Binafsi ambapo kumepelekea kuongezeka kwa idadi ya |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | 15,000 ifakapo mwaka 2020 | | | wanafunzi waliodahiliwa kwenye vyuo vya afya kutoka 8,642 mwaka 2015 mpaka 18,539 mwaka 2018 sawa na asilimia 123.6 ya lengo la wanafunzi 15000 ifikapo 2020. |
| 248. | Kuimarisha Afya ya Msingi kwa Matokeo (Primary Healthcare for Results.(PHC4R) | Kuimarisha huduma ya afya ya msingi kwa kuzingatia zaidi huduma ya afya ya mama na mtoto. | | | • Vituo 6,993 kati ya 8119 vimefanyiwa tathmini ya awali (mwaka 2016/17) kwa vituo vya kutolea huduma ya afya ya msingi sawa na asilimia 86.1 ambapo Vituo 2,399 (asilimia 34) vilipata nyota sifuri, Vituo 3,588 (asilimia 51) nyota moja, Vituo 869 (asilimia 13) vilipata nyota mbili, Vituo 131 (asilimia 2) vilipata nyota tatu na Vituo 6 (asilimia 0.07) vilipata nyota nne;<br>• Vituo 7,289 vilifanyiwa tathmini ya marudio mwaka 2017/18 ambapo Vituo 456 (asilimia 6) vilipata nyota sifuri, Vituo 2,396 (asilimia 33) vilipata nyota moja, Vituo 3,067 (asilimia 42) vilipata nyota mbili, Vituo 1,276 (asilimia 18) vilipata nyota tatu na Vituo 94 (asilimia 1) vilipata nyota nne. Hii inaonyesha kuwa ubora wa huduma za afya kwa |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | mwaka 2017/18 uliongezeka ukilinganisha na mwaka 2016/17;<br>• Jumla ya wajumbe 245 wa timu za Uendeshaji wa Huduma za Afya za Mikoa (RHMTs) na Halmashauri (CHMTs) walipatiwa mafunzo ya nyenzo za ufuatiliaji wa mpango kazi; na<br>• Wizara imetoa mafunzo kwa watumishi 1,020 na kusambaza Mwongozo mpya wa Kitaifa wa Kukinga na Kudhibiti Maambukizo katika Vituo vya Kutolea Huduma za Afya katika mikoa ya Mwanza watumishi 98, Kagera 81, Dar es Salaam 210, Kigoma 85, Katavi 66, Rukwa 61, Pwani 98, Njombe 65, Mbeya 82, Songwe 77 na Dodoma 97. |
| 249. | Uanzishaji wa Huduma za Tiba za Dharura (Emergency Medical Services) | Kuanzisha tiba za dharura katika majaribio katika barabara ya Morogoro katika mikoa mitatu ambayo ni Morogoro, Pwani na Dar es Salaam | 2,500,000,000 | 11,000,000,000 | • Vituo saba vitakavyotoa huduma vimeainishwa (hot spot) ambavyo ni Kimara, Tumbi, Chalinze, Morogoro, Mikumi, St. Kizito na Ruaha Mbuyuni ambapo ujenzi wa vituo upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji; |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | • Mtambo wa mawasiliano utakaotumika kuendesha Ambulence umenunuliwa ili ukishasimikwa huduma zianze kutolewa;<br>• Watoa huduma 538 wa kada mbalimbali wamepata mafunzo; na<br>• Magari 14 ya kubeba wagonjwa wakati wa ajali na dharura yamenunuliwa. |
| 250. | East Africa Public Health Laboratory-Strengrhen Ebola Preparedness | Kuimarisha utayari wa kukabiliana na ugonjwa wa Ebola iwapo utaingia nchini ikiwa ni pamoja na hatua za kugundua, kupima na kumhudumia mgonjwa katika eneo maalum ili kuepusha kusambaa kwa ugonjwa**.** | | 23,000,000,000 | • Kukamilika kwa Ujenzi wa Maabara ya Hospitali ya Rufaa Kifua Kikuu (Kibong'oto);<br>• Kukamilika kwa Ujenzi wa Maabara ya Hospitali ya Rufaa ya Ndanda;<br>• Maabara tatu za hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Mbeya, Taasisi ya Utafiti Kilimanjaro (KCRI) na Maabara ya Taifa zimeboreshwa na kuongezewa uwezo wa kupima Ebola;<br>• Kuanzishwa kwa *Mobile laboratory*;<br>• Kukamilika kwa Ujenzi wa Maabara Kuu ya Afya ya Jamii;<br>• Watoa huduma 50 wa kada mbalimbali wamepewa mafunzo |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | yenye lengo la kuongeza uwezo katika kutambua, kupima na kutoa taarifa;<br>• Vituo vinne vya kuhudumia wagonjwa wa magonjwa ya kuambukiza (infectious disease) vimejengwa katika mikoa ya Kilimanjaro (Mawenzi), Mwanza (Ilemela) na Dar es Salaam (Temeke na Muhimbili);<br>• Vituo vya mpakani 45 vimeboreshwa ili kuweza kutambua wasafiri wenye viashiria hatarishi vya magonjwa hatarishi;<br>• *Thermoscanners* 115 zimenunuliwa na kufungwa katika mipaka ya nchi;<br>• Watumishi 50 wameajiriwa na kupangiwa kufanya kazi Vituo vya Mipakani ili kujenga uwezo wa kufuatilia watu wote wanaoingia na kubaini wenye viashiria vya hatari;<br>• Elimu ya afya kwa umma imetiliwa mkazo kwa kuandaa vipeperushi na ujumbe wa kutoa elimu kwa Umma. Wadau mbalimbali ikiwemo katika ngazi ya jamii wameelimishwa ili kuweza kuelimisha jamii kujikinga na |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | kukabiliana na kuripoti mgonjwa yoyote mwenye viashiria vya magonjwa hatari;<br>• Vifaa na madawa muhimu vya kukabiliana na ugonjwa wa Ebola vimenunuliwa na kuwekwa katika Mikoa na Wilaya hususani katika mikoa kumi hatarishi; na<br>• Watumishi 350 walipewa mafunzo katika Mikoa yenye hatari ya kupata wagonjwa wa Ebola. |
| 251. | Ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii. | Kuboresha majengo na miundombinu ya kujifunzia na kufundishia katika vyuo vya maendeleo ya Jamii. | 220,000,000.00 | - | • Kukamilika kwa ukarabati wa hosteli, kumbi za mihadhara, majengo ya utawala na nyumba za watumishi katika vyuo vya maendeleo ya jamii vya Rungemba, Mlale, Misungwi, Monduli, Mabughai, Ruaha, Buhare na Uyole;<br>• Kukamilisha ujenzi wa eneo la kufulia nguo katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Mlale;<br>• Kukamilisha mfumo wa maji safi katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Buhare;<br>• Kukamilisha ujenzi wa maktaba katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamii |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | Tengeru;<br>• Kukamilika kwa ukarabati wa hosteli na choo kimoja katika Chuo Maendeleo ya Jamii Ruaha;<br>• Kukamilika kwa Ukarabati wa vyoo na mabafu katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Misungwi;<br>• Kukamilika kwa Ukarabati wa miundombinu ya umeme, *partition* kwa ajili ya bweni la wanaume, na bwalo na kuanzishwa kwa Kituo cha Kidigitali cha Ubunifu katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Misungwi;<br>• Kukamilikwa kwa karabati wa nyumba nne za watumishi, hosteli ya wasichana, maktaba na kuzungushia ukuta choo cha wasichana) katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Monduli;<br>• Kukamilika kwa ujenzi wa Maktaba katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Uyole; na<br>• Kuanzishwa kwa vituo sita vya Kidigitali vya Ubunifu katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru na Vyuo vya Maendeleo ya Jamii vya |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | Monduli, Rungemba, Buhare, Ruaha na Misungwi. Vituo hivi vitawezesha kuibua na kukuza mawazo na vipaji vya kibunifu miongoni mwa wanafunzi na jamii ili waweze kuchangia katika maendeleo ya Taifa kwa kuzalisha teknolojia zinazohitajika katika maendeleo ya viwanda, usindikaji wa mazao na bidhaa mbalimbali ili kuongeza mnyororo wa thamani. |
| 252. | Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi | Kuimarisha utoaji wa mikopo yenye masharti nafuu kwa wanawake wajasiriamali. | 45,289,579,189.00 | | • Jumla ya Shilingi 43,889,299,598.19 kutoka katika asilimia 4 ya mapato ya ndani ya Halmashauri zimetolewa kama mikopo yenye masharti nafuu kwa vikundi 21,743 vyenye wanawake wajasiriamali 892,599 katika Halmashauri mbalimbali nchini.<br>• Jumla ya wanawake wajasiriamali 17,306 kutoka katika mikoa 26 ya Tanzania Bara wamewezeshwa mitaji yenye masharti nafuu yenye thamani ya Shilingi 5,636,500,000.00 kupitia Madirisha ya Wanawake yaliyoanzishwa katika Benki ya Posta Tanzania. |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | • Wanawake wajasiriamali 13,566 waliwezeshwa kushiriki Maonesho ya Biashara ya Kitaifa na Kimataifa ikiwemo maonesho ya Sabasaba na mifuko na program za uwezeshaji wananchi kiuchumi. |
| 253. | Uingizaji wa masuala ya jinsia katika sera na mipango | Kuingiza masuala ya kijinsia katika Sera, Mikakati, Mipango na Bajeti za Kisekta | | 457,048,839.00 | • Wawakilishi 881 kutoka katika Wizara, Wakala na Idara za Serikali walipatiwa mafunzo kuhusu uingizaji wa masuala ya jinsia katika mipango ya maendeleo;<br>• Jeshi la Magereza Tanzania limezindua Dawati la Jinsia pamoja na Mtandao wa wanawake wa Jeshi la Magereza. 162; na<br>• Madawati ya Jinsia na Watoto matatu yameanzishwa katika vituo vya polisi vya mbweni, kimara na mburahati na kufanya madawati ya Jinsia na Watoto yaliyoanzishwa katika vituo vya polisi kufikia 420.<br>• Kununuliwa na kusambazwa kwa pikipiki 29 kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri ya Mpanda (15) - Mkoa wa Katavi na |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | Halmashauri ya Chamwino (14) – Jiji la Dododma. |
| 254. | Uhai na Maendeleo ya Mtoto. | Vitendo vya ukatili dhidi ya watoto kupunguzwa hadi kufikia asilimia 50% ifikapo Juni 2021. | 315,484,630 | 1,086,726,642 | • Katika kuhakikisha vitendo vya ukatili dhidi ya watoto vinatokomezwa, Mwongozo wa kutoa elimu ya malezi chanya kwa wazazi na walezi umeandaliwa. Mwongozo huu umetumika kutoa mafunzo kwa watu 546 wakiwemo wazazi, walezi, walimu na waandishi wa habari katika mikoa ya Kilimanjaro, Kigoma, Shinyanga, Katavi, Songwe, Ruvuma, Mwanza, Mbeya, Iringa, Njombe, Mara, Tabora, Dodoma, Singida na Dar es Salaam;<br>• Vikundi vya malezi 2,384 vimeanzishwa katika mikoa 18 ya Arusha, Geita, Kagera, Kigoma, Kilimanjaro, Mara, Morogoro, Mwanza, Pwani, Rukwa, Ruvuma, Shinyanga, Simiyu, Songwe, Dar es Salaam, mbeya, Tanga na Tabora ili kutoa elimu kuhusu malezi kwa watoto na kuzuia ukatili kwa watoto; na |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | • Wadau 600 walihusika katika kufanya mdahalo wa Kitaifa wa kujadili masuala ya Ukatili dhidi ya watoto ikiwemo ukeketaji na mimba za utotoni.<br>• Mkutano Mkuu wa uchaguzi wa Baraza la Watoto la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania umefanyika Mkoani Singida. Wawakilishi wa watoto kutoka mikoa 29 walishiriki kuchagua viongozi. Aidha, Mabaraza ya Watoto na klabu za watoto shuleni zimeanzishwa ili kuwezesha watoto kutoka maoni yao juu ya mambo yanayowahusu ambapo jumla ya mabaraza ya watoto 1,669 yameanzishwa na klabu za watoto shuleni 2,475.<br>• Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto umeandaliwa na umewezesha kuanzishwa kwa jumla ya kamati 11,520 za ulinzi wa wanawake na watoto kuanzia ngazi ya kijiji/mtaa hadi ngazi ya mkoa; na<br>• Huduma ya simu ya bure namba 116 |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | kwa ajili ya kutoa taarifa za ukatili dhidi ya watoto imeratibiwa ambapo jumla ya **watoto 6,877** wamewezeshwa kupata huduma za kisheria, afya, elimu na unasihi kupitia namba 116. |
| 255. | Huduma za Ustawi wa Jamii | Kuendelea kutoa huduma za ulinzi na maendeleo ya mtoto kwa watoto walio katika mazingira hatarishi<br>Kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia katika Taasisi ya Ustawi wa Jamii. | 1,250,434,000.00 | 1,388,372,570.33 | • Kutekeleza Programu ya Kuwatambua Watu wa Kuaminika ili waweze kuwalea watoto walio katka mazingira hatarishi. Watu wa Kuaminika huchaguliwa na wanajamii katika eneo husika ili kulea watoto walio katika mazingira hatarishi hususan watoto yatima. Tangu kuanza kwa programu hii, jumla ya Watu wa Kuaminika 295 walitambuliwa; na<br>• Vilevile, idadi ya watoto waliolelewa na watu wa kuaminika imefikia watoto 527.<br>• **Kukamilika** kwa ukarabati wa makazi ya wazee katika makazi ya wazee ya Kilima, Nunge pamoja na ujenzi wa bweni katika makazi ya Wazee Kolandoto; na |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | • Ujenzi wa maktaba ya kisasa *(Information resource center)*, ukarabati wa miundombinu ya majengo mbalimbali ikiwemo kubadilisha vyumba vya ofisi kuwa madarasa yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 116 kwa wakati mmoja na kuweka samani kwenye chumba cha maabara ya kompyuta na kukarabati mfumo wa umeme na maji taka na ukarabati wa eneo la uzio katika Taasisi ya Ustawi wa Jamii Kijitonyama. |
| **JUMLA NDOGO** | | | **1,473,782,611,595.00** | **2,177,768,572,909.39** | |
| **WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** | | | | | |
| 256. | Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu (Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo katika Sekta ya Elimu - EP4R) | Kuimarisha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa kufanya ukarabati na ujenzi wa miundombinu katika shule za msingi na Sekondari katika mikoa 26 ya Tanzania Bara | - | 144,930,458,408.92 | • Jumla ya Shule 1,420 (Msingi 709 na Sekondari 711) zimejengewa miundombinu ambapo madarasa 2,898, matundu ya vyoo 6,629, mabweni 535, nyumba za walimu 61, mabwalo 76, majengo ya utawala 16, maabara 6, maktaba 1, uwekaji wa maji shule 15 na uzio shule 3 yamejengwa katika Mikoa yote 26 ya Tanzania Bara.<br>• Kununuliwa kwa magari 39 na |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | kusambazwa katika vyuo vyote vya ualimu vya Serikali. |
| 257. | | • Kuimarisha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji kwa kukarabati vyuo ambapo awamu ya kwanza ilihusisha vyuo 10 na awamu ya pili ilihusisha vyuo 7 vya Ualimu na kujenga upya chuo cha Ualimu Murutunguru ili kuboresha mazingira ya utoaji wa Elimu. | | 24,093,094,719.76 | • Ukarabati wa miundombinu ya kufundishia na kujifunzia pamoja na mabweni katika vyuo 10 vya Ualimu umekamilika. Vyuo vilivyokarabatiwa ni Morogoro, Mpwapwa, Butimba, Kasulu, Songea, Tukuyu, Marangu, Kleruu, Korogwe na Tabora.<br>• Ukarabati wa vyuo 7 vya Ualimu upo katika hatua mbalimbali. Vyuo vinavyokarabatiwa ni Tandala, Nachingwea, Tarime, Kinampanda, Mandaka, Patandi na Ilonga<br>• Chuo cha Murutunguru kinajengwa upya kufuatia taarifa ya Wahandisi kubaini kuwa chuo hicho kimechakaa na hakifai kufanyiwa ukarabati |
| 258. | | • Kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia kwa kufanya ukarabati wa shule Kongwe za Sekondari 62. | | 47,171,739,672.39 | • Shule Kongwe za Sekondari 20 zimekamilika.<br>• Shule Kongwe za Sekondari 18 ziko katika hatua ya ukamilishwaji<br>• Shule Kongwe za Sekondari 24 zimefanyiwa tathmini tayari kwa ajili ya kuanza ukarabati |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| 259. | | • Kuimarisha ufundishaji wa masomo ya Sayansi (Fizikia, Kemia na Bailojia) kwa vitendo kwa kununua Kemikali na vifaa vya maabara kwa shule za sekondari 1,696. | | 16,921,654,847.87 | • Vifaa vya Maabara kwa Masomo ya Fizikia, Kemia na Baolojia vimenunuliwa na kusambazwa katika shule za Sekondari 1,696 Tanzania Bara. Kati ya shule hizi, shule 1,625 ni za Wananchi (Maarufu kama Shule za Kata) na 71 ni shule Kongwe. Shule hizi za kata ni jumla ya shule zote zilizokuwa zimekamilisha ujenzi wa Maabara hadi kufikia Desemba 31, 2016. |
| 260. | | • Kununua vifaa vya TEHAMA ili kuimarisha matumizi vifaa yake katika kufundisha na kujifunza katika vyuo vya ualimu 10 vilivyokarabatiwa. | | 745,061,440.00 | • Vifaa vilivyonunuliwa ni Laptop 2 kwa kila chuo, Desktop top 30 na Ups kwa vyuo 7, Projector 2 kwa kila chuo. Vyuo vilivyonufaika ni Morogoro, Mpwapwa, Butimba, Kasulu, Songea, Tukuyu, Marangu, Kleruu, Korogwe na Tabora. |
| 261. | | • Kuimarisha ufundishaji wa masomo ya sayansi kwa vitendo kwa kununua vifaa vya maabara kwa vyuo 9. | | 1,498,588,842.50 | • Vyuo vilivyopatiwa vifaa vya maabara ni Morogoro, Mpwapwa, Butimba, Kasulu, Songea, Tukuyu, Kleruu, Korogwe na Tabora. Vi |
| 262. | | • Kuimarisha Ari ya ufundishaji kwa walimu kwa kulipa madeni ya walimu yasiyo ya | | 33,134,512,584 | • Madai ya walimu 86,234 yasiyo ya mishahara yamelipwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2015/2016 na 2016/2017. Katika kipindi cha |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | Mishahara. | | | mwaka wa fedha 2015/2016 hadi kufikia mwezi Juni, 2016 jumla ya shilingi bilioni 22,629,352,309 zililipwa kwa walimu 63,814 na katika kipindi cha mwaka wa fedha 2016/17 hadi kufikia mwezi Machi, 2017 jumla ya shilingi bilioni 10,505,160,275 zimelipwa kwa walimu 22,420. |
| 263. | | • Kuimarisha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa kujenga upya shule ya Sekondari Ihungo baada ya kuathirika na tetemeko. | | 10,488,414,429.00 | • Ujenzi wa madarasa yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 960, mabweni ya wanafunzi yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,152, vyoo na mabafu katika eneo la madarasa na mabweni pamoja na uwekaji wa mfumo maji taka na maji safi umekamilika.<br>• Aidha ujenzi wa nyumba 30 za walimu upo katika hatua za ukamilishwaji. |
| 264. | | • Kumalizia jengo la Utawala *Phase II stage I* la Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam | | 1,150,000,000.00 | • Ujenzi umekamilika ambapo jengo linauwezo kuchukua wahadhiri 63 kwa kuanzia. |
| 265. | | • Kuboresha mazingira ya | | | • Halmashauri zimelipwa jumla ya |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | kufundishia na kujifunzia kwa kutuma fedha za Motisha kwa Halmashauri zote, kulingana na utekelezaji wa vigezo vilivyokubalika. | | 111,220,189,922.55 | shilingi 15,532,905,100.98 katika mwaka 2016 shilingi 22,360,574,170.58 katika mwaka 2017, shilingi 40,093,582,371.20 mwaka 2018 na shilingi 33,233,128,279.79 mwaka 2019.<br>• Fedha hizo hutumika katika uboreshaji wa miundombinu ikiwemo ujenzi, ukarabati na umaliziaji wa miundombinu ikiwa ni pamoja na madarasa, maabara, usawazishaji wa ikama ya Walimu ndani ya Halmashauri, uimarishaji wa mfumo wa ukusanyaji wa Takwimu za shule pamoja na ununuzi wa madawati. |
| 266. | | • Kuimarisha miundombinu ya elimu ya Msingi | | 35,249,600,000.00 | • Ukamilishwaji wa maboma 2,815 katika shule za Msingi 2,134 katika Halmashauri zote nchini upo katika hatua mbalimbali za ukamilishwaji. |
| 267. | | • Kuimarisha ubora wa elimu ya Msingi na Sekondari kwa kuboresha na kuchapa Vitabu vya shule ya Msingi na Sekondari. | | 8,650,333,846.00 | • Vitabu vya kiada Darasa I – V vimechapwa na kusambazwa kwa uwiano wa 1:3 (isipokuwa Darasa la IV uwiano wa 1:1),<br>• Vitabu vya Darasa la VI vipo hatua ya uchapaji na |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | • Vitabu vya Sekondari viko katika hatua ya uhakiki kisha uchapaji.<br>• Viongozi vya mwalimu kwa masomo ya I – V vimechapwa na kusambazwa. |
| 268. | | • Kuimarisha ufundishaji kwa vitendo kwa kununua vifaa vya maabara kwa ajili ya Chuo Kikuu cha Dodoma. | | 3,000,000,000.00 | • Manunuzi yamekamilika na vifaa hivi vinatumika. |
| 269. | | • Kuimarisha ufundishaji na kwa kugharamia Vifaa vya Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum vilivyonunuliwa na OR – TAMISEMI | | 2,150,590,672.58 | • Manunuzi yamekamilika na vifaa hivi vinatumika. |
| 270. | | • Kuimarisha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji kwa kununua vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika chuo cha MUHAS. | | 58,100,000.00 | • Vifaa mbalimbali vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu vimenunuliwa na kusambazwa. |
| 271. | | • Kuimarisha mfumo wa | | 5,824,695,514.58 | • Magari 54 yamenunuliwa na |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | ufuatiliaji na tathmini kwa kununua magari 54 | | | kusambazwa kwa ajili ya kuimarisha Uthibiti Ubora wa Shule na ufuatiliaji na tathmini. |
| 272. | | • Kuimarisha mazingira ya utendaji kazi kwa kujenga ofisi 100 za Wathibiti Ubora wa Shule za Wilaya | | 15,203,265,000.00 | • Ujenzi wa Ofisi za Wathibiti Ubora unaendelea katika Wilaya 100 Tanzania Bara. Hadi kufikia Septemba 30, 2019 ujenzi ulikuwa katika hatua mbalimbali ikiwemo Boma1, Lenta 3, Ukamilishaji 69 na Upauaji 6. Aidha, ofisi 21 zimekamilika. |
| 273. | | • Kuimarisha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa kukarabati shule ya Sekondari Bukoba baada ya kuathirika na upepo | | 1,148,701,194.33 | • Eneo la ufundishaji limekamilika na wanafunzi wa kidato cha 1-4 wanatumia, aidha wanafunzi wa kidato cha 5-6 wanarudi baada ya ukamilishwaji wa bwalo na hotel;<br>• Ujenzi wa upanuzi wa bwalo na ukarabati wa hostel unaendelea; na<br>• Wanafunzi wa Kidato cha 1-4 wamesha upo katika hatua za ukamilishwaji. |
| 274. | | • Kuongeza ari ya ufundishaji na ujifunzaji kwa walimu na wanafunzi | | 2,918,356,500.00 | • Kutoa motisha kwa shule za msingi na sekondari mwaka 2017, 2018 na 2019. Aidha, fedha hizo hutumika katika ununuzi wa zana na vifaa vya kufundishia na kujifunzia |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| 275. | | • Kuimarisha utendaji kazi wa Vyuo vya Ualimu kwa kununua magari 39 | | 3,432,925,959.32 | • Kulipa jumla ya shilingi 3,432,925,959.32 kwa ajili ya ununuzi wa Prado 3, Land cruiser 35 na Costa 1. |
| 276. | | • Ujenzi wa shule maalum ya Sekondari Patandi yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 640 | | 2,300,000,000.00 | • Ujenzi wa madarasa 4, jengo la utawala, bwalo, jiko, chumba cha maabara, chumba cha TEHAMA, maktaba na bweni moja la wasichana viko katika hatua za mwisho za ukamilishwaji;<br>• Madarasa 8 na ofisi 4 ziko katika hatua ya kupauliwa, kupigwa plasta na dali; na<br>• Mabweni 2 yako katika hatua ya kuezekwa na bweni 1 liko katika hatua ya renta. |
| 277. | | • Kuongeza ufanisi katika utoaji wa elimu bora kwa kuongeza idadi ya Wanataaluma | | 920,449,130.00 | • Kutoa mafunzo kwa wanataaluma 76 wa Shahada ya Uzamili na Uzamivu. |
| 278. | | Kusomesha wahadhiri wa MUHAS | | 1,536,000,000.00 | • Wanataaluma 300 wamepatiwa mafunzo katika ngazi ya masomo ya uzamili (ubingwa) chuo cha MUHAS |
| 279. | | Kuimarisha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji kwa kujenga Kafeteria | | 700,000,000.00 | • Ujenzi wa jengo la kafeteria lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 400 limekamilika. |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | kwenye mabweni mapya ya Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine | | | |
| 280. | | Ujenzi wa Hosteli ya Chuo Kikuu cha Mzumbe | | 6,530,120,000.00 | • Mradi unahusisha ujenzi wa mabweni ya wanafunzi ambayo ni majengo manne (Block-A, Block B, Block C na Block D) yakiwa na ghorofa tatu kila moja. Kwa ujumla majengo haya yanauwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000. utekelezaji unaendelea ambapo:<br>• **Jengo A:** Maandalizi ya kuweka mirunda na sahani kwa ajili ya kumwaga zege ghorofa ya tatu. Aidha, Mkandarasi amekamilisha ufungaji wa fremu za milango ya ndani katika "floor' ya chini.<br>• **Jengo B:** Kumalizia kusuka nondo kwa ajili ya kumwaga zege ghorofa ya pili.<br>• **Majengo C & D:** Maandalizi ya kumwaga katika nguzo za ghorofa ya pili kwa ajili ya kujenga ghorofa ya tatu.<br>**Majengo A, B, C & D:** Kazi ya |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | kupiga plasta kwenye kuta za ndani za “floor” chini zimekamilika isipokuwa vyooni. |
| 281. | | Kuimarisha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji kwa kukarabati hosteli namba 2 na 5 za wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es salaam zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 788 (392 kwa bweni Na. 2 na 396 kwa bweni Na. 5) | | 4,974,927,263.72 | • Mradi umekamilika kwa asilimia 72. Kazi zilizokamilika ni pamoja na:<br>✓ Ubomoaji wa mifumo ya zamani ya majisafi na majitaka, kuta za mbao, makabati, meza za kusomea, milango na mifumo ya zamani ya umeme;<br>✓ Usafishaji wa nondo pamoja na kuzipaka *‘red oxide’* na usafishaji wa kuta za ndani na nje;<br>✓ Uandaaji wa vyumba vya mfano *(sample rooms)* ambavyo vimeidhinishwa na CKD;<br>✓ Kurudishia zege lililoondolewa ili kusafisha nondo;<br>✓ Kujenga mifumo ya maji safi na maji taka;<br>✓ Kuweka ‘frem’ za madirisha na milango;<br>✓ Kuweka mifumo ya umeme; na<br>✓ Kubomoa vigae vya ukutani na kuweka vigae vipya.<br>• Kazi ambazo zinaendelea: |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | ✓ Utengenezaji wa vizuizi vya mwanga wa jua; na<br>✓ Utengenezaji wa makabati na milango. |
| 282. | | Kuboresha ufundishaji na ujifunzaji katika kampasi ya Mloganzila | | 13,324,708,249.55 | • Mradi unajumuisha ujenzi wa hosteli zitakazochukua wanafunzi 1,370, ujenzi wa maktaba, kafeteria, madarasa, ukumbi wa mihadhara na jengo la utawala. |
| 283. | | • Kuimarisha ufuatiliaji na tathmini katika ngazi za Sekretarieti za Mikoa na idara ya elimu OR – TAMISEMI kwa kugharimia ununuzi wa magari. | | 5,136,077,069.65 | • Jumla ya shilingi bilioni 3.4 zimelipwa kwa ajili ya manunuzi ya Magari 30 na shilingi bilioni 1.7 zilipwa kwa jili tozo mbalimbali za ugomboaji wa magari.<br>• Kusambazwa kwa magari 30 katika ofisi za mikoa yote 26 Tanzania bara. |
| 284. | | • Ujenzi wa jengo la maabara -MUCE | | 2,153,127,897.14 | • Kazi ya ujenzi imefikia asilimia 45. Kazi zinazoendelea kwa sasa ni ufungaji wa mbao na uwekaji wa mirunda *(props)* ili kumimina zege la sakafu ya ghorofa ya pili; ufumaji wa vyuma *(steel works)* kwenye sakafu ya pili *(second floor)* na kwenye ngazi; ujenzi wa tofali ili kugawa vyumba kwa sakafu ya chini. |
| 285. | Programu ya | • Kupitia na kuhuisha | | 707,294,112 | • Mapitio ya Programu ya Maendeleo |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) - Kuimarisha Mafunzo ya KKK | programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu (ESDP) ili iendane na Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 na kusambazwa kwa wadau | | | ya Sekta ya Elimu 2016/2017 – 2020/2021 yamekamilika na utekelezaji wake umeanza |
| 286. | | • Kutoa mafunzo kwa walimu wa Elimu ya Awali 16,075, darasa la kwanza hadi la nne 31,966, elimu maalum 2,102 na MEMKWA 1,568 kwa mujibu wa Mtaala ulioboreshwa ili kuwajengea uwezo katika ufundishaji wa Stadi za KKK. | | 36,429,768,014 | • Mafunzo yametolewa kwa walimu wa Elimu ya Awali 16,111, darasa la kwanza hadi la nne 31,966, elimu maalum 2,102 na MEMKWA 1,568 |
| 287. | | • Kununua na kusambaza Mashine za nukta nundu 810, seti 125 za vifaa vya upimaji wa kiafya unaoweza kuathiri ujifunzaji kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum | | 4,037,851,600 | • Ununuzi na usambazaji Mashine za nukta nundu 810, seti 125 za vifaa vya upimaji wa kiafya unaoweza kuathiri ujifunzaji kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum umekamilika. |
| 288. | | • Kujenga uwezo kwa | | 2,244,655,165.67 | • Mafunzo ya kujenga uwezo |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | watumishi wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Tekonolojia makao makuu ili waweze kuongeza ufanisi katika kuratibu mradi wa LANES; uchapaji na usambazaji wa PLSE | | | yametolewa kwa watumishi wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Tekonolojia makao makuu ili waweze kuongeza ufanisi katika kuratibu mradi wa LANES; pamoja na uchapaji na usambazaji wa vitabu vya tathmini ya PLSE |
| 289. | | • Kuandika na kusambaza vitabu vya kiada kwa ajili ya wanafunzi wasioona na wenye uono hafifu | | 140,400,000 | • TET imeandaa na kusambaza vitabu vya kiada darasa III na IV katika maandishi ya nukta nundu (Braille) na maandishi makubwa (large print) kwa wanafunzi wasioona na wenye uono hafifu. (Uwiano wa 1:1) |
| 290. | | • Kuandaa na kuchapa vitabu vya hadithi kwa Darasa la I na la II | | | • Nakala 6,450,000 za vitabu vya Hadithi Darasa la I - II aina 25 zimesambaza (uwiano wa 1:3) |
| 291. | | • Kufunga mfumo wa kompyuta wa kukusanya na kuhifadhi taarifa za wanafunzi (PreM) kuanzia darasa la kwanza hadi la saba katika mikoa yote ili kuweza kufuatilia mwenendo wa wanafunzi | | 2,666,811,808.00 | • Mfumo wa kompyuta wa kukusanya na kuhifadhi taarifa za wanafunzi (PreM) kuanzia Darasa la Kwanza hadi la Saba umekamilika katika mikoa yote ili kuweza kufuatilia mwenendo wa wanafunzi |
| 292. | | • Kuanzisha na kuimarisha 'Reading Corners' kwa | | 865,632,000 | Kona za usomaji (Reading Corners) kwa watoto wadogo zimeanzishwa |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | watoto wadogo kwenye maktaba 43 nchini ili kujenga utamaduni wa kujisomea kwa watoto wadogo | | | katika maktaba 43 nchini ili kujenga utamaduni wa kujisomea kwa watoto wadogo. |
| 293. | | • Kuendesha Matamasha ya Usomaji "Reading Week Festival" katika Maktaba za Mikoa 22 nchini ili kujenga utamaduni wa kujisomea kwa watoto wadogo. | | 310,883,828.80 | Matamasha ya Usomaji "Reading Week Festival" yalifanyika katika Maktaba za Mikoa 22 mwishoni mwa mwaka 2018 na kuzihusisha Shule mbalimbali za Msingi za Serikali katika Mikoa husika. Shughuli hiyo imehamasisha watoto wadogo kupenda kujisomea na kutumia Maktaba za Umma. |
| 294. | | Kutoa Mafunzo kwa walimu wa nyongeza 1,598 wanaofundisha darasa la I na II kwa lengo la kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za KKK | | 1,600,744,227 | Mafunzo yametolewa kwa walimu wa nyongeza 1,598 wanaofundisha darasa la I na II kwa lengo la kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za KKK |
| 295. | | Kutoa mafunzo kwa walimu wa nyongeza 402 wa Elimu Maalum kwa lengo la kuwapa walimu stadi za kufundisha Stadi za KKK kwa wanafunzi wasioona na | | 398,785,000 | Mafunzo yametolewa kwa walimu wa nyongeza 402 wa elimu maalum kwa lengo la kuwajengea uwezo walimu katika ufundishaji na ujifunzaji stadi za KKK kwa wanafunzi wasioona na viziwi wa darasa la I-IV kwa |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | Viziwi wa Darasa la I-IV kutumia mtaala mpya pamoja na watoto wenye Mtindio wa akili na usonji; | | | kuzingatia Mtaala ulioboreshwa. |
| 296. | | Kuwezesha ununuzi wa pikipiki 2,894 kwa ajili ya maafisa elimu kata kwa lengo la kuimarisha usimamizi wa shule | | 8,566,070,201 | Jumla ya pikipiki 2,894 zimenunuliwa kwa ajili ya Maafisaelimu Kata ili kuimarisha usimamizi wa shule’ |
| 297. | | Kuwezesha maandalizi ya kiunzi cha uthibiti ubora wa shule pamoja na zana zake ili kuimarisha mfumo wa uthibiti ubora wa shule | | 1,103,831,364 | Kukamilisha maandalizi ya Kiunzi cha Uthibiti Ubora wa Shule pamoja na zana zake kwa lengo la kuimarisha mfumo wa uthibiti ubora wa shule. |
| 298. | | Kuchapisha Mwongozo wa Uthibiti Ubora wa Shule pamoja na kutoa mafunzo kwa wathibiti ubora wa shule wote ili kuwawezesha kutekeleza kazi zao kwa ufanisi | | 704,321,364 | Uchapishaji na usambazaji wa miongozo ya uthibiti ubora wa shule umekamilika sambamba na utoaji wa mafunzo kwa wathibiti ubora wa shule wote ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi |
| 299. | | Kufanya upimaji wa umahiri wa KKK kwa wanafunzi wa Darasa la II kama sehemu ya tathmini ya mwisho ya Programu | | 529,785,091.76 | • Upimaji wa umahiri wa KKK umefanyika kwa wanafunzi wa darasa la II katika mikoa 11, halmashauri 2 kwa kila mkoa. Uchambuzi wa matokeo ya upimaji unaendelea. |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| 300. | | Kugharamia masomo na tafiti katika masuala ufundishaji na ujifunzaji KKK kwa madarasa ya awali zitakazosaidia kuweka mipango thabiti ya kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji | | 2,145,291,413.86 | Kugharamia wanachuo 15 wa shahada ya uzamili na uzamivu pamoja kukamilisha tafiti nne kuhusu ufundishaji, ujifunzaji na upimaji wa stadi za KKK zitakazosaidia kuweka mipango na mikakati thabiti ya kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za KKK |
| 301. | | Kufanya ufuatiliaji wa pamoja kwa mwaka kwa ajili ya kufanya tathmini ya utekelezaji wa Mikakati ya Sekta ya Elimu. | | 195,455,000.00 | Ufuatiliaji wa pamoja kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo umefanyika mara mbili kwa ajili ya kufanya tathmini ya utekelezaji wa Mikakati ya Sekta ya Elimu kuweka mikakati mipya. |
| 302. | | Kufanya Mapitio/ Maboresho ya mtaala wa elimu ya ualimu ili kuendana na mahitaji ya wakati | | 689,988,885.95 | Kuandaa Mwongozo wa Kitaifa wa Mtaala ambao utakuwa unaongoza zoezi la kuandaa na kuhuisha mitaala nchini kwa ngazi za Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Elimu ya Ualimu;Utekelezaji umefikia silimia 50 |
| 303. | | Kufanya matengenezo kinga kwa magari 38 ya wathibiti ubora wa shule ili kuwezesha utekelezaji wa shughuli za uthibiti ubora wa shule | | 328,501,540 | matengenezo kinga kwa magari 38 ya wathibiti ubora wa shule yamefanyika ili kuwezesha utekelezaji wa shughuli za uthibiti ubora wa shule |
| 304. | | Kuwezesha uchapishaji na | | 11,996,457,379.05 | imekamilisha usambazaji wa vitabu vya |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | usambazaji wa nakala 6,849,000 za vitabu vya Darasa la nne. Vitabu hivi vitasaidia kuleta ufanisi katika ufundishaji wa stadi za KKK kwa kufanya uwiano wa 1:1 kwa darasa la nne | | | kiada nakala 6,201,440 kwa Darasa la Nne (uwiano wa 1:1) masomo ya Hisabati, English, Uraia na Maadili, Maarifa ya Jamii, Stadi za Kazi, Sayansi na Teknolojia na Kifaransa katika Halmashauri za Mikoa 26 ya Tanzania Bara. |
| 305. | | Kuandaa maudhui ya kielektroniki kwa ajili ya wanafunzi wa darasa la I na II ili kuwawezesha kujifunza kwa ufanisi | | 500,000,000 | Imekamilisha maandalizi ya maudhui ya kielektronik na kuanza kurusha hewani kipindi cha Vikaragosi (Cartoons) kupitia TBC – Kipindi cha watoto kiitwacho Nyota Njema (siku ya Jumamosi na Jumapili kuanzia saa 4 asubuhi) kwa ajili ya kukuza stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) kwa wanafunzi wa Darasa la Kwanza na la Pili Utekelezaji umekamilika |
| 306. | | Kufanya Mkutano wa wadau wa kutathimini utekelezaji wa sekta ya Elimu, Sayansi na Teknolojia 2018 (JESR) ili kufanya tathmimini ya pamoja na kuweka maazimio yatakasaidia kukabiliana na changamoto zilizopo katika | | 224,200,000 | Mkutano wa wadau wa kutathimini utekelezaji wa sekta ya Elimu, Sayansi na Teknolojia 2018 (JESR) umefanyika ili kuweka maazimio ya pamoja yatakayosaidia kukabiliana na changamoto zilizopo katika sekta ya elimu |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | sekta ya elimu | | | |
| 307. | | Kununua na kusambaza vifaa vya elimu maalum kwa ajili ya kuhakikisha wanafunzi wenye mahitaji maalum wanajifunza kwa ufanisi. | | 2,346,016,939.00 | Vifaa vimeshanunuliwa taratibu za mapokezi zimeanza wazabuni watalipwa mara baada ya kukamilisha taratibu za mapokezi |
| 308. | Huduma ya Maji, Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira Shuleni (SWASH) | Kufanya ufuatiliaji, tathmini pamoja na ukaguzi wa ujenzi wa miundombinu ya vyoo bora kwenye halmashauri zote zilizopatiwa fedha za Kampeni ya Kitaifa ya Usafi wa Mazingira. | | 195,999,300.00 | Utekelezaji umekamilika ambapo ufuatiliaji na tathmini umefanyika katika shule zilizo katika Halmashauri zinazotekeleza Kampeni ya Kitaifa ya Usafi wa Mazingira Tanzania Bara. Aidha changamoto kama vile upatikanaji wa maji safi na salama pamoja upungufu wa miundommbinu bora ya vyoo shuleni ulibainishwa na ushauri ulitolewa katika Halmashauri husika. |
| 309. | | Kuwajengea uwezo waratibu wa Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira wa ngazi ya Mikoa na Halmashauri, Waheshimiwa Wabunge na Wadau Mbalimbali kuhusu Elimu ya Hedhi Salama Shuleni. | | 86,360,000.00 | Utekelezaji umekamilika kwa asilimia 100 ambapo washiriki 73 wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, Wawakilishi wa Mashirika yasiyokuwa ya kiserikali (NGOs), wawakilishi kutoka vyuo vikuu, asasi za kiraia, Maafisa Elimu wa Mikoa na Wilaya (REOs & DEOs) pamoja na walimu kutoka katika |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | baadhi ya shule Nchini walipata mafunzo hayo. |
| 310. | | Kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji katika utekelezaji wa shughuli za Huduma ya Maji, Elimu ya Afya katika Mikoa na Halmashauri mbalimbali Nchini kwa kutoa mafunzo elekezi ya utumiaji wa mwongozo wa Huduma ya Maji, Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira Shuleni. | | 120,783,500.00 | Utekelezaji umekamilika kwa asilimia 100 ambapo mafunzo ya Mwongozo wa Huduma ya Maji, Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira (*School WASH Guideline*) yametolewa kwa Wathibiti Ubora wa Wilaya kwa Halmashauri 111 (W1) kutoka mikoa ya Mtwara, Lindi, Manyara, Iringa, Dar es Salaam, Morogoro, Singida, Pwani, Njombe, Ruvuma, Mbeya, Songwe, Rukwa, Katavi, Arusha, Dodoma, Tanga, Mtwara, Lindi, Manyara, Iringa, Dar es Salaam, Morogoro, Singida, Pwani na Kilimanjaro. |
| 311. | | Kuimarisha utoaji wa huduma ya maji safi na salama kwa kuweka miundombinu ya maji safi na salama shuleni ili kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia. | | 36,000,000 | Utekelezaji umekamilika kwa asilimia 100 ambapo miundombinu ya Maji Safi na Salama pamoja na vifaa vya kutibu maji ya kunywa kwa ajili ya wanafunzi vimewekwa katika shule za Msingi za Kongowe, Mzinga pamoja na shule yenye watoto wenye mahitaji maalum ya Maweni. |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| 312. | | Kuimarisha ukusanyaji wa takwimu za Huduma ya maji, Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira Shuleni kwa kutoa mafunzo ya mfumo wa kitaifa wa ukusanyaji wa takwimu za Elimumsingi (BEMIS) ili kuweka mipango ya utekelezaji pamoja kutoa taarifa ya hali ya miundombinu ya maji na usafi wa mazingira shuleni kila mwaka. | | 140,000,000.00 | Utekelezaji umekamilika kwa asilimia 100 ambapo mafunzo ya ukusanyaji wa takwimu za Huduma ya Maji, Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira Shuleni kupitia mfumo wa BEMIS yametolewa kwa Maafisa Elimu Vifaa na Takwimu wa Elimu ya Msingi (SLOs) wa Halmashauri zote za Tanzania Bara |
| 313. | Kuboresha Miundombinu ya Ufundishaji na Kujifunzia kwa Vyuo vya Ualimu (UTC) | • Ujenzi na Ukarabati wa Vyuo vya Ualimu vya Ndala, Kitangali, Shinyanga na Mpuguso | 4,040,640,894.94 | 18,083,506,810.38 | • Ndala Lot 1 – Ambayo inajumuisha kazi za Ujenzi wa mabweni mawili ya gorofa moja, Madarasa mawili ya gorofa moja, Jengo la maktaba, Jengo la Maabara, Ukumbi ya mikutano na ujenzi wa majengo mawili ya “Ablution” kwa ajili ya wanawake na wanaume ambapo mradi huu kwa ujumla utekelezaji wake umefikia asilimia 20<br>• Ndala Lot 2 – Ambayo inajumuisha kazi za Ujenzi wa nyumba 2 za wafanyakazi zenye vyumba vinne kila |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | moja, Nyumba 3 za wafanyakazi zenye vyumba vitatu kila moja, Majengo mawili ya gorofa moja kwa ajili ya wafanyakazi, Majenzo mawili ya "Ablution" kwa ajili ya wanawake na wnaume pia kazi ya ukarabati wa mabweni mawili ya wanafunzi wakike na wakiume ambapo kwa ujumla utekelezaji wa mradi huu umefikia asilimia 97<br>• Shinyanga Lot 1 – Ambayo inajumuisha kazi za Ujenzi wa Bweni moja la gorofa moja, Jengo moja la gorofa moja kwa ajili ya wafanyakazi na ujenzi wa ukuta kuzunguka eneo la Chuo. Pia kuna ukarabati wa nyumba mbili za wafanyakazi, nyumba moja ya Mkuu wa Chuo, Bweni moja lenye gorofa mbili kwa ajili ya wasichana na mabweni mawili ya wavulana na wasichana ambapo utekelezaji wa mradi huu kwa ujumla umefikia asilimia 100<br>• Shinyanga Lot 2 – Ambayo inajumuisha kazi za Ujenzi wa bweni moja la gorofa moja, Majengo mawili |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | ya gorofa moja kwa ajili ya madarasa, Jengo la maktaba na ujenzi wa majengo mawili ya "Ablution" kwa ajili ya wanawake na wanaumem na pia kazi za ukarabati wa bweni moja la wavulana, Ukumbi wa chakula na jiko na jengo la utawala lenye madarasa ambapo utekelezaji wa mradi huu kwa ujumla umefikia asilimia 74<br>• Mpuguso Lot 1 - Ambayo inajumuisha kazi za Ujenzi wa mabweni mawili ya gorofa moja kwa ajili ya wanafunzi wakike na wakiume, Nyumba ya vyumba vitatu kwa ajili ya watumishi, Nyumba 3 za gorofa kwa ajili ya watumishi na pia kazi ya ukarabati wa nyumba nne za watumishi ambapo utekelezaji wa mradi huu kwa ujumla umefikia asilimia 100<br>• Mpuguso Lo 2 Ambayo inajumuisha kazi za Ujenzi wa majengo mawili ya gorofa kwa ajili ya madarasa, Jengo la Maktaba, Jengo la Maabara, jengo la ukumbi wa miadhara na ujenzi wa |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | majengo mawili ya "Ablution" kwa ajili ya wanawake na wanaume na pia kazi za ukarabati wa jengo lenye vyoo na mabafu ya wanafunzi ambapo utekelezaji wa mradi huu kwa ujumla umefikia asilimia 67<br>• Ujenzi wa Ukumbi wa mikutano katika Chuo cha Ualimu Mpuguso ambao utekelezaji wake umefikia asilimia 2<br>• Kitangali Lot1 Ambayo inajumuisha kazi za Ujenzi wa nyumba 10 za wafanyakazi zenye vyumba vitatu, nyumba moja ya wafanyakazi yenye vyumba vinne na ukumbi wa mikutano ambapo utekelezaji wake kwa ujumla umefikia asilimia 99<br>• Kitangali Lot2 Ambayo inajumuisha kazi za Ujenzi wa majengo mawili ya gorofa moja kwa ajili ya madarasa, Ujenzi wa majengo mawili ya gorofa moja kwa ajili ya mabweni, jengo la Maktaba, jengo la Maabara, jengo la Kumbi ya mihadhara, Vyoo vitatu vyenye matundu 8 kila kimoja na na ujenzi wa majenzo mawili ya |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | "Ablution" kwa ajili ya wanawake na wnaume ambapo utekelezaji wake kwa ujumla umefikia asilimia 85 |
| 444. | Programu ya Maendeleo Unganishi ya Viwanda (*Integrated Industrial Development Programmes)* | • Kutekeleza Mpango wa kuendeleza viwanda kwa kujenga miundombinu kwa ubia na wadau wa maendeleo (*World Bank, na AfDB)* pamoja na kuvutia wawekezaji; na<br>• Kuwezesha mafunzo ya ubora wa bidhaa kwa wenye viwanda kwa kushirikiana na Shirika la Viwanda la Umoja wa Mataifa - UNIDO. | 600,000,000.00 | | • Maandalizi ya awali ya kufanya *Industrial mapping* (ToR, Action Plan, Desk Research) kwa ajili ya kubaini maeneo ya kujenga viwanda na malighafi adimu *(strategic industrial metals)* ambazo zinatakiwa kulindwa yamekamilika;<br>• Waraka wa kuanzisha *Program for Country Partnership* – PCP umekamilika na kuridhiwa na kikao IMTC tayari kwa kuwasilishwa BLM;<br>• Mradi wa *Industrial Transformation* ambao utazingatia ujenzi wa miundombinu wezeshi ya kuendeleza viwanda umekamilika na upo katika hatua za majadiliano na Wizara ya |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | Fedha na Mipango;<br>• Kukamilika kwa *Analytical Report of Annual Survey of Industrial Production* - ASIP 2015/16 ;<br>• Taarifa za awali kwa ajili ya kuanzisha Kanzidata *(Database)* ya Viwanda imeandaliwa;<br>• Taarifa ya tathmini ya uwezo wa ndani wa ubanguaji wa Korosho na hali halisi ya teknolojia za ubanguaji wa Korosho, uchakataji wa Chikichi na Pamba zimekamilika; na<br>• Maandalizi ya Miradi ya uboreshaji wa mifumo ya uchakataji wa mazao ya kimkakati ya Korosho, Pamba na Chikichi yamekamilika na tayari kujadiliwa na Wizara ya Viwanda na Biashara na Wizara ya Fedha na Mipango kwa hatua ya utekelezaji. |
| 445. | *Tanzania Mini Tiger Plan 2020- Bagamoyo (Bagamaoyo Technology Park & William Benjamin Mkapa SEZ, Mtwara SEZ na Kigoma SEZ).* | • Kukamilisha majadiliano na wawekezaji (CMPort & SGRF) na kuandaa mikataba katika eneo la Bagamoyo SEZ;<br>• Kufanya usanifu wa kina na ujenzi wa Miundombinu ya | 1,123,150,000.00 | | • Rasimu ya *key terms agreement* imekamilika;<br>• Kukamilika kwa rasimu ya Mikataba ya Utekelezaji wa Mradi (Bagamoyo SEZ Development Agreement);<br>• Kukamilika kwa rasimu ya vivutio (proposed incentive package); |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | ndani (Detail design of onsite infrastructure-Roads) katika eneo la Kituo cha Teknologia Bagamoyo *(Bagamoyo Technological Park*);<br>• Kufanya usanifu wa kina na ujenzi wa miundombinu ya ndani (Detail design of onsite infrastructure-Roads) katika eneo la Mtwara SEZ; na<br>• Kutafuta mwekezaji, kufanya majadiliano na kuandaa mkataba katika eneo la Bagamoyo SEZ. | | | • Mpango Kabambe wa kuendeleza eneo la hekta 175 lililotengwa kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Teknolojia umekamilika;<br>• Miundombinu katika eneo la William Benjamin Mkapa SEZ imekarabatiwa;<br>• Kuendesha majadiliano ya awali na wawekezaji wa Bagamoyo SEZ (CMPort & SGRF);<br>• Andiko fupi (*Project Profile*) la kuonesha mpango wa uendelelezaji na makisio ya gharama ya kuendeleza miundombinu wezeshi ya eneo lililolipiwa fidia umekamilika;<br>• Makampuni 12 yamepewa leseni na kujenga viwanda katika eneo la Bagamoyo SEZ lililokwisha lipiwa fidia nje ya eneo lililotolewa kwa ajili ya Mradi wa ujenzi wa bandari mpya na ukanda wa Viwanda na jiji (hekta 30000). |
| 446. | | • Kulipa fidia katika eneo la Mradi la Kigoma SEZ; na<br>• Kufanya usanifu wa kina na ujenzi wa miundombinu ya | 4,722,983,408.00 | | • Fidia ya Shilingi 768,912,094 katika eneo la Mradi wa Kigoma SEZ imelipwa;<br>• Usanifu wa miundombinu ya |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | ndani *(Detail design of onsite infrastructure – roads)* katika eneo la Mtwara SEZ. | | | barabara na maji umekamilika;<br>• Mikataba ya Utekelezaji (*Performance Contracts*) kati ya EPZA na Wawekezaji (Third party implementing agencies –TARURA na MTUWASA) katika eneo la Mtwara SEZ imekamilika na kusainiwa;<br>• Miundombinu ya maji imekamilika kwa asilimia 100; na<br>• Ujenzi wa barabara (*access road)* katika eneo la mradi umeanza. |
| 447. | *SMES Industrial Infrastructure Expansion & Capacity Building* | • Kutunisha mtaji wa Mfuko wa Wafanyabiashara na Wananchi *(NEDF)*. | | | • Mfuko wa NEDF (ambao ni revolving fund) ulianza na mtaji wa Shilingi Milioni 500 mwaka 1994 na umekuwa ukiongezwa kwa awamu hadi kufikia shilingi bilioni 5.05 mwaka 2015 na umeendelea kuzungushwa na hivyo umekua na kufikia shilingi bilioni 7.8 mwezi Februari 2019;<br>• Mikopo yenye thamani ya shilingi 7,853,163,831 kwa wajasiriamali wadogo zaidi ya 4,541 imetolewa; na<br>• Ajira 4,438 inayojumuisha wanawake 2,130 na wanaume 2,308 |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | imezalishwa. |
| 448. | *Rural Micro Small and Medium Enterprises Support Programme (MUVI)* | • Kuanzisha vikundi vya wakulima na kuimarisha vilivyopo kwa lengo la kuboresha mnyororo wa thamani kwa mazao yaliyochaguliwa. | 100,000,000.00 | | • MUVI ilitekelezwa katika Wilaya 19 za Mikoa 7 ya Iringa, Manyara, Mwanza, Njombe, Pwani, Ruvuma na Tanga.<br>• MUVI inatoa huduma za uendeshaji wa mashamba darasa ya mbegu; miradi ya uongezaji thamani mazao; miundombinu 23 ya masoko; huduma ya uuzaji kwa pamoja kwa vikundi 618; uanzishaji wa vikundi 30 vya kuweka na kukopa (SACCOS); utaratibu wa upatikanaji wa taarifa za masoko; na mafunzo ya kilimo bora kwa wakulima 53,503 na kilimo biashara kwa wakulima 48,203; na<br>• Kuendelea na usimamizi wa mradi katika mikoa sita na wilaya 19 ambazo ni Iringa Vijijini na Kilolo – Iringa; Njombe; Simanjiro, Hanang na Babati – Manyara; Bagamoyo, Rufiji na Mkuranga - Pwani; Songea Vijijini, Namtumbo na Mbinga - Ruvuma; Sengerema, Kwimba na Ukerewe - Mwanza; na Muheza, Korogwe, Kilindi na Handeni – |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | Tanga. |
| 449. | Programu ya Maendeleo ya Kilimo Awamu ya Pili – *ASDP II.* | • Kuanzisha Maeneo ya Viwanda (*Industrial Parks*) kwa ajili ya kuongeza thamani ya mazao ya kilimo na mifugo ikiwa ni pamoja na uzalishaji wa bidhaa za ngozi *(Leather and leather products)* katika Mkoa wa Dodoma na uendelezaji wa zao la chikichi na korosho;<br>• Kuimarisha Mifumo ya Taarifa za Masoko (bei, ugavi) ya mazao ya kilimo na mifugo;<br>• Kuanisha na kubainisha teknolojia muafaka za uongezaji thamani mazao na kuzisambaza kwa wajasiriamali; na<br>• Kuendeleza mpango wa kukuza masoko na kuendeleza mnyororo wa thamani na kuwezesha wakulima kuunganishwa na masoko. | 4,6606,872,263.00 | | • Eneo la Kongano la Bidhaa za Ngozi la Zuzu Jijini Dodoma lenye ekari 107 limeanzishwa. Mkandarasi anasafisha na kusawazisha *(Clearing and Levelling)* eneo na kuandaa *detatiled design* kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu na majengo ya viwanda kwa wajasiliamali;<br>• Fidia kwa wananchi waliotoa eneo kwa ajili ya kupisha ujenzi wa Soko la Kimataifa la Mazao ya Kilimo katika Halmashauri ya mji wa Makambako imelipwa ambapo ni jumla ya Shilingi 3,026,341,090;<br>• Elimu ya umuhimu wa matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala katika ununuzi wa zao la ufuta katika mikoa ya Lindi na Mtwara imetolewa;<br>• Ufuatiliaji matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala katika zao la korosho katika mikoa ya Mtwara, Lindi, na Ruvuma umefanywa;<br>• Taarifa za bei za mazao ya kilimo kwa mikoa 26 na taarifa za bei za |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | mifugo kwa minada 53 zimekusanywa, kuchambuliwa na kusambazwa kwa wadau kwa njia ya redio, luninga, ujumbe wa simu za kiganjani, mitandao ya kompyuta na magazeti;<br>• Ufuatiliaji wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala katika zao la ufuta;<br>• Kubaini changamoto zinazokabili Kongano la Alizeti katika mikoa ya Dodoma, Manyara na Singida na kupendekeza hatua bora za kutatua changamoto hizo;<br>• Kuhamasisha na kujenga uelewa katika matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala katika ununuzi wa zao la ufuta katika mikoa ya Lindi, Manyara na Dodoma;<br>• Sensa ya Kilimo na Mifugo kwa mwaka 2018/2019 kupitia NBS inaendelea kufanywa kwa kushirikisha Wataalam kutoka Wizara za Kisekta zinazosimamia Kilimo na Mifugo pamoja na Taasisi za Umma zinazosimamia na kutekeleza Mradi wa ASDP. Kazi |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | zilizofanyika ni pamoja na: kutambua wataalam, kutoa mafunzo kwa wataalam kuhusu mbinu na taratibu za kufanya sensa, kuandaa madodoso, kuorodhesha kaya *(households listing),* kufanya majaribio ya madodoso kwenye Wilaya ya Chamwino, kufanya sensa ya majaribio *(piloting study)* kwa Mikoa 7 ambayo ni Mara, Arusha, Pwani, Ruvuma, Dodoma, Tabora na Iringa ambapo uchambuzi na uhakiki wa taarifa za kaya za kilimo zitakazoshirikishwa katika sensa unafanywa kuanzia Septemba 30, 2019 na utakamilishwa Oktoba 7, 2019;<br>• Kufanya ufuatiliaji wa matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala katika mikoa ya Mtwara, Lindi, na Ruvuma. Katika msimu wa mwaka 2016/2017, jumla ya tani 249,912 za korosho zilikusanywa kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala na mwaka 2017/2018 jumla ya tani 291,677 zilikusanywa kupitia Mfumo huo. |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | • Kushiriki katika **Operesheni korosho**, kutembelea na kuhakiki maghala na viwanda vya korosho Mkoani Lindi. Jumla ya maghala 33 yalihakikiwa. Kati ya hayo: maghala kumi (10) ni katika viwanda vya kubangua korosho na maghala mengine 23 hayana viwanda yapo kwa ajili ya uhifadhi;<br>• Ufuatiliaji wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala katika zao la ufuta ulifanyika na manunuzi kwa kutumia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala na Soko la Bidhaa *(Commodity Exchange)* kwa majaribio ambapo jumla ya kilo 88,410 zilikusanywa kupitia Chama Kikuu cha Ushirika cha RIVAKU. |
| 450. | **Mradi wa SADC TRF** | Mradi huo unalenga kusaidia nchi wanachama wa SADC kutekeleza Itifaki ya Biashara ya Jumuiya hiyo (SADC *Trade Protocol)* kwa kujikita katika utekelezaj wa maeneo yanayohusu uendelezaji wa Sera ya Viwanda na Mpango Mkakati; uendelezaji wa | | 3,524,790,035 | • Ununuzi wa vifaa vya maabara kwa ajili ya Shirika la Viwango Tanzania (TBS) umefanyika;<br>• Ununuzi wa vifaa vya maabara *(pest and diseases diagnostic equipments)* kwa ajili ya Wizara ya Kilimo umefanyika;<br>• Kitabu cha Muongozo wa Mauzo nje *(Export Guide)* kimeandaliwa; na<br>• Sekta binafsi wakiwemo wanachama |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | mnyororo wa thamani kwa zao la alizeti; uwezeshaji biashara; na utafiti katika biashara ya huduma | | | wa Taasisi ya Wazalishaji wa Mafuta ya Alizeti (TASUPA) wamewezeshwa kushiriki maonesho ya bidhaa za mafuta ya alizeti mjini Nampula, Msumbiji. |
| 451. | **Mradi wa Uwezeshaji Biashara wa TMEA** | • Kuimarisha uwezeshaji biashara nchini *(Trade facilitation);*<br>• Kufadhili utekelezaji wa Mikataba na Itifaki za Jumuiya ya Afrika Mashariki na barani Afrika. | | 4,000,000,000 | • Uchambuzi kuhusiana na majadiliano yanayoendelea ya uanzishwaji wa Eneo Huru la Biashara Afrika (AfCFTA) umefanyika;<br>• Warsha za kuelimisha umma kuhusu AfCFTA zilifanyika;<br>• Kamati ya Kitaifa ya Uwezeshaji Biashara (NCTF) iligharamiwa;<br>• Rasimu ya mapitio ya Sera ya Taifa ya Biashara imeandaliwa;<br>• Mikutano ya Kamati ya Kitaifa ya Uondoaji wa Vikwazo vya Kibiashara Visivyokuwa vya Kiushuru (NMC) imefanyika; na<br>• Kuzijengea nchi wanachama uwezo wa kibiashara *(trade capacity)* hususan kwa kubaini changamoto za uzalishaji na uuzaji wa bidhaa pamoja na huduma ili kuziwezesha kunufaika na fursa zilizopo kati ya Nchi na Nchi, Kikanda na Kimataifa. |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| 452. | **Mradi wa *EU-EAC Market Access Upgrade Programme*** *(MARKUP)* | • Kutatua changamoto za uzalishaji *(supply side constraints)* na za upatikanaji wa masoko *(market access)* kwa baadhi ya bidhaa zinazouzwa nje kama vile Kahawa, Chai na Kakao *(agro-industrial crops)* na bidhaa za mboga mboga na matunda pamoja na viungo vya chai, na<br>• Kuimarisha uwezo wa nchi za EAC kukua kupitia biashara kwa kuzingatia rasilimali walizo nazo | | 4,229,479,018 | • Warsha kuhusiana na Vikwazo vya Kibiashara Visivyokuwa vya Kiushuru na namna ya kupunguza au kutatua changamoto zimefanyika |
| 453. | Kituo cha Zana za Kilimo na Ufundi Vijijini – CAMARTEC. | • Kufanya tafiti ya mahitaji ya zana za kilimo na teknolojia za kilimo vijijini ili kuboresha utendaji kazi na maisha vijijini;<br>• Kubuni na kutengeneza teknolojia; na<br>• Kuendelea na majaribio na ukaguzi wa zana za kilimo na teknolojia za vijijini ili kuhakiki ubora wa zana | 640,060,625.00 | | • *Prototype* tatu 3 za teknolojia ya kubangua Korosho zimebuniwa na mashine 40 zimeanza kuzalishwa kibiashara *(commercialization)*. Aidha, *Prototype* moja ya teknolojia ya kusindika chikichi imekwisha buniwa;<br>• Kituo kimefanya uchambuzi wa mahitaji *(need assessment)* ya teknolojia katika mikoa mbalimbali na kubuni zana 50 za kupandia mazao ya kilimo ikiwa ni pamoja na zao la Alizeti; |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | hizo kwa manufaa ya wadau. | | | • Teknolojia ya kufunga majani kwa ajili ya malisho ya mifugo imebuniwa, inatengenezwa na kuuzwa kwa watumiaji;<br>• Teknolojia ya Majiko yanayotumia nishati kidogo *(community stoves)* katika Taasisi kama mashule na magereza imekamilika na tayari inatumika katika shule tano na gereza moja la Kwitanga – Kigoma;<br>• Majaribio ya baadhi ya zana za kilimo kama vile matrekta ya CFT yanayotengenezwa na CARMATEC yamekamilika na tayari matrekta 4 yameuzwa kwa watumiaji; na<br>• Kuhamasisha wananchi kuhusu teknolojia ya kuchakata mihogo na kuondoa sumu ya *cynide*. |
| 454. | Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda-TIRDO | • Kufanya tafiti mbalimbali za maendeleo ya viwanda nchini; na<br>• Kuboresha maabara ili kukidhi vigezo vya kupata ithibati. | 1,745,000,000 | | • TIRDO inaendelea na kazi za utafiti wa teknolojia za ubanguaji Korosho na usindikaji wa Michikichi ambapo kwa sasa wapo katika hatua ya udukuzi *(Reverse Engineering)* wa mitambo;<br>• Ujenzi wa Maabara ya Mafuta, Gesi, *Biotechnology* na Makaa ya Mawe |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | umekamilika; na<br>• Ununuzi wa vifaa mbalimbali vya maabara kwa ajili ya tafiti za mafuta, sumukuvu *(Biotechnology)* gesi na makaa ya mawe umefanyika. |
| 455. | Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo-TEMDO | • Kufanya tafiti mbalimbali za kihandisi na usanifu wa mitambo;<br>• Kuendelea na uboreshaji wa karakana na ofisi ya usanifu pamoja na miundombinu ya Taasisi;<br>• Kubuni na kuendeleza chasili cha mtambo wa kukausha mazao ya kilimo ili kuongeza thamani; na<br>• Kuendeleza chasili cha mtambo mdogo wa kutengeneza brikwiti kutokana na vumbi la makaa ya mawe kwa ajili ya kuongeza vyanzo vya nishati katika kukausha mazao na matumizi ya nyumbani. | 1,855,385,000 | | • Shirika lipo katika hatua ya udukuzi Chasili *(prototype)* cha Mtambo wa kukausha mazao kama chai;<br>• Shirika limebuni michoro ya Chasili cha kutengeneza '*briquette*' kutokana na vumbi la Makaa ya Mawe ikilenga zaidi kupata teknolojia nzuri ya nishati na yenye gharama nafuu katika kukausha korosho wakati wa ubanguaji; na<br>• Uboreshaji wa maabara za utafiti kwa kununua mitambo na vifaa vya kisasa umefanyika. |
| 456. | Chuo cha Elimu ya | • Kuboresha mazingira ya | 1,928,000,000 | | • Ukarabati wa jengo la utawala, jengo |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | Biashara-CBE | kujifunza na kufundishia katika Chuo cha CBE Kampasi ya Mwanza na DSM. | | | lenye madarasa 8, hosteli yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 89 na maabara 1 ya kompyuta unaendelea;<br>• Ununuzi wa eneo na majengo ya iliyokuwa Shule ya Sekondari ya New Helen – Nyasaka Mwanza, yenye ukubwa wa ekari kumi (10) na majengo ya kisasa kwa ajili ya chuo cha CBE Kampasi ya Mwanza pamoja na ukarabati wa majengo hayo umekwishakamilika; na<br>• Ujenzi wa ghorofa nne (4) katika jengo la 'Cafeteria' Kampasi ya Dar es Salaam unaendelea; |
| 457. | Wakala wa Vipimo-WMA | • Kuboresha uwezo wa WMA kwa kununua vifaa vya kisasa vya kuhakiki mizani ya kupimia madini na vito vya madini; na<br>• Ununuzi wa mashine *(Laser Scanner)* ya uhakiki wa matenki ya kupokelea mafuta katika Bandari za Dar es Salaam na Mtwara. | 1,000,000,000 | | • Ununuzi wa vifaa vya kupimia usahihi wa mizani ya kupimia madini na vito vya thamani ili kuzuia udanganyifu katika viwango vya madini yanasosafirishwa nje ya nchi umefanyika. |
| 458. | Mradi wa Kusaidia Kukondowesha | • Kuwajengea uwezo wajasiriamali wa bidhaa ili | | 196,140,000 | • Mafunzo kwa wajasiriamali wafugaji wa nyuki juu ya namna bora ya |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | Biashara *(Support for Trade Mainstreaming)* | kupata fursa za masoko ndani na nje ya nchi. | | | ufugaji na usindikaji wa asali mkoani Tabora yamefanyika;<br>• Maafisa Biashara 74 walijengewa uwezo katika masuala ya ukondoweshaji wa biashara; na<br>• Maafisa wa Wizara na Taasisi zinazoshughulika na Biashara wamejengewa uwezo katika masuala ya uandaji wa miradi inayoweza kusaidia kuibua fursa za biashara kwa wananchi. |
| 459. | Shirika la Uendelezaji wa Viwanda Vidogo – SIDO | • Kuimarisha Vituo vya Maendeleo ya Teknolojia *(Technology Development Centers*-TDCs) vya SIDO; na<br>• Kujenga miundombinu ya viwanda (barabara, mifumo ya maji, umeme, mitaro, ya maji taka na uzio) katika mikoa. | 7,000,000,000.00 | | • Kituo cha Teknolojia cha Lindi kimeboreshwa kwa kununua mitambo mipya;<br>• Vituo vya teknolojia vya Shinyanga na Kigoma vimeimarishwa ili viwe katika nafasi nzuri ya kutengeneza teknolojia za kuchakata zao la Chikichi pamoja na mazao mengine;<br>• SIDO imetambua, kuanzisha na kusambaza teknolojia mpya 40 za ubanguaji korosho usindikaji na ufungashaji wa vyakula, utengenezaji wa vifaa vya ujenzi hasa matofali, utengenezaji wa chokaa na chaki, ukamuaji wa mafuta ya kula kutokana |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | na michikichi na usindikaji wa ngozi kwa kutumia njia za asili; na<br>• Majengo 12 ya kufanyia shughuli za viwanda kwa wajasiriamali wadogo *(industrial sheds)* katika mikoa ya Dodoma, Geita, Kagera, Manyara, Mtwara na Njombe, Ruvuma na Kigoma yamekamilika na baadhi yameanza kutumika;<br>• Ofisi 4 za SIDO za kutolea huduma katika Mikoa mipya ya Geita, Simiyu na Katavi pamoja na Wilaya ya Chato zimekamilika;<br>• Maeneo ya ujenzi yamekwishafanyiwa upembuzi yakinifu, michoro ya usanifu *(architectural drawings)* imeshaandaliwa na gharama zake kubainishwa, katika mitaa ya viwanda mikoa ya Mara, Shinyanga na Singida; na<br>• Miundombinu ya umeme na maji imeshajengwa katika mikoa ya Simiyu, Geita na Kagera. |
| 460. | Eneo la Kongane ya Viwanda – TAMCO. | • Kuendeleza Eneo la Viwanda TAMCO ili kuruhusu ujenzi wa | 3,000,000,000 | | • Ujenzi wa barabara za ndani zenye urefu wa mita 580 umekamilika na sasa wanakamilisha ujenzi wa mitaro |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | viwanda mbalimbali;<br>• Ujenzi wa bwawa la maji safi na maji taka; na<br>• Kujenga barabara za ndani ya Mradi. | | | ya pembeni ya barabara hivyo, kufanya kazi ikamilike kwa asilimia 94; na<br>• Mkandarasi kwa ajili ya kujenga Kituo cha Kupozea Umeme (Power Sub-station) amepatikana. Makubaliano ya malipo kati ya Mkandarasi na *Textile Development Unit* yamekamilika. |
| 461. | Mradi wa Matrekta ya URSUS TAMCO – Kibaha. | • Ujenzi wa Kiwanda cha Kuunganisha Matrekta 2,400 katika eneo la TAMCO Kibaha kupitia Kampuni ya URSUS S.A ya Poland;<br>• Kuimarisha Kiwanda cha *Kilimanjaro Machine Tool* (KMTC) ili kuwezesha utengenezaji wa tela kwa ajili ya matrekta ya URSUS; na<br>• Kusimamia na kulipia gharama za uingizaji matrekta bandarini pamoja na zana zake na kuyapeleka eneo la Mradi. | 4,500,000,000 | | • Ujenzi wa kiwanda kipya cha kuunganisha matrekta katika eneo la viwanda la TAMCO kibaha, umekamilika kwa asilimia 60;<br>• Jumla ya Wataalam 27 wa kitanzania wamepata mafunzo katika fani ya ufundi na usimamizi wa namna ya kuunganisha Matrekta ya URSUS nchini Poland;<br>• Jumla ya matela ya matrekta 15 yaliyosanifiwa na CAMARTEC na TEMDO yameshatengenezwa na 10 yako katika hatua za awali za matengenezo katika Kiwanda cha *Kilimanjaro Machine Tools* (KMTC). Uzinduzi rasmi wa matrela hayo umefanyika mwanzoni mwa mwezi |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | Julai, 2019;<br>• Mpaka sasa jumla ya Matrekta 825 yaliyo katika mfumo wa *Semi Knocked Down* – SKD yamewasili kutoka Poland na kuunganishwa; na<br>• Kuendelea na mikakati ya kuuza matrekta ya URSUS ikiwemo; Kusaini makubaliano na benki ya kilimo ili kutoa mikopo kwa wakulima; na Mkakati maalum wa kuwakopesha wakulima, ambao umepata muitikio mkubwa kutoka kwa wakulima ambapo jumla ya matrekta 586 yameuzwa. |
| 462. | TBS<br>Ujenzi wa Jengo la Maabara ya Kisasa – Dar es Salaam (TBS Test House) | • Ujenzi wa Maabara yenye nafasi na huduma za kutosheleza;<br>• Kusaidia viwanda katika Nyanja zote za upimaji wa bidhaa na ugezi wa vifaa;<br>• Kuwezesha biashara ndani ya nchi;<br>• Kusaidia katika utafiti wa kuendeleza bidhaa mbalimbali nchini; na | 19,325,304,165.47 | | • Shirika limefanikiwa kukamilisha ujenzi wa jengo jipya la maabara ya kisasa lenye ghorofa nane (8) ambalo litarahisisha utendaji wa shughuli za maabara na kutatua tatizo la ufinyu wa nafasi kwa ajili ya vifaa pamoja na sampuli uliokuwepo awali pamoja na kutatua changamoto ya ucheleweshwaji wa majibu ya sampuli. |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | • Kulinda afya ya umma na mazingira. | | | |
| **JUMLA NDOGO** | | | **96,578,755,461.47** | **11,950,409,053.00** | |
| **WIZARA YA NISHATI** | | | | | |
| 463. | Mradi wa Kufua Umeme wa Maji Julius Nyerere - MW 2,115 | Lengo la kuu la mradi huu ni kuhakikisha kunakuwa na upatikanaji wa umeme wa uhakika nchini, wenye kutosheleza na kwa bei nafuu. | 1,248,221,921,361.14 | - | • Ujenzi wa barabara za muda za kuingia sehemu mbali mbali za maeneo ya mradi zimekamilika kwa asilimia mia moja (100%).<br>• Utafiti wa miamba na udongo umekamilika kwa asilimia mia moja (100%).<br>• Ujenzi wa daraja la muda umekamilika kwa asilimia mia moja (100%).<br>• Kazi ya matayarisho ya uchimbaji wa njia ya kuingilia kwenye mtaro wa kuchepushia maji (Adit tunnel)- imekamilika kwa asilimia themanini na nne (84%).<br>• Kukamilika kwa upembuzi yakinifu wa awali wa ujenzi wa njia za kusafirisha umeme ya kV 400 (Rufiji hadi Chalinze) na taratibu za ununuzi za kumpata Mtaalam Mwelekezi kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | unaendelea.<br>• Ujenzi wa bwawa (main dam) na ujenzi wa njia ya kupitisha maji (diversion tunnel) umekamilika kwa asilimia 24.74. |
| 464. | Mradi wa ujenzi wa Njia ya Msongo wa kV 220 kutoka Makambako hadi Songea. | • Kuunganisha mkoa wa Ruvuma na baadhi ya maeneo katika Mkoa wa Njombe katika Gridi ya Taifa.<br>• Kuondoa mitambo ya kuzalisha umeme kwa kutumia mafuta mazito na kuokoa gharama kubwa zilizokuwa zinatumiwa na Serikali kuzalisha umeme kwa kutumia mitambo hiyo mkoani Ruvuma.<br>• Kuongeza uwezo wa umeme unaosafirishwa na kusambazwa katika ya mikoa ya Njombe na Ruvuma. | 57,734,498,967.70 | 102,450,682,527.10 | • Kukamilika kwa asilimia 100 kwa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kV 220, yenye urefu wa kilomita 250 kutoka Makambako hadi Songea kupitia Madaba pamoja na ujenzi wa vituo vya kupoza umeme vya Madaba na Songea na upanuzi wa kituo cha Makambako;<br>• Kukamilika kwa kazi ya kufunga reactor na distribution panel katika kituo cha Madaba; na<br>• Kuendelea kwa kazi ya kuunganisha wateja wapya. |
| 465. | Mradi wa TEDAP wa kuboresha njia za | • Kuboresha miundombinu ya umeme katika mikoa ya | 253,000,000.00 | 45,251,000,000.00 | • Kukamilika kwa baadhi ya njia za kusafirisha na kusambaza umeme |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | usafirishaji, usambazaji na vituo vya kupozea umeme mikoa ya Dar es Salaam, Arusha na Kilimanjaro. | Dar es Salaam, Arusha na Kilimanjaro.<br>• Ujenzi wa miradi midogo *(home system)* ya kusambaza umeme nje ya Gridi ya Taifa pamoja na kujenga uwezo wa wataalamu katika sekta ya nishati. | | | pamoja na vituo vya kupozea umeme. Vituo vya kupozea umeme vilivyokamilika ni KIA na Kiyungi pamoja na njia za kusafirisha umeme kutoka Mbagala-FZII, FZII-FZIII, Ubungo-Kurasini na Kilimanjaro – Arusha;<br>• Kukamilika kwa ujenzi wa njia ya kusafirishia umeme kutoka Kurasini-Kigamboni pamoja na kituo cha kupozea umeme cha Kurasini;<br>• Umekamilika Septemba 2018 |
| 466. | Mradi wa Kupeleka Umeme Vijijini (REA) | | | | |
| 467. | a. Kupeleka Umeme Vijijini kupitia REA Awamu ya Pili (REA II) | Kuwezesha usambazaji wa umeme vijijini na Makao Makuu ya Wilaya 13 yaliyokua hayana umeme ili kuongeza ushiriki wa wananchi katika kuinua uchumi. | 860,398,106,943.00 | 109,115,300,277.00 | • Kupeleka umeme katika makao makuu ya wilaya ya Mlele ikiwa ni ukamilishaji wa kupeleka umeme katika makao makuu ya wilaya 13;<br>• Ujenzi wa miundombinu ya msongo wa kati km 1,951 zilizobaki kati ya 17,735 za wigo wa mradi,<br>• Ujenzi wa miundombinu ya msongo mdogo km 2,851.2 zilizobaki kati ya 10,966.2 za wigo wa mradi;<br>• Ufungaji wa transfoma 1,764 kati ya |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | 4,104; na<br>• Kuunga wateja 150,543; |
| 468. | b. Mradi wa Ujazilizi (Densification) unaolenga kupeleka Umeme kwenye vitongoji na maeneo ambayo hayajafikiwa na umeme ndani ya vijiji vyenye umeme. | Kuongeza wigo wa usambazaji umeme katika maeneo ambayo miundombinu ya umeme imefika ili kuongeza ushiriki wa wananchi katika kuinua uchumi na kuboresha huduma za kijamii. | - | 63,295,020,126.54 | • Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu na kuwezesha kupatiwa umeme vijiji 295 na vitongoji 99 na kuunga jumla ya wateja 34,102 kati ya 34,600 wameunganishiwa umeme. Uunganishwaji wa wateja unaendelea chini ya usimamizi wa TANESCO.<br>• Mradi wa Ujazilizi 1 (REDP 1) umekamilika na TANESCO wanaendelea kuunga wateja. |
| 469. | c. Usambazaji umeme kwenye vijiji vilivyo pembezoni mwa mkuza wa Njia Kuu ya Umeme wa Msongo wa kV 400 (BTIP VEI) kutoka Iringa hadi Shinyanga | Lengo ni kupeleka umeme katika vijiji vilivyosambamba na mkuza ikiwa ni mkakati wa kupunguza au kudhibiti athari za kijamii na mazingira na kuongeza ushiriki wa wananchi katika kuinua uchumi na kuboresha huduma za kijamii. | - | 44,800,000,000 | • Hadi kufikia tarehe 31 Disemba 2019, vijiji vyote 115 na vitongoji vyote 6 vimeunganishiwa umeme na wateja 14,511 kati ya 30,350 wameunganishiwa umeme. Kwa sasa Wakandarasi wanaendelea na kazi ya kuunganisha wateja na ukamilishaji wa ujenzi wa kituo cha kupoozea umeme cha Mtera 220/33kV, 2 x 10MVA *sub-station* .<br>• Mradi wa kusambaza umeme umekamilika na TANESCO wanaendelea kuunga wateja. |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| 470. | d. Usambazaji Umeme Vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Kwanza (REA III Round I). | Mradi unalenga kufikisha umeme kwenye vijiji 3,559 ambavyo havijafikiwa na miundombinu ya umeme wa gridi. | 547,172,229,462.05 | - | • Hatua iliyofikiwa ni kuunganishiwa umeme kwa vijiji 7,094 na hivyo kufanya vijiji vilivyopatiwa umeme nchini kote kufikia 9,112. |
| 471. | e. Kupeleka Umeme nje ya Grid ya Taifa (Off-Grid) | Lengo ni kushirikisha sekta binafsi kufikisha umeme katika maeneo ya visiwa na yaliyo pembezoni ambayo hayawezi kufikiw na Gridi ya Taifa. Vyanzo vya nishati jadidifu ndivyo vinapewa kipaumbele kupItia mradi huu. | - | 19,234,442,300.00 | • Vijiji 102 kati ya 119 vilivyopo kwenye Mpango vimepatiwa umeme ambayo ni sawa na **asilimia 86**<br>• Waendelezaji 7 kati ya 13 waliopata ufadhili wamekamilisha miradi |
| 472. | Mradi wa kuunganisha Mikoa yote katika Gridi ya Taifa pamoja na Kuzima Mitambo ya Mafuta | Kuondoa gharama kubwa zilizokuwa zinatumiwa na Serikali kuzalisha umeme kwa kutumia mitambo ya mafuta pamoja na kununua umeme kutoka mitambo ya IPTL, Symbion na Aggreko. | 67,734,498,967.70 | 102,450,682,527.10 | • Kuokoa Shilingi bilioni 22.28 kwa mwaka kwa kuzima mitambo ya mafuta ya Songea, Madaba, Mbinga, Namtumbo, Biharamulo, Ngara, Ludewa, Kilwa na Masasi;<br>• Kuokoa shilingi bilioni 635 kwa mwaka kwa kuzima mitambo ya IPTL na Aggreko;<br>• Kuokoa Shilingi bilioni 84 kwa mwaka kuacha kutumia mitambo ya |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | Symbion;<br>• Kuunganishwa kwa mkoa wa Ruvuma na baadhi ya maeneo katika Mkoa wa Njombe katika Gridi ya Taifa<br>• Kuunganishwa kwa mikoa ya Mtwara na Lindi katika Gridi ya Taifa; na<br>• Kuunganishwa kwa Wilaya za Biharamulo na Ngara sawia katika Gridi ya Taifa. |
| 473. | Njia ya Kusafirisha Umeme ya Msongo wa kV 400, Iringa - Shinyanga - BTIP Phase II | Kuongeza uwezo (upgrade) wa kusafirisha umeme pamoja na vituo vya kupoza umeme kutoka kV 220 hadi kV 400 katika miji ya Iringa, Dodoma, Singida na Shinyanga. | - | USD: 17,973,837.00<br>TZS: 1,226,494,882.00 | • Mkandarasi wa kutekeleza kazi katika vituo vya kupoza umeme vya Dodoma na Singida anaendelea na ujenzi;<br>• Kuanza ufungaji wa *Reactors* na *Transformers* kwa vituo vya Dodoma na Singida;<br>• Kukamilika kwa awamu ya Kwanza (Phase I) ya ujenzi wa njia kuu ya kusafirisha umeme kV 400 kutoka Iringa hadi Shinyanga (Backbone) kupitia Dodoma na Singida yenye urefu wa kilometa 670 mwezi Desemba, 2016 kwa gharama ya Shilingi bilioni 512; na |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | • Awamu ya pili ya utekelezaji wa mradi inaendelea |
| 474. | Mradi wa kuzalisha umeme wa Kinyerezi II MW 240 kwa kutumia teknolojia ya *Combined Cycles*. | Kuongeza uwezo wa kufua umeme kutokana na gesi asilia na kuongeza uwezo wa uzalishaji na kuimarisha umeme katika Gridi ya Taifa . | - | 39,082,372,000.00 | • Ujenzi wa mitambo yote sita (6) ya kufua umeme kwa kutumia gesi asilia umekamilika na mitambo hiyo inazalisha jumla ya MW 168.<br>• Mitambo ya kufua umeme kwa kutumia *exhaust gas (waste heat)* kutoka mitambo ya gesi katika kuzalisha mvuke yote miwili imekamilika na sasa imezalisha MW 80 na kufikisha jumla ya MW 248 na kuingizwa katika Gridi ya Taifa<br>• Mkandarasi amekamilisha majaribio ya mitambo mwezi Desemba, 2018.<br>• Kukamilika kwa mradi huu kumeongeza uwezo wa kuzalisha umeme katika Gridi ya Taifa *(total installed capacity)* kufikia MW 1,613.52. |
| 475. | Mradi wa kufua umeme wa Kinyerezi I *Extension* MW185 | Kupanua mradi wa Kinyerezi I MW 150 uliokamilika kwa kuongeza mitambo mingine ya MW 185 na hivyo kufanya uwezo wa kituo hicho kuwa na | 265,449,872,089.00 | 84,000,000,000.00 | • Kuanza kufungwa kwa mitambo yote minne (4);<br>• Kuendelea na upanuzi (upgrade) wa njia ya msongo wa KV 132 kutoka Kinyerezi I hadi kituo cha kupoza umeme cha Gongo la Mboto |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | jumla ya MW 335. | | | ambapo utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 85. |
| 476. | Mradi wa kuunganisha Gridi ya Taifa Mikoa ya Lindi na Mtwara hadi Ruangwa | • Kuunganisha Mikoa ya Lindi na Mtwara katika Gridi ya Taifa.<br>• Kuongeza na kuboresha hali ya upatikanaji umeme katika mikoa ya Lindi na Mtwara. | 14,700,000,000.00 | - | • Kukamilika kwa mradi kwa asilimia 100. |
| 477. | Mradi wa ujenzi wa kituo cha kupozea umeme cha Dege Kigamboni | • Kuboresha hali ya upatikanaji wa umeme katika manispaa ya Kigamboni. Mradi huu unahusiha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kV132 na kituo cha kupozea umeme 132/33 kV. | 1,079,909,124.00 | - | • Kukamilika kwa malipo ya awali kwa mkandarasi wa kituo cha kupozea umeme;<br>• Kukamilika kwa tathmini ya fidia;<br>• Kukamilika kwa sehemu ya kuweka transfoma; na<br>• Kufikia asilimia 94 kwa kazi ya ujenzi wa jengo la kudhibiti mfumo wa umeme. |
| 478. | Tanzania – Zambia (TAZA) Interconnector Project. Njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kV 400, North West Grid (Iringa - Mbeya – | • Mradi huu utawezesha kuunganisha umeme maeneo ya Magharibi na Kaskazini-Magharibi mwa Tanzania katika Gridi ya Taifa na kuondoa matumizi ya mitambo ya mafuta (diesel) katika | 14,994,619,458.00 | - | • Benki ya Dunia tayari imekwishatenga Dola za Kimarekani Milioni 455 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu. Taratibu za makubaliano zinaendelea na wafadhili watakaofadhili kwa pamoja na Benki ya Dunia. Shirika la Maendeleo la Ufaransa (Agence |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | Tunduma - Sumbawanga ) | maeneo hayo na kuwafikishia umeme wananchi wengi.<br>• Pia, kukamilika kwa mradi huu kutawezesha unganishaji wa gridi ya mataifa ya Kusini mwa Afrika (SAPP) kupitia Zambia na gridi ya mataifa Mashariki mwa Afrika (EAPP) kwa kupitia Kenya. | | | Francaise de Developpment (AFD)) litatoa kiasi cha Dola za Kimarekani Milioni 100 na Umoja wa Ulaya (EU) itachangia EURO Milioni 30 (Grant).<br>• Upitiaji upya taarifa zilizoandaliwa awali (update) kuhusu mazingira na shughuli za ujenzi wa mradi huu bado zinaendelea kufanyika chini ya Mshauri Mwelekezi (Consultant) ambaye ni Kampuni ya SWECO International AB kutoka Sweden ikiwa ni pamoja na uandaaji wa zabuni kwa ajili ya kuwapata wakandarasi. Mchakato kuwatafuta wakandarasi unatarajiwa kuanza mwezi Desemba 2019. |
| 479. | Mradi wa Kufua umeme wa Rusumo MW 80 | Ujenzi wa kituo cha kufua umeme wa MW 80 kwa kutumia nguvu ya maporomoko ya maji ya mto wa Kagera kwa ushirikiano wa nchi tatu (3) za Tanzania, Rwanda na Burundi. | - | 9,453,000,000.00 | • Kuendelea na kazi ya kufunga mitambo ambapo utekelezaji umefikia asilimia 52;<br>• Kukamilika kwa milango ya kuingiza na kuchepusha maji (spillway and intake gates); na<br>• Kukamilika kwa asilimia 56 ya kazi ya uchimbaji wa handaki la kupitishia maji. |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | • Utekelezaji umefikia asilimia 60. |
| 480. | Njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 400 kutoka kituo cha kuzalisha umeme cha Julius Nyerere katika maporomoko ya mto Rufiji hadi Kinyerezi na Dodoma kupitia Chalinze. | Kusafirisha umeme (MW 2,115) utakao zalishwa katika bwawa la Mwalimu Nyerere na kuunganishwa katika Gridi ya taifa. | 1,000,000,000.00 | - | • Kukamilika kwa upimaji na tathmini ya mali za wananchi watakaopisha mradi kwa sehemu ya Kinyerezi hadi Chalinze;<br>• Tathimini ya Athari ya Mazingira na Jamii katika njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 400 kutoka Rufiji hadi Chalinze inaendelea;<br>• Upembuzi yakinifu (Feasiblity study) kwa ajili ya ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka bwawa la Mwalimu Nyerere hadi Kinyerezi kupitia Chalinze unaendelea;<br>• Upembuzi yakinifu (Feasiblity study) kwa ajili ya ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Chalinze hadi Dodoma umekamilika; na<br>• Mchakato kwa ajili ya kupata Wakandarasi kwa ajili ya ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Chalinze hadi Dodoma unaendelea. |
| 481. | Njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa Kv 400, kutoka | Ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa kV 400 yenye urefu wa kilomita 414 | TZS: 44,882,886,873.85 | USD: 70,926,854.55<br>EUR: 2,613,962.59<br>TZS: 26,213,357,150.33 | • Kukamilika kwa asilimia 70 ya utekelezaji wa mradi huu ambapo |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | Singida –Arusha - Namanga | kutoka Singida hadi Namanga kupitia Arusha ambapo mradi umegawanyika katika makundi matano (5) ya utekelezaji ambayo ni: Singida-Babati (km 150); Babati-Arusha-Namanga (km 114); ujenzi na upanuzi wa vituo vya kupoza umeme (substations) na usambazaji wa umeme katika vijiji 14 vitakavyopitiwa na mradi. | | | nguzo (Tower) 621 kati ya 1,072 zimefungwa; na<br>• Utekelezaji wa mradi huu unaenda sambamba na utekelezaji wa mradi wa Backbone awamu ya pili (Backbone Phase II) unaolenga kuongeza uwezo (Upgrade) wa vituo vya kupoza umeme kutoka kV 220 mpaka kV 400 katika Mikoa ya Iringa, Shinyanga, Singida na Dodoma ambapo utekelezaji umefikia asilimia 83. |
| 482. | Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kV 400 kutoka Somanga Fungu – Kinyerezi | Mradi huu unahusisha, Ujenzi wa njia kuu ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 400, kilometa 198 kutoka Somanga hadi Kinyerezi.<br><br>Gharama za Mradi zinakadiriwa kuwa Dola za Kimarekani 59.4 Milioni.<br><br>Mradi unatarajiwa kuanza Januari 2010 na kukamilika | 273,000,000.00 | - | • Mhandisi Mshauri amewasilisha Taarifa ya awali ya durusu ya Upembuzi yakinifu "Draft Feasibility Study Report" pamoja na makabrasha ya zabuni "Draft Bid document" kwa ajili ya kudurusiwa na TANESCO;<br>• Fidia kwa waathirika wa mradi inaendelea; na<br>• TANESCO imeshalipa kiasi cha shilingi bilioni 57.45 kati ya shilingi bilioni 69.14 sawa na asilimia 83.10 kwa waathirika 3,169 kati ya 3,901. |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | mwaka 2021 Disemba. | | | |
| 483. | Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kV 400 kutoka Chalinze – Dodoma. | Mradi huu unahusisha, Ujenzi wa njia kuu ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 400, kilometa 342 kutoka Chalinze hadi Dodoma. Gharama za Mradi zinakadiriwa kuwa Dola za Kimarekani 146.5 Milioni. Mradi unatarajiwa kuanza Julai 2020 na kukamilika mwaka 2021 Disemba. | 2,200,000,000.00 | - | • Kukamilika kwa Upembuzi Yakinifu, uandaaji wa makabrasha ya zabuni na tathmini ya mali za wananchi watakaopisha mradi. |
| 484. | Mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Uganda hadi Tanzania. | Kujenga bomba la usafirishaji wa Mafuta Ghafi kutoka Hoima, nchini Uganda hadi Bandari Tanga nchini Tanzania. | 1,205,654,061 | - | • Kukamilika kwa kazi ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira; na<br>• Kuendelea na utoaji wa elimu kwa umma kwa maeneo ya pembezoni mwa eneo la mradi. |
| 485. | Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia – Lindi (LNG). | Kuendeleza Gesi Asilia inayozalishwa katika kina kirefu baharini kwa kuichakata gesi hiyo kuwa kimiminika. | 819,946,900 | - | • Kuendelea kwa tafiti za namna ya kuzalisha na kusafirisha gesi kutoka bahari kuu hadi eneo la mradi;<br>• Kuendelea na majadiliano ya Mikataba Hodhi (Host Government Agreement - HGA) baina ya Serikali na Kampuni za utafutaji na uendelezaji zitakazotekeleza mradi; na |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | • Ulipaji wa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi |
| 486. | Mradi wa Hifadhi ya Kimkakati ya Mafuta ya Akiba ya Dharura (*Strategic Petroleum Reserve - SPR*) | Uanzishaji wa hifadhi ya kimkakati ya mafuta ya akiba ya dharura | 351,750,912 | - | • Kukamilika kwa Sheria, Kanuni (regulations) na taratibu za usimamizi wa mradi (SPR manual);<br>• Kupatikana kwa maeneo ya ujenzi wa miundombinu ya kupokelea na kuhifadhi mafuta ya akiba ya Taifa katika mikoa ya Tanga na Dodoma. Taratibu za utwaaji wa maeneo hayo zinaendelea;<br>• Kufanyika kwa utafiti wa namna bora ya kuagiza mafuta ya hifadhi na biashara kwa kulinganisha *(benchmarking)* nchi za Nigeria, Ghana, Saudi Arabia, Kuwait, UAE na Oman; na<br>• Kukamilika kwa hadidu za rejea za kumpata Mshauri Mwelekezi wa kufanya Usanifu wa Kihandisi *(Engineering Design)* wa ujenzi wa miundombinu ya uhifadhi wa mafuta pamoja na kufanya Tathmini ya Athari za Mazingira na Jamii (ESIA) kwa eneo la Dodoma na Tanga. |
| 487. | Utafutaji na | Kutafuta mafuta na gesi | 188,409,153 | - | • Kukamilika kwa Tathmini ya Athari |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | ukusanyaji wa taarifa za mitetemo aina ya 3D katika vitalu vya 4/1B & 4/1C | asilia. | | | za Mazingira (EIA) kwa kazi ya kukusanya data za mitetemo aina ya 3D;<br>• Kukamilika kwa tafiti za geochemical na petro-physical kwa visima vya Kitalu Na. 1 vilivyo karibu na Vitalu Na. 4/1B na 4/1C; na<br>• Kuendelea na taratibu za manunuzi za kumpata Mkandarasi wa kukusanya na kuchakata takwimu za mitetemo za 3D kiasi cha kilomita za mraba 600. |
| 488. | Ujenzi wa miundombinu ya kusambaza gesi asilia katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Mtwara na Lindi | Ujenzi wa miundombinu ya usambazaji wa gesi asilia katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Mtwara na Lindi kwa awamu. | 16,405,548,739 | - | Dar es Salaam<br>• Ujenzi wa miundombinu ya kusambaza gesi yenye urefu wa Kilomita 18 unaohusisha kuunganisha wateja wa gesi kupikia majumbani maeneo ya Mikocheni, Mlalakuwa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam umefikia asilimia 95. Mradi huu utaziunganisha jumla ya nyumba 195 za awali pamoja na Cafeteria za Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; na<br>• Kuunganisha miundombinu ya bomba kuu la kusafirisha gesi kutoka Mtwara na Songo Songo katika |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | bomba la usambazaji gesi la Ubungo-Mikocheni pamoja na kuunganisha kiwanda cha Coca Cola umekamilika kwa asilimia 100. Kiwanda cha Coca Cola kwa sasa kinatumia gesi asilia wastani wa futi za ujazo milioni 0.1 kwa siku.<br><br><u>Pwani</u><br>• Kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu ya kusambaza gesi yenye urefu wa Kilomita 5.5;<br>• Kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu ya kupeleka gesi asilia kiwanda cha Goodwill Ceramics. Kiwanda hiki kwa sasa kinatumia gesi asilia wastani wa futi za ujazo milioni 4.5 kwa siku;<br>• Kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu ya kupeleka gesi asilia kiwanda cha Lodhia. Kiwanda hiki kwa sasa kinatumia gesi asilia wastani wa futi za ujazo milioni 0.2 kwa siku; na<br>• Kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu ya kupeleka gesi asilia |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | kiwanda cha Knauf. Kiwanda hiki kipo kwenye hatua za mwisho kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya kupokelea gesi kiwandani ili kukiwezesha kutumia gesi asilia.<br><br><u>Mtwara na Lindi</u><br>• Kukamilika kwa Ujenzi wa miundombinu ya kusambaza gesi yenye urefu wa Kilomita 17 kwa Mkoa wa Mtwara;<br>• Ununuzi wa mabomba na viunganishi vya mabomba ya gesi asilia kwa ajili ya kuunganisha nyumba 125 na taasisi 5 za awali umekamilika;<br>• Kuanza kwa Mchakato wa Ununuzi wa mita za kusomea matumizi ya gesi unaendela;<br>• Kukamilika kwa asilimia 95 za Ujenzi wa kuunganisha nyumba 125 na taasisi 5 za awali; na<br>• Kukamilika kwa Upembuzi wa awali wa mradi wa usambazaji gesi asilia Mkoa wa Lindi. |
| 489. | Utafutaji wa mafuta | Kutafuta mafuta na gesi | 7,876,828,479 | - | • Kukamilisha uchorongaji wa visima |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | na gesi katika kitalu cha Eyasi Wembere | asilia. | | | viwili (2) vifupi katika maeneo ya Kining'inila-Igunga na Nyaranja-Meatu katika Kitalu cha Eyasi – Wembere. |
| 490. | Utafutaji wa mafuta na gesi katika kitalu cha Mnazi Bay Kaskazini | Kutafuta mafuta na gesi asilia. | 994,708,581 | - | • Kukamilika kwa tathmini ya taarifa za kijiolojia na kijiofizikia na kumpata Mtaalamu Mshauri wa uchorongaji. |
| 491. | Kuunganishwa gesi asilia katika kiwanda cha Saruji Dangote | Ujenzi wa miundombinu ya kuunganisha gesi asilia katika kiwanda cha Dangote kwa ajili ya kuzalisha umeme na matumizi ya nishati ya gesi asilia kwa kuchoma malighafi za kuzalisha saruji. | 10,789,099,694 | - | • Kukamilika na kuwezesha matumizi ya gesi kuzalisha umeme kwa kiwanda cha Dangote ambapo hadi sasa Dangote anatumia gesi asilia wastani wa futi za ujazo milioni 5 kwa siku kwa kuzalisha umeme; na<br>• Kukamilika kwa awamu ya pili ya mradi wa ujenzi wa miundombinu ya bomba la kusafirisha gesi asilia kwenda kiwanda cha Dangote, umbali wa kilomita 2.7 kwa ajili ya kuwezesha gesi asilia kutumika kama nishati ya kuchoma malighafi za kuzalisha saruji. Kwa sasa Dangote anatumia gesi asilia wastani wa futi za ujazo milioni 15 hadi 20 kwa siku kwa ajili ya uzalishaji wa saruji.<br>• Mradi umekamilika |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| 492. | *Sustainable Energy for All* | • Kujenga uwezo katika masuala ya nishati endelevu<br>• Kuhamasisha upatikanaji wa nishati ya kisasa<br>• Kuhamasisha uendelezaji wa nishati jadidifu kwa kuwa na taarifa za maeneo ya nishaji jadidifu zinazowezesha uwekezaji<br>• Kuandaa miongozo ya uhamasishaji wa matumizi bora ya nishati | - | 321,833,714.00 | • Ubainishaji na uhakiki wa maeneo yanoyafaa kwa uzalizalishaji wa umeme wa nishati jua katika maeneo ya Same, Kilimanjaro; Zuzu, Dodoma na Mkwese, Manyoni.<br>• Kuanza kwa upembuzi yakinifu kwa eneo la Mkwese, Manyoni lenye uwezo wa kuzalisha zaidi ya MW 150 za umeme kwa kutumia jua.<br>• Uaandaaji wa miongozo ya utekelezaji wa jitihada za nishati endelevu kwa wote (Mkakati wa upatikanaji wa rasilimali, Mpango wa Uperembaji na tathimini, Mkakati wa mawasiliano n.k) ulikamilika<br>• Kukamilika kwa Mpango Kazi wa utekelezaji wa matumizi bora ya nishati<br>• Kuratibu maandalizi ya Mkakati wa Matumizi bora ya nishati.<br>• Kujenga uwezo wa kitasisi kupitia warsha na mikutano ya kimataifa. |
| 493. | Nishati Jadidifu | • Kuhamasisha na kuendeleza matumizi ya vyanzo jadidifu na mbadala vya umeme | 21,009,450,514.52 | 4,460,396,692.94 | • Kuwasilishwa kwa miradi mbalimbali ya umeme-jua katika Fungamano la Kimataifa la Nishati ya Jua *(International Solar Alliance)*; |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | kamavile jua, upepo, maporomoko madogo ya maji na *biogas*.<br>• Kuhamasisha matumizi bora ya nishati. | | | • Upatikanaji wa ahadi ya Dola za Kimarekani milioni 380 kutoka Serikali ya India katika mkutano wa kwanza wa wakuu wa nchi za International Solar Alliance uliofanyika Machi 2018;<br>• Kushirikiana na Serikali ya Morocco kupitia taasisi yake ya nishati endelevu *(Moroccan Agency for Sustainable Energy – MASEN)* kuendeleza miradi ya kuzalisha umeme-jua nchini yenye jumla ya MW 300;<br>• Kufanyika kwa tathmini ya awali katika maeneo ya Zuzu (Dodoma), Manyoni (Singida) na Same (Kilimanjaro) ili kubaini ukubwa wa maeneo na kiasi cha umeme kinachoweza kuzalishwa;<br>• Uzalishaji wa umeme kutokana na Tungamotaka na Biogas kufikia MW 42 kutoka MW 38 za mwaka 2016/17;<br>• Uzalishaji wa umeme kupitia maporomoko madogo ya maji kufikia MW 42 kutoka MW 36.99 |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | mwaka 2016/17;<br>• Kukamilisha tafiti nne (4) za kina (detailed surface studies) za uendelezaji wa nishati jadidifu katika maeneo ya Ngozi na Kiejo-Mbaka Mkoani Mbeya, Songwe Mkoani Songwe na Luhoi Mkoani Pwani;<br>• Kuandaliwa kwa Mkakati wa Kitaifa wa Matumizi Bora ya Nishati (Energy Efficiency Strategy) pamoja na kukamilisha maandalizi ya Mpango Kazi wa Matumizi Bora ya Nishati (Energy Efficiency Action Plan)<br>• Kutekelezwa kwa mradi wa uendelezaji wa Nishati Jadidifu kupitia Wakala wa Nishati Vijiji (REA) awamu ya Kwanza ambapo inahusisha usambazaji wa umeme vijijini kwa maeneo yaliyopo nje ya gridi kwa mfumo wa Malipo kwa Matokeo (Results Based Financing - RBF). Utekelezaji huu ulihusisha kusainiwa kwa Mikataba ya miradi 22 yenye uwezo wa kuzalisha jumla ya MW 24.4 zitakazosambazwa katika |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | vijiji 139 na kuunganisha wateja 33,939. Mikataba hiyo ilisainiwa kati ya REA na Waendelezaji wa Miradi na kazi hiyo katika Mikoa ya Iringa, Njombe, Tanga, Dodoma, Singida, Lindi, Mtwara, Tabora, Mwanza, Geita na Kagera.<br>• Kutekelezwa kwa mradi wa nishati jadidifu kupitia REA unaohusisha kufunga mifumo ya umeme-jua (solar PV systems) katika Taasisi za Umma zikiwemo shule za sekondari, vituo vya afya na zahanati zilizopo mbali na gridi pamoja na masoko ili kuboresha huduma zinazotolewa katika taasisi hizo. Mradi huu unatekelezwa katika Wilaya nane (8) za Biharamulo, Bukombe, Chato, Sikonge, Kasulu, Kibondo, Tunduru na Namtumbo. Utekelezajiwa mradi ulifikia asilimia 95.<br>• Kufanikisha maandalizi ya nyaraka za utaratibu wa upatikanaji wa miradi ya kuzalisha umeme kwa njia yaa ushindani.<br>• Kupitia TANESCO kutangazwa |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | miradi ya kuzalisha umeme kutumia jua (MW 150) na (MW 200) upepo. Jumla ya wawekezaji 18 walipitishwa kuwasilisha maandiko ya kuzalisha umeme kutumia jua na 13 kutumia upepo. |
| 494. | Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme ya Msongo wa Kv 220 kutoka Bulyanhulu- Geita. | Lengo la mradi ni kujenga njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 220 yenye urefu wa kilomita 55 kutoka Bulyanhulu hadi Geita. Mradi huu unahusisha ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Geita kV 220, upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Bulyanhulu, usambazaji wa umeme katika vijiji 10 vilivyopo ndani ya eneo la mradi na kubadilisha mita za umeme za kawaida (conventional meters) 1,500 mkoani Geita. | 1,000,000,000 | - | • Kukamilika kwa asilimia 82 ya ujenzi na upanuzi wa vituo vya kupoza umeme pamoja na ujenzi wa njia za kusafirisha umeme; na<br>• Kukamilika kwa ulipaji wa fidia kwa wananchi wanaopisha mradi.<br>• Kazi ya kuvuta nyaya kwa ajili ya usambazaji wa umeme vijijini imefikia asilimia 92.<br>• Utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 85. |
| 495. | Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme ya Msongo wa Kv 220 Rusumo – | Mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kV 220 yenye urefu wa kilomita | 5,200,000,000 | | • Kazi ya kulipa fidia kwa Wananchi waliopitiwa na mradi imekamilika;<br>• Kazi za usanifu na Upimaji udongo zimekamilika; na |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | Nyakanazi | 98 kutoka kituo cha kuzalisha umeme cha Rusumo hadi Nyakanazi. | | | • Kazi za kusafisha njia ya kujenga umeme na ujenzi wa barabara za kando kando ya njia kuu ya umeme (access road construction) na kusanifu nguzo zitakavyokaa kwenye njia kuu ya kusafirisha umeme (Tower Spotting) zinaendelea. |
| 496. | Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme ya Msongo wa Kv 220 Ya Geita – Nyakanazi | Lengo la mradi ni kujenga njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 220 yenye urefu wa kilomita 144 kutoka Geita hadi Nyakanazi (Lot A), Vituo vya kupozea umeme vya Geita na Nyakanazi (Lot B) na usambazaji wa umeme katika vijiji 32 katika eneo la Geita hadi Bwanga na Nyakanazi mpaka Kakonko (Lot C). | 6,794,619,458 | - | • Kukamilika kwa upimaji wa udongo na usanifu wa mradi;<br>• Kukamilika kwa ulipaji wa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi; na<br>• Kuanza ujenzi wa kituo cha kupoza umeme. |
| **JUMLA NDOGO** | | | **3,198,730,559,737.96** | **863,865,154,128.01** | |
| **WIZARA YA KILIMO** | | | | | |
| 497. | Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili *ASDP II* | • **Mafunzo:** Kudahili na kufundisha wanafunzi 2,500 ngazi ya Astashahada na Stashahada, Kukarabati | 74,165,664,903.10 | 2,052,600,357.00 | • **Mafunzo:** Serikali ilifadhili na kufundisha wanafunzi 3,987 kwenye mafunzo ya kilimo ngazi ya Astashahada na Stashahada katika |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | miundombinu ya vyuo vya mafunzo ya Kilimo Mlingano, KATC, HORTI Tengeru, Maruku, Ukiriguru, Tumbi na Mubondo.<br><br>• **Utafiti na Maendeleo:** | | | Vyuo vya Ilonga, Mlingano, Mtwara, Tumbi, Ukiriguru, Uyole, HORTI Tengeru, Mubondo, Maruku, KATC Moshi, Igurusi, KATRIN, Chuo cha Sukari Kidatu na Inyala.Vile vile, kudahiliwa kwa wanafunzi 684 wanaojilipia katika ngazi ya Astashahada na Stashahada. Wanafunzi 2,121 wa ngazi ya Stashahada na Astashahada walihitimu masomo yao.<br>• Ukarabati wa jengo la utawala na bweni katika Chuo cha kilimo Mubondo umekamilika kwa asilimia 70; bweni la wasichana MATI Mlingano kwa 90%; jengo la utawala, nyumba za watumishi, madarasa, mabweni na vyoo katika Chuo cha Inyala 60%. Vile vile kwa mwaka 2019/20 ukarabati wa majengo ya vyuo vya kilimo Maruku, HORTI Tengeru, Mlingano, Tumbi, Igurusi na Mtwara upo kwenye hatua ya uchambuzi.<br><br>• **Utafiti wa mbegu** |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | Kutafiti teknolojia za kilimo kwa kuzingatia mnyororo wa thamani kwa mazao ya kipaumbele; Kukarabati na kuvipatia vifaa muhimu vya kufanyia utafiti vituo 7 vya utafiti (Ukiriguru, Ilonga, Seriani, Tumbi, Naliendele, Uyole na Makutopora) na kukarabati kituo cha Taifa cha Utunzaji Nasaba za Mimea ili kiweze kutoa huduma bora. | | | Jumla ya miche bora ya korosho 37,816 imezalishwa na kusambazwa kwa wakulima wa mikoa ya Mtwara (7,155), Lindi (20,156), Pwani (6,950), Ruvuma (2,000), Tanga (1,120), Dodoma (135), Singida (200) na Dar es Salaam (100).<br><br>Aidha, jumla ya mbegu bora 13 zimegunduliwa. Kati ya mbegu hizo, aina nne (4) za mahindi (WE5135, WE5141, WE7118 na WE7133) zimegunduliwa na TARI kwa ajili ya matumizi ya wakulima. Mbegu nyingine tisa (9) zimegundiliwa na mashirika ya Utafiti mengine ya binafsi na ya umma. Mbegu hizo ni: zao la tumbaku (TRD 17) kutoka TORITA, Mahindi (EAS 5019) kutoka Kampuni ya East African Seed, Mahindi (AMH500, AMH501) kutoka Kampuni ya Alssem Seed, Mahindi (SY6444, SY 5344) kutoka kampuni ya syngenta, Soya (SC Semeki, SC Signal, SC Saxon) kutoka kampuni ya Seed Co. Tanzania Ltd. |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | Vile vile, TARI kupitia ufadhili wa COSTECH imefanya ukarabati wa mitambo ya kuchakata mzabibu kilichopo Makutopora, Dodoma. Aidha, ukarabati wa maabara ya Bioteknolojia katika kituo cha TARI Tengeru unaendelea na umefikia hatua nzuri. Ambapo, hadi kufikia Desemba 2019/20 TARI imegundua aina 22 za mbegu bora za mazao. Kati ya hizo aina 9 ni za muhogo, aina 2 ni za alizeti, 2 za mahindi, 2 za mpunga, 1 ya ulezi, na 6 ni za viazi vitamu. Mbegu za muhogo zina sifa za kustahimili ugonjwa wa michirizi kahawia na batobato na zinatoa mavuno kati ya tani 25 hadi 30 kwa hekta. Mbegu za alizeti zina kiwango kikubwa cha mafuta ukilinganisha na mbegu zilizopo, mbegu za viazi vitamu zina virutubisho vya vitamini A. Aidha, mbegu za mpunga zinatoa mavuno kati ya tani 7.3 hadi 7.9 kwa hekta na zina harufu nzuri na kupikika vizuri, wakati mbegu za mahindi zinatoa mavuno kati ya tani |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | • Upatikanaji na usambazaji wa mbolea | | | 7 hadi 10 kwa hekta na zina ukinzani dhidi ya ugonjwa wa Maize Streak na Turcium Blight virus.<br>• Kuweka vifaa vya kutunza ubora wa nafaka katika maghala 79 yanayohifadhi Mahindi katika Mikoa ya Rukwa – Halmashauri ya Kalambo (9), Ruvuma – Songea Vijijini (20), Songwe – Mbozi Vijijini (20), Mbeya – Mbeya Vijijini (13), Iringa – Mufindi (10), Njombe - Njombe Vijijini (7). Hadi kufikia mwisho wa msimu wa ununuzi, Wakala wa Hifadhi ya Chakula ya Taifa umefanikiwa kununua jumla ya tani 62,087.997 za Mahindi sawa na asilimia 62 ya lengo.<br>• Upatikanaji na usambazaji wa mbolea katika mikoa 26 ya Tanzania Bara ulifikia tani 492,394 ikilinganishwa na mahitaji ya tani 514,138 katika msimu wa 2018/19. Katika mwaka 2018/19, wafanyabiashara wapya wa mbolea 496 wamesajiliwa na kufikia idadi ya wafanyabiashara wa mbolea 2,784 |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | nchini wanaonunua na kusambaza mbolea kwa wakulima. Aidha, katika mwaka 2019/20 mahitaji ya mbolea yalikuwa tani 586,604 na hadi kufikia Februari, 2020 upatikanaji wa mbolea umefikia tani 519,813 sawa na asilimia 89. Kati ya kiasi hicho, tani 168,397 ni bakaa ya msimu wa 2018/19, tani 17,832 zimezalishwa ndani ya nchi na tani 333,583 zimeingizwa kutoka nje ya nchi na tani za mbolea 197,596 zilitokana na mfumo wa BPS ambapo tani 103,340 (Urea tani 74,840 ba DAP tani 28,500) ziliagizwa katika mwaka 2019/2020 na tani 94,256 ni baada ya mwaka 2018/19.<br><br>• Katika mwaka 2018/19, upatikanaji wa mbegu bora zikiwemo za mahindi, ngano, maharage, mpunga, soya, alizeti, mtama, ufuta, viazi mviringo na mbegu za mazao ya bustani umefikia tani 49,040.66. Kati ya kiasi hicho, tani 38,507.87 zimezalishwa hapa nchini, tani |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | 8,361.46 zimeagizwa toka nje ya nchi na tani 2,171.33 ni bakaa ya msimu wa 2017/18. Vile vile, miche bora 1,507 ya miwa, vipando 121,805 vya muhogo na vikonyo 520,000 vya viazi lishe vimezalishwa. Pia, aina mpya 13 za mbegu bora zikiwemo tisa (9) za mahindi, soya tatu (3) na tumbaku moja (1) zimeidhinishwa na zitakazoanza kuzalishwa msimu wa 2019/2020. Aidha, upatikanaji wa mbegu bora nchini hadi kufikia Desemba ,2019 ni tani 71,155.13, kati ya hizo tani 34,678.54 ni za nafaka, mikunde, mbegu za mafuta na bustani; tani 35,000 ni za pamba na tani 1,476.61 ni za viazi mviringo, tumbaku na malisho.<br><br>• Udhibiti wa Ubora wa mbegu umefanyika ambapo, hekta 42,999.6 za mashamba ya mbegu, maduka 713 na maghala 43 ya mbegu yamekaguliwa katika mikoa ya Mbeya, Arusha, Morogoro, Rukwa na Mwanza. Vilevile, kutokana na |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | • **Maendeleo ya Mazao;** Kudhibiti visumbufu vya milipuko (Kwelea kwelea, | | | kuimarishwa kwa TOSCI kupitia ujenzi wa miundombinu ya kisasa ya maabara na rasilimaliwatu, Serikali imepata ithibati ya Shirika la Kimataifa la Uthibiti wa Ubora wa Mbegu (International Seeds Testing Association – ISTA) kwa maabara ya TOSCI ambayo itaiwezesha nchi kufanya biashara ya mbegu kimataifa. Hadi kufikia Desemba 2019 hekta 819.8 za mashamba ya mbegu zimekaguliwa; tani 13,000 za mbegu zimekaguliwa katika maghala 70 na maduka 633 ya wafanyabiashara wa mbegu yamekaguliwa na 87 yalifungwa.<br>• Uzalishaji wa jumla kwa mazao ya kimkakati umeongezeka kutoka tani 901,641 msimu wa 2016/17 hadi tani 967,184 msimu wa 2017/18 sawa na ongezeko la asilimia 7.2.<br><br>**Maendeleo ya Mazao**<br>• Katika kuendeleza mazao, miche bora ya korosho 12,252,197 imesambazwa katika mikoa 17 |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | viwavijeshi Panya na Nzige), na magonjwa ya mimea. | | | inayolima zao hilo. Vilevile, mbegu za korosho kilo 47,484 ambazo zitazalisha miche 6,647,760 ya kutosheleza ekari 391,045.19 zimezalishwa na Kituo cha Utafiti cha Naliendele. Kwa upande wa zao la kahawa, jumla ya miche bora 6,494,930 imezalishwa. Vile vile, upatikanaji wa mbegu za pamba UKM08 ulifikia tani 21,535.62 ambazo zilisambazwa kwa wakulima. Miche bora ya chai milioni 7.13 imezalishwa ambapo miche milioni 3.1 imesambazwa kwa wakulima katika wilaya za Njombe, Ludewa, Tarime, Rungwe na Mufindi.<br><br>• Jumla ya tani 31,500 na lita 520,000 za salfa kwa ajili ya zao la korosho zimenunuliwa ambapo wakulima wamenunua tani 1,994.175 na lita 14,283.<br><br>• Ekapaki milioni 3.3 za viuatilifu vya zao la pamba vilisambazwa katika Halmashauri 41 za mikoa ya |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | • **Usalama wa Chakula;** | | | Kigoma, Katavi, Singida, Dodoma, Kagera, Mara, Tabora, Geita, Mwanza, Shinyanga na Simiyu.<br><br>• Katika kipindi cha mwaka 2019/20, mahitaji ya viuatilifu vya korosho yalikuwa ni tani 30,000 za salfa ya unga na lita 500,000 vya viuatilifu vya maji. Ambapo, hadi kufikia Desemba, 2019 upatikanaji umefikia tani 19,000 za salfa ya unga na lita 270,000 za viatilifu vya maji. Viuatilifu hivyo vimeuzwa kwa wakulima kupitia vituo vya mauzo vilivyopo kwenye mikoa na wilaya zinazolima korosho nchini. Matumizi ya viuatilifu kwa ajili ya zao la pamba unatarajiwa kufikia Ekapaki 8,000,000 ambazo zitatosheleza ekari milioni 8. Aidha, Serikali imepanga kununua na kusambaza mabomba 20,000 yatakayotumika kupulizia dawa katika zao la pamba.<br><br>• **Usalama wa Chakula:** Hadi kufikia tarehe 09 Agosti 2019, Wakala wa |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | Kusimamia ujenzi wa maghala ya kimkakati katika mikoa ya Mwanza, Kagera, Kigoma, Singida, Tanga, Tabora na Manyara. | | | Hifadhi wa Chakula wa Taifa aliweza kununua jumla ya tani 788.782 za mahindi sawa na asilimia 0.72 ya lengo la tani 110,000.00 na ukarabati maghala 105 yenye uwezo wa kuhifadhi tani 31,500 katika Halmashauri za Mbozi (46), Momba (4), Mbeya (13), Iringa (11), Mufindi (10), Njombe (4), Kalambo (9) na Songea/Madaba. Ambapo, hadi kufikia Desemba 2019, NFRA ilikuwa imenunua jumla ya tani 3675.056 sawa na asilimia 3.5 ya lengo la ununuzi kupitia mapato yake ya ndani. |
| 498. | Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili *(ASDP II)* | Kuleta mageuzi ya Sekta ya kilimo (kilimo, mifugo na uvuvi) ili kuongeza uzalishaji na tija, kukifanya kilimo kiwe cha kibiashara zaidi na kuongeza pato la wakulima wadogo wadogo kwa ajili kuboresha maisha yao, usalama wa chakula na lishe. | 35,001,828,000.00 | | • Ununuzi wa mahindi na ufungaji wa mashine za kusaga mahindi na kukamua mbegu za alizeti: Bodi ya nafaka na mazao mchanganyiko imenunua mahindi tani 6,200.89 na alizeti tani 621 na kusagisha tani 3,820.96 za mahindi ambazo zimetoa tani 2,808.05 za unga wa mahindi na tani 1,024.80 za pumba. Aidha Bodi imefunga mashine za kukamua mafuta ya alizeti na kusaga mahindi |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | katika eneo la Kizota Jijini Dodoma ambapo hadi kufikia Juni 30, 2019 kazi hizo zimefikia asilimia 98 kwa jengo la mahindi na asilimia 96 kwa jengo la alizeti. Mashine hizo zitakuwa na uwezo wa kusaga tani 60 za mahindi kwa siku na kukamua mafuta ya mbegu za alizeti tani 20 kwa siku.<br>• Zao la korosho: Katika mwaka 2019/20, Wizara kupitia Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko ilipanga kununua tani 275,198 za korosho za msimu wa mwaka 2018/19. Hadi kufikia Desemba 2019 tani 222,561.179 za korosho ghafi zimenunuliwa kutoka kwa wakulima sawa na asilimia 81 ya lengo. Hadi kufikia Februari 2020, tani 210,445.524 za korosho ghafi za msimu wa 2018/19 zimeuzwa ambapo tani 148,077.892 ziliuzwa kwa utaratibu wa Malipwani (FOB) na tani 62,367.632 ziliuzwa kwa utaratibu wa malighalani (ex-warehouse) thamani ya korosho |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | zilizouzwa ni dola za Kimarekani 233,864,795.62 na shilingi 3,246,739,000.<br><br>• **Akiba ya chakula**<br>Katika mwaka 2019/2020 Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula ulipanga kununua tani 110,000 za nafaka. Wakala ulianza msimu wa ununuzi wa nafaka tarehe 23 Julai, 2019 ukiwa na akiba ya tani 67,335.917 za nafaka ambazo ni bakaa ya mwaka 2018/2019. Hadi kufikia Desemba, 2019, jumla ya tani 3,841.863 za mahindi zilikuwa zimenunuliwa, sawa na asilimia 3.5 ya lengo la ununuzi. Hali hii ilisababishwa na upatikanaji mdogo na bei kubwa ya mahindi. Wakala umeendelea kuhudumia mahitaji ya dharura ya chakula pamoja na kukabiliana na mfumuko wa bei ya nafaka katika baadhi ya Halmashauri nchini na upungufu wa chakula katika nchi jirani. Kati ya jumla ya tani zilizonunuliwa; tani 18,679.683 zimeuzwa. Kati ya hizo, tani 17,000 |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | • **Skimu ya umwagiliaji;** Kufanya upembuzi yakinifu, usanifu wa kina, kujenga na kukarabati skimu za umwagiliaji pamoja na kuanzisha vyama vya umwagiliaji | | | ziliuzwa nchini Zimbabwe na tani 1,679.683 zimeuzwa ndani ya nchi na hivyo kufanya wakala kubaki na akiba ya tani 52,498.097 za chakula katika maghala yake.<br>• Katika mwaka 2018/19, lita 296,000 na kilo 3,000 za viuatilifu vyenye thamani ya Shilingi bilioni tisa (9) zimenunuliwa kwa ajili ya kukabiliana na milipuko ya visumbufu vya mazao vikiwemo Viwavijeshi vamizi, Kweleakwelea, Panya, Nzige wekundu, na nzi wa matunda. Lita 119,000 zilisambazwa kwa ajili ya kudhibiti Viwavijeshi Vamizi katika Kanda ya Ziwa, Nyanda za Juu Kusini, Kanda ya Kati, Kanda ya Magharibi, Kanda ya Kaskazini na Kanda ya Mashariki.<br>• Ukarabati na ujenzi wa mabwawa ya Usoke (Urambo), Itagata (Manyoni) na Dongobesh katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu umekamilika. Upembuzi yakinifu wa mabwawa ya Lwanyo na Gidahababierg katika Halmashauri ya Wilaya ya Hanang’ |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | katika maeneo mbalimbali nchini | | | umekamilika. Vilevile, Upembuzi yakinifu katika skimu za Ibanda (Geita/Sengerema) na Luiche (Kigoma) umefikia wastani wa asilimia 60. Aidha, jumla ya vyama vya wamwagiliaji 161 vilivyosajiliwa. |
| 499. | Mradi wa Kuongeza Uzalishaji wa Zao la Mpunga *(Expanding Rice Production Project – ERPP)* | Kuongeza uzalishaji wa mazao ya mpunga na kuimarisha upatikanaji wa pembejeo za kilimo.<br><br>• Kuimarisha mfumo endelevu wa mbegu | 87,050,000 | 16,874,694,118 | • Kutambulisha aina 11 ya mbegu mpya za mpunga kwa wakulima katika skimu/vijiji 40: Aina 11 za mbegu mpya za mpunga [TXD 306, TXD 88, TXD 85, Tai, Kalalu na Komboka) ambazo zinafaa kwa kilimo cha mabondeni; NERICA 1, NERICA 2, NERICA 4 na NERICA 7 ambazo zinafaa kwa kilimo cha maeneo ya miinuko (upland)] zilitambulishwa kwa wakulima kupitia mashamba ya mfano yapatayo 130 yaliyoendeshwa msimu wa 2016/2017 na 91 yaliyoendeshwa msimu 2017/2018 katika wilaya 7 za Mkoa wa Morogoro. Mwaka 2018/2019 wakulima waliwezeshwa kuchagua aina 2 za mbegu walizopendelea |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | zaidi. Mbegu walizochagua ni TXD 306 (SARO 5) kwa kilimo cha mabondeni na NERICA 7 kwa kilimo cha maeneo ya miinuko (upland).<br>• Hadi kufikia Desemba 2019, jumla ya mbegu za Mpunga 11 zimesafishwa kupitia Mradi wa Kuongeza Uzalishaji wa Mpunga (ERPP) unaotekelezwa na kituo cha utafiti TARI Ifakara. Kati ya hizo, tano (5) zinazolimwa maeneo ya bondeni na umwagiliaji (TXD 306, TXD 88, Komboka, Tai, Supa) na sita (6) zinazolimwa maeneo ya milimani (NERICA 1, NERICA 2, NERICA 4, NERICA 7, WAB 450-12-2-BL1-DV4). Aidha, kituo kimezalisha tani 13.8 za mbegu mama na za msingi za mpunga ((TXD 306 tani 5.1, TXD 88 tani 2.6, KOMBOKA tani 2.3, NERICA 7 tani 1.4, SUPA tani 2.4). |
| | | | | | • Kuhamasisha uzalishaji endelevu wa mbegu za mpunga: Tani 27.3 za mbegu za awali (pre-basic); tani 48.4 |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | za mbegu mama (basic seeds) na tani 156 ya mbegu zilizopasishwa (certified seeds) zilizalishwa katika msimu wa 2016/17 na 2017/18. Katika msimu wa 2018/19, TARI Ifakara ililima eneo la hekta 3.5 kwa ajili ya kuzalisha mbegu za awali za mpunga (pre-basic rice seeds) aina ya TXD 306, TXD 88, Komboka, Supa na NERICA 7. Kwa sasa uchakataji wa mbegu hizo unafanyika ili kupata kiasi halisi kilichozalishwa. Aidha ASA ilizalisha katika eneo la hekta 80 mbegu mama za mpunga aina ya TXD 306 (hekta 10) na mbegu za daraja la upasishwa aina ya TXD 306, TXD 88 na Supa katika eneo la hekta 70. Uvunaji na uchakataji wa mbegu hizo unaendelea. Ili kuongeza uzalishaji wa mbegu bora za mpunga kukidhi mahitaji ya wakulima, tarehe 19 Desemba 2018, Mradi kwa kushirikiana na Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA), Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) Kituo cha Ifakara na Taasisi ya Kudhibiti |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | Ubora wa Mbegu Tanzania (TOSCI) ulifanya kikao pamoja na Kampuni Binafsi 11 na kuzifahamisha kuhusu fursa zilizopo za kuzalisha mbegu za mpunga. Kampuni zilionesha nia ya kuzalisha mbegu za mpunga aina ya TXD 306 na NERICA 7.<br>• Kuimarisha udhibiti wa ubora wa mbegu: Mashamba kwa ajili ya kuzalisha mbegu yaliandikishwa na ukaguzi kufanyika wakati mimea ikiwa mashambani; uhakiki umefanyika kujua kiasi cha mbegu zilizozalishwa kutoka TARI Ifakara, TARI Dakawa, ASA na kutoka wakulima waliozalisha mbegu zenye ubora wa kuazimiwa (Quality Declared Seeds – QDS).<br>• TOSCI imefanya uchunguzi wa kimaabara wa mbegu na kukagua mbegu katika maghala/maduka yanayouza mbegu.<br>• Wakaguzi wa mbegu waliopasishwa wapatao 18 kutoka Wilaya za Kilosa, Kilombero, Mvomero, Ulanga, Malinyi na Gairo walipatiwa |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | mafunzo ya ukaguzi wa ubora wa mbegu.<br>• Wakulima 23 kutoka wilaya za Kilombero, Kilosa, Mvomero, Malinyi na Mji wa Ifakara walipatiwa mafunzo ya kuzalisha mbegu zenye ubora wa kauzimiwa (QDS).<br><br>Aidha, hadi kufikia Desemba, 2019 mafunzo ya kilimo bora cha mpunga ikiwemo kilimo shadidi yalitolewa kwa wakulima 5,647, Maafisa Ugani na Mafundi Sanifu wa Umwagiliaji 109 kutoka skimu 40 za umwagiliaji. Vile vile, wakulima viongozi 40 kutoka skimu nne (4) za Mkindo, Kigugu, Dihombo na Mbogokomtonga wamepewa elimu kuhusu teknolojia bora za uvunaji, hifadhi na usindikaji wa mpunga.<br><br>• Maafisa 13 kutoka TARI Ifakara, TARI Dakawa na ASA walipatiwa mafunzo ya uzalishaji na udhibiti wa ubora wa mbegu.<br>• Sampuli za mbegu za mpunga aina ya |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | TXD 306, TXD 88, Komboka, Tai na NERICA 7 kutoka TARI Ifakara, TARI Dakawa na ASA zilifanyiwa uhakiki wa usafi (purity verification).<br>• Mbegu za mpunga aina ya TXD 306, TXD 88, TXD 85, Komboka, Tai, Supa, NERICA 1, NERICA 2, NERICA 4, NERICA 7 na WAB 450-12-2-BL1-DV4 zilioteshwa na kusafishwa (purification) katika eneo la hekta 1.5 lililopo TARI Ifakara.<br>• Ujenzi wa jengo la maabara ya mbegu katika Makao Makuu ya ASA Morogoro umekamilika. |
| 500. | | • Ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji na uhamasishaji wa matumizi ya kanuni bora za uzalishaji wa mpunga; | | | • Ukarabati/ujenzi wa miundo mbinu ya umwagiliaji: Ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji ya skimu za Kigugu (hekta 200) [Mvomero]; Mvumi (hekta 249) [Kilosa]; Msolwa Ujamaa (hekta 675) na Njage (hekta 325) [Kilombero], barabara za kuingia katika skimu ya Mvumi yenye urefu wa kilomita 8 na Njage kilomita 7, pamoja shamba la mbegu la Kilangali (hekta 400 umeanza. Aidha wajumbe 311 wa |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | Umoja wa Umwagiliaji (Irrigator Organization) kutoka skimu za umwagiliaji za Njage, Msolwa Ujamaa Mvumi, Kigugu na Mbogo Komtonga wamepatiwa mafunzo ya kuimarisha na kuendesha umoja wao; usimamizi na matengenezo ya miundombinu ya umwagiliaji; utunzaji wa kumbukumbu; usimamizi wa fedha na usuluhishi wa migogoro.<br>Aidha, hadi kufikia Desemba 2019 Ujenzi wa Maghala ya kuhifadhi mazao kupitia Mradi wa Kuongeza Uzalishaji wa Mpunga (ERPP) imefikia hatua mbalimbali (Msola Ujamaa – 86%), (Mbogo kwa Mtongo – 80%), (Mvumi – 100%), (Njage – 90%), na (Kigugu – 84%) |
| 501. | | • Kuhamasisha matumizi ya kanuni bora za uzalishaji wa mpunga | | | • Kuhamasisha matumizi ya kanuni bora za uzalishaji wa mpunga: Maafisa Ugani/Mafundi Sanifu wa Umwagiliaji 109 na wakulima 5,647 kutoka skimu za umwagiliaji 40 wamepatiwa mafunzo ya kilimo shadidi cha mpunga (System of Rice |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | Intensification – SRI). Mashamba darasa ya SRI yapatayo 1,331 yaliendeshwa katika mwaka wa 2017/2018. Aidha wataalamu 40 na wakulima 268 waliwezeshwa kushiriki ziara za mafunzo ndani ya nchi kuhusu mnyororo wa thamani wa zao la mpunga.<br>• Vile vile wakulima 3,534 waliopata mafunzo walichangia asilimia 50 ya gharama za pembejeo na kupatiwa pembejeo kwa ajili ya kilimo shadidi cha mpunga. Wakulima 168 waliwezeshwa kufanya ziara ya mafunzo ndani ya nchi kuhusu mnyororo wa thamani wa zao la mpunga. Maafisa Ugani/Fundi Sanifu wa Umwagiliaji wapatao 60 walipatiwa mafunzo ya kilimo shadidi cha mpunga yaliyofanyika TARI Dakawa. Wakulima 320 kutoka halmashauri 6 za Mkoa wa Morogoro wamepatiwa mafunzo ya kilimo shadidi cha mpunga yaliyofanyika TARI Dakawa. Sekretariati ya Mkoa wa Morogoro |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | pamoja na Halmashauri za Wilaya 6 ziliwezeshwa fedha za kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa mradi wa ERPP katika maeneo yao |
| 502. | | • Mikakati bunifu ya masoko | | | • Kujenga miundombinu ya uhifadhi ili kurahisisha masoko: Usanifu wa maghala matano ulifanyika na kukamilika. Ujenzi wa maghala katika skimu za Mbogo Komtonga na Kigugu (Mvomero); Mvumi (Kilosa); Njage na Msolwa Ujamaa (Kilombero) umeanza na kwa wastani umefika asilimia 26.<br>• Kuimarisha mfumo na taarifa na upatikanaji wa masoko: Utambuzi wa wadau wa mnyororo thamani wa zao la mpunga pamona na utafiti wa mfumo wa masoko ya mpunga katika mkoa wa Morogoro umefanyika. Aidha, mwongozo wa kufundisha wakulima masuala ya masoko umeandaliwa. Wakulima viongozi wapatao 40 na Wataalam 6 kutoka Wilaya ya Mvomero wamepatiwa mafunzo ya usimamizi wa mpunga baada ya kuvunwa ili |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | kupunguza upotevu. |
| 503. | | • Uratibu na Usimamzi wa Mradi | | | • Uratibu na usimamizi wa mradi umefanyika na unaendelea. Magari 6, pikipiki 6, vifaa vya ofisi na mahitaji mengine ya ofisi yalinunuliwa na kutumika kufanikisha utekelezaji wa mradi.<br>• Vikao vinne vya kamati ya usimamizi wa mradi (Technical Steering Committee Meeting) na vitatu vinavyojumuisha Bara na Zanzibar (Joint Steering Committee Meeting) vimefanyika. Benki ya Dunia imefanya ziara 6 za ufuatiliaji wa utekelezaji wa mradi pamoja na mapitio ya muda wa kati wa utekelezaji (Mid-Term Review - MTR). Aidha mafunzo ya usimamizi wa mikataba (contract management) yalifanyika Morogoro na kuhudhuriwa na maafisa 17 kutoka Wizara ya Kilimo na Halmashauri za Wilaya za Mvomero, Kilosa na Kilombero. Benki ya Dunia iliendesha mafunzo hayo.<br>**Kutekeleza masuala ya mazingira** |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | **na jamii katika mradi:**<br>• Mipango ya Usimamizi wa Mazingira na Jamii (Environmental and Social Management Plans) imeandaliwa kwa skimu za Kigugu, Mbogo Komtonga, Mvumi, Msolwa Ujamaa, Njage na Shamba la Mbegu la Kilangali. Ufuatiliaji wa utekelezaji wa masuala ya usimamizi wa mazingira na jamii pamoja na mfumo wa wakulima kuwasilisha malalamiko (Grievance Redress Mechanism- GRM) yatokanayo na utekelezaji wa mradi umefanyika na unaendelea katika skimu za Kigugu, Mbogo Komtonga, Mvumi, Msolwa Ujamaa na Njage na Shamba la Mbegu la Kilangali. Mpango wa Uhaulishaji (Resettlement Action Plan) na Usimamizi wa Mazingira na Jamii ya ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji ya shamba la mbegu la ASA-Kilangali umeandaliwa na kukamilika. Mwongozo wa Wakulima wa Mbinu Husishi za Kudhibiti Visumbufu vya Mimea na |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | Matumizi Salama ya Viuatilifu uliandaliwa na kukamilishwa. Tathmini ya Athari za Mazingira na Jamii kwa skimu ya Mbogo Komtonga inafanyika. Wakulima 829 (wanaume 485 na wanawake 344) wamepatiwa mafunzo ya usimamizi wa maji ya umwagiliaji ili kupunguza magonjwa yaenezwayo kupitia maji kama vile kichocho. Wakulima hao walitoka skimu za umwagiliaji za Mkindo, Kigugu na Mbogo Komtonga (Mvomero); Mvumi na Chanzuru/Ilonga (Kilosa); Njage na Msolwa Ujamaa (Kilombero); Tulo Kongwa (Morogoro), Minepa (Ulanga) na Itete (Malinyi). |
| 504. | Mpango wa kuendeleza Kilimo Ukanda wa Kusini mwa Tanzania (*Southern Agriculture Growth Corridor of Tanzania (SAGCOT)*) | Kuchochea uwekezaji mkubwa wa sekta binafsi ili kufanikisha ukuaji haraka wa kilimo endelevu, kuwepo kwa uhakika wa chakula, kupungua kwa hali ya umasikini na kupunguza athari za mabadiliko ya tabia | 2,903,148,058 | 0 | • Kuendeleza kongane sita zenye tija katika uzalishaji, uongezaji wa thamani wa mazao, upatikanaji wa wasambazaji wa pembejeo, Masoko na watoa huduma mbalimbali *(key private service provide)*<br>• Kuwaunganisha wakulima na wadau wa kilimo ili kuleta tija, kuongeza |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | nchi. | | | kipato kwa wakulima na kuongeza chakula na lishe kwenye kaya za wakulima wa Viazi vitamu, Soya, Nyanya, Chai na wafugaji wa ng'ombe wa maziwa *(High potential commodities in clusters).*<br>• Kulimwa kwa hekta 38,477 za mazao kwa kutumia teknolojia bora za kilimo kama vile utumiaji wa mbegu bora na matumizi ya njia bora na za kisasa za umwagiliaji.<br>• Wakulima wadogo 16,384 wamefikiwa na kampuni binafsi zinazoshirikiana na SAGCOT na wameshirikishwa kwa kutumia njia mbalimbali za ushirikishwaji.<br>• Jumla ya fursa mpya za ajira za kudumu 547 zimetolewa kupitia shughuli za uongezwaji thamani wa mazao kupitia kampuni binafsi 17 zinazoshirikiana na kituo cha SAGCOT.<br>• Kupatiwa mafunzo kwa wakulima 752 juu ya kilimo bora, mfano kikundi cha Mtanga kilichopo Iringa Vijijini kinacholima viazi Mviringo |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | na Kikundi cha kina mama kinacholima soya kulichopo Ludewa Mkoani Njombe.<br>• Mfuko wa SAGCOT *Catalytic Trust Fund* umetoa ufadhili wa ujenzi wa ghala la kuhifadhia mpunga pamoja na ukarabati na ujenzi wa barabara zinazounganisha ghala na skimu ya umwagiliaji ya Mwendamtitu katika kijiji cha Mwakaganga, Kata ya Ubaruku, Wilayani Mbarali. Ghala linauwezo wa kuhifadhi tani 7,500 za mpunga. Utaratibu wa matumizi ya ghala umeandaliwa ambapo wakulima wapatao 450 wameandikishwa katika matumizi ya ghala hilo na kuweka utaratibu wa marejesho ya uwekezaji uliofanyika.<br>• Mfuko umefadhili uanzishwaji wa mfumo wa taarifa za kilimo na mkulima mdogo kupitia kanzi data kama nguzo muhimu ya utoaji wa ufadhili wa miradi ya kilimo biashara. Mfuko umenunua *cloud server* kwa ajili ya mfumo huu pamoja na kuwalipa wakandarasi katika hatua mbili za |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | mwanzo za uundwaji wa mfumo na uwekaji mfumo katika *cloud server* hizo. Hatua iliyofikia hadi sasa katika mfumo huo ni uingizwaji wa taarifa za wakulima na wafugaji wapatao 300 wa kuanzia ili kuhakiki namna mfumo utakavyofanya kazi kabla ya kuingiza taarifa za wakulima wengi zaidi. Mfumo huu unahusisha wakulima wa maziwa katika Wilaya za Rungwe, Busokelo (Mbeya) Njombe, Njombe Mji na Mkambako (Njombe) kupitia makampuni ya ASAS Dairies na *Njombe Milk Factory*. Mfumo huu pia unahusisha wakulima wa mpunga katika Wilaya za Mbarali, Kyela na Momba kupitia kampuni ya Mtenda Kyela Rice. Mfumo unatekelezwa kwa ubia na makampuni ya Litenga Holding, Animal Breeding East Africa (ABEA) na Chuo Kikuu cha Tekinolojia Cha Nelson Mandela- Arusha.<br>• Kilimo hifadhi kina endelezwa katika mikoa ya Iringa, Njombe na |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | wakulima wanafundishwa matumizi ya chokaa ya kilimo. Uwekezaji unaofanyika sasa unaingiza wastani wa US$ 22 milioni kwa mwaka na kuchangia kupunguza hali ya umasikini. Aidha, hadi kufikia Desemba 2019, jumla ya wakulima 2600 wameunganishwa na masoko kupitia mfumo wa farmers electronic monitoring system ambapo wakulima 1,500 waliunganishwa na soko la Mtenda Kyela Rice Supply Ltd, wafugaji 400 waliounganishwa na soko la ASAS Dairies Ltd, na Wafugaji 700 waliounganishwa na soko la Njombe Milk Factory Ltd. |
| 505. | Mradi wa Kuongeza Uhifadi wa Nafaka) *(Storage Capacity Expansion Project)* | • Kuongeza uwezo wa hifadhi kwa kujenga Vihenge vya kisasa na maghala kwa tani 250,000 ifikapo 2020. | 736,621,000.00 | 60,662,641,412.73 | • Asilimia 81.63 ya vifaa vimeingizwa nchini kwa ajili ya ujenzi katika vituo vya Makambako, Mbozi, Songea, Shinyanga na Dodoma;<br>Ujenzi wa vihenge umefikia asilimia 48.30 ambapo eneo la ujenzi wa maghala na vihenge la Babati, Mpanda na Sumbawanga limekabidhiwa kwa mkandarasi mwezi Desemba 2018 na taratibu za |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | ujenzi zinaendelea. Aidha makadirio ya ukarabati (BOQ) kwa ghala za Kipawa, Singida na Musoma yamekamilika. Vile vile mfumo wa umeme katika ghala la Laela umekamilika. |
| 506. | Mradi wa Kudhibiti Sumukuvu (Tanzania Initiative for Preventing Aflatoxin contamination project) | • Kudhibiti sumu kuvu (Aflatoxin) katika mazao ya Mahindi na Karanga kwa kuimarisha miundombinu, Teknolojia na Usimamizi wa mazao kabla na baada ya mavuno; Kuongeza elimu na uelewa wa wadau juu ya masuala na athari za sumu kuvu; na kuimarisha mamlaka na taasisi za usimamizi na udhibiti wa sumu kuvu kwenye mnyororo wa thamani. | 0 | 264,892,508.30 | • Mradi huu unatekelezwa katika mikoa ya Morogoro, Dodoma, Manyara, Tabora, Kigoma, Mwanza, Simiyu, Geita, Mtwara Ruvuma na Zanzibar. (i) Hadi kufikia Desemba, 2019, Wizara imesaini mkataba na Mtaalam Elekezi kwa ajili ya usanifu wa maghala 14 yenye uwezo wa kuhifadhi tani 1000 hadi 3000 (ii) Elimu kuhusu udhibiti wa sumukuvu imetolewa Wilayani kiteto. Aidha, mafunzo ya udhibiti wa sumu kuvu yametolewa kwa wakufunzi 72 kutoka katika vyuo 24 vya kilimo Tanzania |
| 507. | Mradi wa Kuendeleza Skimu za Umwagiliaji za Wakulima Wadogo (SSIDP) | • kujenga na kukarabati skimu za umwagiliaji 119 katika Halmashauri 68 nchini | 0 | 4,4785,179,330 | • Mradi wa Skimu za Umwagiliaji za Wakulima Wadogo (SSIDP) unaofadhiliwa na Serikali ya Japan kupitia Shirika lake la Maendeleo (JICA) unatekelezwa na Tume ya |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | Taifa ya Umwagiliaji na TAMISEMI kupitia Halmashauri 68 nchini. Utekelezaji wa mradi ulianza katika mwaka 2014/2015 ambapo ujenzi na ukarabati wa skimu za umwagiliaji 125 katika Halmashauri 68 nchini unaendelea. Kati ya skimu hizo, ukarabati na ujenzi wa skimu 120 sawa na asilimia 96 umekamilika. Aidha, Ununuzi wa mitambo 17 ya aina mbalimbali pamoja na magari 17 yamenunuliwa kupitia mradi. |
| **JUMLA NDOGO** | | | **77,892,483,961.10** | **124,640,007,726.03** | |
| **WIZARA YA MADINI** | | | | | |
| 508. | Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali Madini | Kuimarisha uwezo wa Serikali kusimamia Sekta ya Madini na kuboresha manufaa ya kijamii na kiuchumi yatokanayo na uchimbaji mkubwa na mdogo. | 3,193,577,279.5 | 44,288,332,104.41 | • Kukamilika kwa ujenzi wa vituo vinne (4) vya umahiri *(Centre of Excellency)* katika maeneo ya Bariadi, Musoma, Bukoba na Handeni; kuendelea na ujenzi wa vituo vitatu (3) vya Songea, Mpanda na Chunya;<br>• Kuanzishwa kwa masoko 28 na vituo vidogo 25 vya ununuzi wa madini;<br>• Kukamilika kwa ukarabati wa ofisi za madini Moshi na Nachingwea;<br>• Kukamilika kwa ujenzi wa ukuta katika ofisi za madini Moshi ambapo |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | kwa sasa kazi zinazoendelea ni upakaji wa rangi na ufungaji wa taa;<br>• Jengo la Taaluma la Chuo cha Madini (Dodoma) linajengwa katika Chuo cha Madini, eneo la Miuji Jijini Dodoma ambapo ujenzi umekamilika kwa asilimia 95;<br>• Kukamilika kwa ujenzi wa mgodi wa mfano na ufungaji wa mitambo ya uchenjuaji wa madini ya dhahabu kwa ajili ya mafunzo kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu Lwamgasa mkoani Geita;<br>• Kukamilika kwa ufungaji wa mitambo ya uchenjuaji wa madini ya dhahabu kwa ajili ya mafunzo kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu katika eneo la Katente mkoani Geita;<br>• Ufungaji wa mitambo ya uchenjuaji wa madini ya dhahabu kwa ajili ya mafunzo kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu katika eneo la Katente mkoani Geita ambapo mradi umekamilika kwa asilimia 85;<br>• Ufungaji wa mitambo ya uchenjuaji madini ya dhahabu kwa ajili ya |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | mafunzo kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu katika eneo la Itumbi mkoani Mbeya ambapo mradi umekamilika kwa asilimia 75;<br>• Kuwezesha ununuzi wa mashine ya uchorongaji *(Drill Rig)* iliyokabidhiwa STAMICO ili kutoa huduma za kitafiti kwa wachimbaji wadogo wa madini kwa gharama nafuu. Mashine hii kwa sasa imeanza kazi katika maeneo ya Buck-reef na Lwamgasa kwa wachimbaji wadogo kwa ajili ya kupata taarifa za kijiolojia;<br>• Kukamilika kwa uandaaji wa Mwongozo wa Mpango wa Utunzaji wa Mazingira kwa wachimbaji wadogo. Hatua inayofuata ni kuchapisha Mwongozo huo na kuusambaza kwa wahusika hususan wachimbaji wadogo;<br>• Kukamilika kwa uchapishaji wa vitabu vya Mwongozo wa Wachimbaji Madini Wadogo. Hatua inayofuata ni kusambaza kwenye Ofisi za Madini za Mikoa (RMOs) pamoja na ofisi mbalimbali za |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | Serikali;<br>• Kuandaa Mwongozo wa Mpango wa Ufungaji Migodi *(Mine Closure Guidelines)* kwa kushirikiana na Tume ya Madini.<br>• Kukamilika kwa ujenzi wa Kituo cha Pamoja - *One Stop Center* (Mirerani) katika eneo la Mirerani. Lengo la kituo hiki ni kuhakikisha kuwa shughuli zote zinazohusu biashara ya madini zinafanyika ndani ya eneo moja ili kudhibiti utoroshaji. Aidha, kituo hicho kitasaidia upatikanaji wa takwimu sahihi za madini.<br>• Kuwapatia mafunzo wachimbaji wadogo 638 kutoka katika vituo 6 vilivyofanyiwa utafiti wa kina wa jiosayansi. Lengo la mafunzo hayo lilikuwa ni kuelimisha wachimbaji wadogo kuhusu mbinu za utafutaji, uchimbaji salama, tabia za mbale mbalimbali, uchenjuaji wa madini na utunzaji wa mazingira. |
| 509. | Uwazi na Uwajibikaji katika Usimamizi wa Rasilimali Madini, | Kuhamasisha Serikali kuweka mifumo ya uwazi na uwajibikaji katika usimamizi | | 901,039,239.86 | • Kukamilika kwa taratibu za manunuzi kwa ajili ya kuandaa na kutoa kwa Umma taarifa ya TEITI |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | Mafuta na Gesi Asilia. | wa rasilimali za madini, mafuta na gesi asilia | | | ya mwaka 2016/17 na 2017/18. |
| 510. | Regional Mining Offices Development | Kukarabati na kujenga majengo ya ofisi za madini. | 100,000,000 | | Ukarabati wa jengo umekamilika. |
| 511. | Kuongeza mchango wa sekta ya madini kwa Taifa | Uboreshaji wa Mikataba ya uchimmbaji madini | | | • Kufanyika kwa marekebisho ya sheria na mikataba ya uwekezaji katika sekta ya madini na hivyo kuanzishwa kwa Kampuni mpya ya Twiga Minerals Corporation Limited inayomilikiwa kwa ubia kati ya Serikali (hisa asilimia 16) na Kampuni ya Barrick (hisa asilimia 84); na kufanyika kwa malipo ya fidia ya dola za Marekani milioni 100 kutoka Kampuni ya Barrick ikiwa ni sehemu ya kwanza ya kiasi cha makubaliano ya awali ya kulipa fidia ya dola za Marekani milioni 300. Aidha, marekebisho ya Sheria yamewezesha kuanza kwa majadiliano baina ya Serikali na Makampuni yote makubwa ya madini kwa lengo la kupata asilimia 16 ya hisa kwa Serikali; na<br>• Kuongezeka kwa maduhuli ya |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | Serikali kutoka shilingi bilioni 196 mwaka 2015/16 hadi zaidi ya shilingi bilioni 470 mwaka 2019/20. |
| **JUMLA NDOGO** | | | **6,397,154,559.00** | **89,477,703,448.68** | |
| | | **WIZARA YA MALIASILI NA UTALII** | | | |
| 512. | Mradi wa Kusimamia Maliasili na Kuendeleza Utalii Kanda ya Kusini ( REGROW) | Kufungua fursa za vivutio vilivyoko ukanda wa kusini mwa Tanzania kwa kutekeleza mradi wa kuendeleza baadhi ya maeneo muhimu yenye vivutio ili kuongeza mchango wa sekta ya utalii kwenye uchumi na maendeleo ya nchi. | 0 | 6,834,597,667 | • Maandalizi ya awali ya mradi yalifanyika ikiwa ni pamoja na kufanya tafiti mbalimbali katika maeneo ambayo mradi utatekelezwa, kuandaliwa na kuchapishwa kwa Andiko la Mradi (PAD) na Mwongozo wa Utekelezaji Mradi (PIM);<br>• Hadidu za rejea za kazi za ujenzi na Specifications za vifaa na mitambo inayohitajika kwa ajili ya utekelezaji wa mradi zimeandaliwa;<br>• Tenda tano zimetangazwa kwa ajili ya kupata wazabuni na wakandarasi;<br>• Hadidu za Rejea kwa ajili ya kupata wakandarasi na washauri wa ujenzi wa miundombinu itakayojengwa kwenye hifadhi;<br>• Kukamilika kwa ununuzi wa vifaa na samani kwa ajili ya ofisi za mradi;<br>• Kutolewa kwa ushauri elekezi |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | kuhusu mazao ya utalii katika jamii na utafiti kuhusu hali ya kijamii na kiuchumi katika jamii zinazozunguka maeneo yaliyohifadhiwa katika ukanda wa kusini;<br>• Kukamilika kwa zoezi la ufuatiliaji maeneo ya Mbarali na Pori la Akiba la Selous;<br>• Tathmini ya mtaalam atakaye fanya kazi ya kuandaa Mpango Mkakati wa Masoko ya Utalii katika maeneo ya kusini imekamilika;<br>• Rasimu za maandiko kwa ajili ya shughuli za ujenzi wa uwezo kwenye Skimu ya umwagiliaji ya Madibira katika Wilaya ya Mbarali umeandaliwa;<br>• Vifaa vya matangazo kwa ajili ya ushiriki katika maonesho ya Karibu Kusini vilinunuliwa na maonyesho yalifanyika;<br>• Mafunzo ya usimamizi wa fedha na manunuzi yalifanyika kwa maafisa kutoka taasisi zinazotekeleza mradi; na |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | • Vifaa kwa ajili ya kufanya doria katika Hifadhi ya Taifa Ruaha vimenunuliwa na kukabidhiwa kwenye hifadhi hiyo. |
| 513. | Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Ikolojia ya Ardhioevu ya Bonde la Mto Kilombero na Mto Rufiji (KILORWEMP) | Kusimamia Ikolojia ya ardhi oevu ya bonde la Kilombero na Mto Rufiji kwa kuwezesha uhifadhi shirikishi wa maliasili na kuimarisha uwezo wa Serikali Kuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Mradi unatekelezwa katika Mikoa ya Morogoro na Pwani hususan bonde la Kilombero la Mto Kilombero na Mto Rufiji ambapo wanufaika ni wananchi wa Wilaya za Kilombero, Malinyi, Ulanga na Rufiji. | - | 2,924,500,000 | • Kukamilika kwa ujenzi wa ofisi ya Maliasili katika Wilaya ya Ulanga;<br>• Kukamilika kwa ujenzi wa vituo viwili vya asikari wa wanyamapori katika wilaya ya Ulanga; kuanzishwa vikundi vine (4) vya uvuvi katika Mto Kilombero na kuviwezesha kutekeleza majukumu yake;<br>• Kurejesha maeneo yaliyoharibika kimazingira katika hali yake ya awali (habitat restoration);<br>• Kutoa elimu kwa jamii kuhusu usimamizi wa matumizi bora ya ardhi;<br>• Kufanya mapitio ya mipango ya usimamizi na uvunaji wa misitu katika wilaya ya Ulanga;<br>• Kujenga na kununua vifaa vya ofisi mbili (2) za Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori ya Ngorongoro, Utete na Rufiji (JUHIWANGUMWA) na Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori ya Ifakara, Lupiro na Mang'ula |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | (ILUMA) Kilombero; na<br>• Mradi ulifungwa tarehe 22 Septemba, 2018. |
| 514. | Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Maliasili. | Kuwezesha jamii kushiriki katika usimamizi endelevu wa maliasili. | - | 12,241,890,028 | • Kuwezesha maandalizi ya Mpango Mkakati na miongozo ya kuwezesha Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori – TAWA kujiendesha;<br>• Kuwezesha wananchi kuanzisha VICOBA katika Wilaya ya Serengeti;<br>• Kununua magari 2 kwa ajili ya Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA);<br>• Kununua gari 1 na pikipiki 6 kwa ajili ya kusaidia kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu katika Wilaya ya Serengeti;<br>• Kutoa mafunzo kwa wananchi wa Wilaya ya Serengeti kuhusu namna ya kujilinda na wanyamapori wakali na waharibifu;<br>• Kutoa mizinga ya nyuki (115) kwa wananchi wa Wilaya za Serengeti (80) na Ngorongoro (35) ili kuwezesha wananchi kiuchumi na kuendeleza uhifadhi;<br>• Kuhamasisha uhifadhi wa mazingira kwa wananchi kupitia michezo |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | ambapo Mradi umedhamini michezo katika wilaya husika kuanzia ngazi ya Kata hadi Wilaya;<br>• Kujengea uwezo Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji na Kata ambapo jumla ya Wajumbe 240 wa Mabaraza hayo wamepatiwa mafunzo;<br>• Mwongozo wa uwindaji wa Simba na Chui umeandaliwa kwa kuzingatia mahitaji ya Mkataba wa Kimataifa wa Biashara ya Viumbe vilivyo katika hatari ya kutoweka;<br>• Mpango wa Usimamizi wa Pori la Akiba la Kijereshi umeandaliwa na kubainisha maeneo ya uwekezaji na uendelezaji utalii. Aidha Mpango wa Usimamizi wa Pori la Akiba la Mkungunero upo katika hatua za ukamilishaji;<br>• Maboma kwa ajili ya kujilinda na wanyama wakali wakati wa usiku yamejengwa katika vijiji 10 katika Wialaya ya Serengeti;<br>• Mipango shirikishi ya usimamizi wa misitu na sheria ndogo zimeandaliwa katika vijiji 6 katika Wilaya ya Serengeti. Kwa Wilaya ya Ngorongoro, Mpango Shirikishi wa usimamizi wa Misitu umeandaliwa kwa ajili ya Msitu wa Jamii |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | Enguserosambu; na<br>• Mafunzo kwa Maafisa Mazingira na Uhifadhi katika ngazi ya Kata na Vijiji yamefanyika katika wilaya ya Ngorongoro. |
| 515. | Mradi wa Kujenga Uwezo katika Hifadhi za Taifa. | Mradi huu unatekelezawa kwa lengo la kuboresha miundombinu (barabara, viwanja vya ndege, nyumba za watumishi, madaraja, ofisi na miundo mbinu ya utalii) ndani ya Hifadhi. | 84,042,912,145 | 0 | • Kukamilika kwa ukarabati wa viwanja 18 vya ndege (Air strips) ndani ya Hifadhi;<br>• Kukamilika kwa ujenzi wa mageti, ofisi na nyumba za watumishi 38;<br>• Kukamilika kwa ujenzi wa barabara kwenye maeneo ya Hifadhi zenye urefu wa kilometa 185.9 na ukarabati wa kilometa 2,091.85 za barabara; na<br>• Malipo ya awali kwa ajili ya Ujenzi wa Hotel ya Kitalii hifadhi mpya ya Burigi Chato. |
| 516. | Mradi wa Kujenga Uwezo katika Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro. | Mradi huu unatekelezwa kwa lengo la kuboresha miundombinu ndani ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro. Wanufaika wa mradi ni Mamlaka, watalii na Taifa kwa ujumla kupitia kuongezeka kwa mapato yatokanayo na shughuli za utalii. | 48,256,860,139 | 0 | • Kukamilika kwa ukarabati wa uwanja wa ndege Ndutu kwa kuongeza tabaka la juu;<br>• Kukamilika kwa Jengo la Kitega Uchumi la 'NTC' na jengo limeshaanza kutumika;<br>• Matengenezo ya mara kwa mara kwenye barabara kuu ya Loduare hadi Golini yenye urefu wa KM 88;<br>• Kukamilika kwa Geti la |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | Endamaghay;<br>• Kukamilika kwa Jengo la Wafanyakazi katika eneo la Lemala;<br>• Kukamilika kwa ukarabati wa barabara ya Crator;<br>• Kukamilika kwa ujenzi wa mashimo ya maji taka kwenye maeneo Ngoitoktok na Simba A;<br>• Kukamilika kwa ukarabati wa nyumba 3 za wafanyakazi katika eneo la Kamyn Estate;<br>• Kukamilika kwa ujenzi wa Bomba la maji lenye urefu wa KM 5 kutoka Makao Makuu ya Mamlaka hadi Oloilobi;<br>• Kukamilika kwa majengo mawili ya Armory katika vituo vya Mbulumbulu na Enduleni;<br>• Kukamilika kwa jengo la kusubiria wageni katika eneo la uwanja wa Ndege Ndutu;<br>• Kukamilika kwa jengo la kusubiria wageni katika eneo la uwanja wa Ndege wa Ngorongoro;<br>• Kukamilika kwa mradi wa ufungaji |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | wa kamera za CCTV eneo la Makao makuu na mageti ya Naabi na Loduare;<br>• Kukamilika kwa mradi wa bwawa la kunyweshea mifugo katika eneo la Seneto – Ndepes;<br>• Ukarabati wa bwawa la kunyweshea mifugo katika kijiji cha Nasipooron;<br>• Kukamilika kwa ujenzi wa bohari ya kuhifadhia matairi ya magari;<br>• Kukamilika kwa ujenzi wa choo katika Kambi ya Mturi;<br>• Kukamilika kwa ujenzi wa nyumba ya wafanyakazi Laitoli;<br>• Kukamilika kwa ujenzi wa geti katika eneo la Nasera Rock; na<br>• Kukakilika kwa matengenezo ya barabara ya Lositete yenye urefu wa kilomita 6 kwa kiwango cha changarawe. |
| 517. | Mradi wa Panda Miti Kibiashara. | Kuongeza uchumi wa wananchi wa Nyanda za Juu Kusini ili kupunguza umaskini, kuleta usawa katika jinsia, kuongeza thamani ya mazao ya misitu kwa kutumia mbegu bora | 0 | 90,522,600,000 | • Kufanya tafiti kuhusu ushiriki wa sekta binafsi katika upandaji miti;<br>• Kuwezesha Jumuiya za Upandaji Miti (Tree Growers Assosiations) ambapo jumla ya miche ya miti |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | ikiwa ni pamoja na kuongeza ajira. | | | 5,015, 626 ilipandwa. Aidha, eneo jipya la hekta 3,932 lilihakikiwa na kupandwa miti Katika mwaka uliopita wa fedha;<br>• Kuwezesha Jumuiya za Wapandaji Miti, Wafanyabiashara wa mazao ya miti na watumishi kufanya ziara za mafunzo;<br>• Kuziwezesha jamii za wapandaji miti kuanzisha miradi ya kiuchumi kwa ajili ya kujiongezea kipato;<br>• Kujenga uwezo wa Wapandaji miti kupitia kituo cha Midsitu na Viwanda vya Misitu kilichopo Mafinga. Kituo hiki kilianzishwa chini ya mpango huu;<br>• Kukamilisha maandalizi ya mitaala ya ufundi stadi katika misitu na viwanda vya misitu – ngazi ya kwanza, ya pili na, tatu;<br>• Kuwezesha Ofisi ya Mradi kutekeleza majukumu yake kila siku;<br>• Kukamilika kwa tafiti tano kwa ajili ya kusaidia upandaji miti kibiashara;<br>• Shughuli za mradi zimeratibiwa na kusimamiwa kwa ushirikiano na |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | Wizara ya Maliasili na Utalii;<br>• Jumuiya ya Wapandamiti wamewezeshwa miche ya miti 5,500 aina ya Misindano;<br>• Kukamilika kwa Mradi mpya wa Kuongeza thamani mazao ya Misitu (Forestry and Value Chain – FORVAC);<br>• Wakulima wadogo wadogo wa miti wamepatiwa msaada wa miche bora ya miti na kuweza kupanda zaidi ya hekta 10,000 ambapo lengo kuu mpaka mwisho wa awamu hii ya kwanza ni kufikia hekta 15,000. Zaidi ya kaya 3000 katika vijiji 40 zimenufaika na mpango huo;<br>• Mpaka sasa Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi katika vijiji 48 imefanyika kupitia programu hii;<br>• Kutambulika na kuanzisha kwa vikundi vya wapanda miti 116 mpaka sasa ambao ni wanufaika wa programu;<br>• Kituo cha mafunzo cha mambo ya misitu na teknologia za misitu kimeweza kuanzisha katika mji wa |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | Mafinga walengwa wakuu wakiwa ni wakulima wa miti na wafanya biashara wa mazao ya misitu;<br>• Kuanzishwa kwa mfumo wa taarifa za masoko (SMS based) ambao unamuunganisha mkulima wa miti na mnunuzi, pamoja na wauzaji wa pembejeo za misitu;<br>• Kuanzishwa kwa zaidi ya hekta 190 za mashamba ya mbegu katika maeneo mbalimbali ya mradi; na<br>• Taarifa za wakulima wa miti zaidi ya 8000 na mashamba yao zimeweza kukusanywa ili kuweza kuwaunganisha na masoko na pia kuweza kuwasaidia kwa kutoa mafunzo na ushauri mbalimbali kuhusiana na namna ya kutunza mashamba yao ya miti hii ili kuweza kujua ni kiasi gani cha rasilimali misitu katika maeneo husika ili taarifa hizi ziweze kuwakifika wadau mbalimbali wa misitu ikiwa ni pamoja na wawekezaji wakubwa wa viwanda vya misitu. |
| 518. | Mradi wa Kuwezesha | Kuwezesha Jamii za Wilaya | 0 | 3,318,799,500 | • Masuala ya uhifadhi na uzalishaji |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | Wananchi Kunufaika na Rasilimali za Misitu kwa Maendeleo ya Kiuchumi (NRM - LED). | za Uvinza, Kigoma, Kasulu,Kibondo, Kakonko, na Buhingwe kunufaika na rasilimali za misitu | | | mali imeingizwa kwenye mipango ya Vijiji 20 na Halmashauri za Wilaya 6 za Uvinza, Kigoma, Kasulu, Buhigwe, Kibondo na Kakonko;<br>• Jumla ya Hakimiliki 893 zimekabidhiwa walengwa; haki 2503 zipo katika hatua za mwisho;<br>• Mipango ya Vijiji ya Matumizi Bora ya Ardhi katika vijiji 24 kwenye Halmashauri za Wilaya tano za Uvinza, Kakonko, Buhigwe, Kasulu na Kibondo;<br>• Hifadhi za Misitu ya Vijiji katika vjijiji 28 vyenye misitu 39 na ukubwa wa misitu yote ni jumla ya hekta 39,449;<br>• Kumeanzishwa Kamati za Fukwe (Beach Management Units – BMU) 3 za Mtanga, Kigalye na Kalalangabo na vikundi vya wavuvi 5 Katika vijiji vya Kasisi, Mtegowa noti, Malagarasi, Itebula na Chagu;<br>• Jumla ya mitumbwi 23 imetengenezwa na kukabidhiwa kwa vikundi vya wavuvi;<br>• Mashindano ya biashara yalifanyika na vikundi 18 vilipewa tuzo;<br>• Vikundi 18 vya ujasiriamali |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | vilipewa fedha kwa ajili ya kuendesha shughuli mbalimbali zinazohusiana na uhifadhi wa rasilimali;<br>• Mafunzo mbalimbali yalitolewa kwa vikundi vya uvuvi, nyuki, watengeneza samani,wataalam wa Halmashauri, uperembaji wa shughuli za hifadhi ya rasilimali;<br>• Kamati za vijiji ziliwezeshwa kwa vifaa mbalimbali kwa ajili ya ulinzi na usimamizi wa rasilimali katika misitu yao ya hifadhi;<br>• Timu za Mradi za Wilaya na Vijiji na Kamati za Mikoa zimepatiwa Mafunzo kwa ajili ya utekelezaji wa Mipango ya Usimamizi wa Maliasili na Usimamizi wa Sheria ndogo. Aidha Mipango ya Usimamizi wa Misitu ya Vijiji nane (8) imeandaliwa pamoja Mipango minane (8 ya Uvunaji wa Misitu;<br>• Hati za kienyeji za umiliki wa ardhi 3500 zimetolewa. Aidha Mradi umewezesha kusajiliwa kwa ramani za vijiji 5 kwenye Tume ya Taifa ya Matumizi ya Ardhi;<br>• Taarifa ya mwisho ya Tathmini ya Mradi imekamilishwa na kuwasilishwa katika Mkutano |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | uliohusisha Wajumbe kutoka Kamati Endeshaji ya Mradi, Mkoa na Wilaya;<br>• Washindi 18 wa Mashindano ya Uandishi wa Mipango ya Biashara walipewa tuzo zao;<br>• Mipango ya Usimamizi wa Misitu ya Vijiji 34 yenye ukubwa wa eneo la hekta 39,447 imewasilishwa Wizara ya Maliasili na Utalii kwa ajili ya usajili; na<br>• Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi 29 imepitishwa katika ngazi ya Wilaya na imewasilishwa Tume ya Taifa ya Matumizi Bora ya Ardhi kwa ajili ya usajili. |
| 519. | Mradi wa Kuwezesha Jamii kupitia Mafunzo ya Ushiriki katika Uhifadhi wa Misitu na Programu ya Mabadiliko ya Tabianchi. | Kuziwezesha Halmashauri za Wilaya na taasisi zisizo za kiserikali kusimamia utekelezaji wa mabadiliko ya tabia nchi. | 0 | 6,488,946,506 | • Kuendelea kuwajengea uwezo wa watumishi wa Halmashauri za wilaya na taasisi zisizo za kiserikali katika kutoa huduma za mipango na shughuli za USM, MKUHUMI na Mabadiliko ya Tabianchi na kuwajibika kwa wateja;<br>• Kutenga misitu ya vijiji 14 pamoja na kuandaa mipango ya usimamizi kwenye Halmashauri za Wilaya za Same, Kibondo, Kilindi na Manyoni;<br>• Kuwezesha wadau wa kanda ya Mashariki kuhudhuria warsha ya |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | kurejelea sera ya Taifa ya Misitu;<br>• Kutoa mafunzo juu ya wanavijiji kufanya tathmini ya rasilimali ya misitu.;<br>• Kukamilisha ujenzi wa majengo mawili (Jengo la Mikutano na Bweni la Wasichana) katika Chuo cha Misitu Olmotoni. na;<br>• Kukamilisha ukarabati wa nyumba tano (5) za walimu katika chuo cha Misitu Olmotonyi. |
| 520. | Programu ya Misitu na Uendelezaji wa Mnyororo wa Thamani wa Mazao ya Misitu (FORVAC). | Kuiwezesha jamii kushiriki katika uzalishaji na biashara ya mazao ya misitu katika wilaya za Mufindi, Kilolo, Njombe, Makete, Ludewa na Kilombero. | 0 | 14,656,367,881 | • Tafiti nane kuhusu misitu binafsi zimefanyika;<br>• Uratibu na mawasiliano ya usimamizi wa miradi umefanyika;<br>• Vyama 37 vya wapandaji miti vimewezeshwa kupanda miti;<br>• Kuwezeshwa kwa ubadilishanaji uzoefu katik ya vijiji na wadau kwa kufanya mafunzo;<br>• Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi 25 iliandaliwa;<br>• Kuwezesha Wizara ya Maliasili na Utalii kuandaa mwongozo wa kuandaa Mipango ya Usimamizi wa Hifadhi za Misitu Asilia;<br>• Miche 230,000 ya Miti aina ya Mitiki ilinunuliwa kutoka TFS na kusambazwa katika vijiji 3 kwa ajili |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | ya kupandwa;<br>• Kikosi Kazi cha uendelezaji wa Mkaa kilichambua fursa za Mkaa na kuandaa Mkakati kwa ajili ya uendelezaji wa zao la Mkaa;<br>• Nakala 3500 za Kitabu cha Usimamizi wa Misitu ya Jamii zilichapishwa;<br>• Waandishi wa habari 27 walipatiwa mafunzo kuhusu mnyororo wa thamani wa mazao ya misitu na uandishi wa habari za kiuchunguzi.<br>• Mfumo wa utoaji na upashanaji wa taarifa ulisimkwa; na<br>• Jumla ya wawakilishi 30 wa vikundi vya wafugaji nyuki na wanakijiji 45 katika vijiji vya mradi katika wilaya za Kilindi, Handeni, na Nyasa waliwezeshwa kushiriki maonesho ya Nanenane. |
| 521. | Mradi wa Hifadhi za Misitu za Mazingira Asilia. | Kuziwezesha Wizara, Idara, Halmashauri za Wilaya na Asasi zisizokuwa za Serikali kuboresha usimamizi wa sheria za mazingira ili kulinda mifumo ikolojia, na bioanuwai kwa ajili ya ustawi na usimamizi wa rasilimali za misitu. | 0 | 4,324,395,181 | • Kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali Misitu Mitano ya Hifadhi ya Mazingira Asilia ya Chome, Magamba, Mkingu, Minziro na Udzungwa Scarp;<br>• Kusimamia ukarabati wa Nyumba za Watumishi katika hifadhi za Chome, Mlima Rungwe, Mkingu na Minziro ambapo kazi zimeshatekelezwa kwa 90% kazi |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | inaendelea kwa hifadhi za Magamba and Uzungwa Scarp;<br>• Kikao kimoja cha Kamati Endeshi kiliwezeshwa kukaa kujadili mpango kazi na bajeti kwa mwaka 2016/17, 2017/18, 2018/2019 na 2019/2020.;<br>• Jumla ya kilometa 85.53 za barabara za msituni zimetengenezwa ili kuwezesha upitikaji katika Hifadhi zote za Misitu ya Asili;<br>• Jumla ya kilometa 37.3 za njia za msituni katika hifadhi za misitu asilia ya Udzungwa, Kilombero, Mlima Hanang na Minziro zimetengenezwa ili kuboresha upitikaji;<br>• Mapitio ya tovuti ya Hifadhi ya Misitu ya Asilia umefanyika na kutambua mapungufu ambayo yanafanyiwa kazi; na<br>• Jamii zinazopakana na Hifadhi za Misitu Asilia ziliwezeshwa kuanzisha manzuki, vitalu vya miche, ufugaji samaki na kusindikiza watalii katika hifadhi za misitu asilia ya Chome, Mkingu, Minziro, Kilombero, Mlima Rungwe, Mlima, Mlima Hanang na |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | Magamba. |
| **JUMLA NDOGO** | | | **132,299,772,284.34** | **137,420,223,088.35** | |
| **WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI (MIFUGO)** | | | | | |
| 522. | Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Nchini II (ASDP II) | Kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa miradi ya ASDP II | 280,000,000 | | Ufuatiliaji ulifanyika katika mazeneo ya miradi. Maeneo yaliyotembelewa ni pamoja na mashamba ya kuzalisha mbegu bora za malisho ya Langwira (Mbeya) na shamba la mifugo Ngerengere; TALIRI Uyole na Wakala wa Mafuno ya Mifugo (LITA) Kampusi za Buhuri na Mpwapwa. |
| 523. | | Kujenga madarasa matatu katika Kampasi za LITA Madaba na Kikulula | | | Ukarabati wa jengo la kompyuta (Computer lab), ukarabati wa ofisi za watumishi na nyumba mbili za watumishi umeendelea katika Kampasi za Madaba, Morogoro na Kituo cha Kikulula sawia. |
| 524. | | Kuiwezesha Wakala Elimu na Mafunzo (FETA) kutekeleza majukumu yake. | | | Madarasa ya Chuo cha Elimu na Mafunzo ya Uvuvi Kampasi ya Mtwara – Mikindani yamejengwa. |
| 525. | | Kuimarisha kituo cha Taifa cha Uhimilishaji cha NAIC na Sao Hill. | | | Kifaa (Chiller) kwa ajili ya mtambo wa kuzalisha kimiminika cha Nitrogeni cha NAIC USA River Arusha kimenunuliwa na uzalishaji wa mbegu za uhimilishaji unaendelea. |
| 526. | | Ujenzi wa minada miwili (2) | | | Minada ya Upili ya Pugu (Dar es |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | ya Mpakani, (Longido na Kirumi) na kukarabati Minada ya Upili (Nyamatala na Kasesya) ili kuongeza ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali. | | | Salaam), Kizota (Dodoma) na Nyamatara (Mwanza) imekarabatiwa. |
| 527. | | Kudhibiti kupe na magonjwa wayaenezayo kwa kuogesha mifugo na kutoa chanjo dhidi ya Ndigana Kali. | 1,980,020,000 | | Jumla ya lita **8,823.53** za dawa za kuogesha mifugo aina ya Paranex zimenunuliwa na zimesambazwa katika mikoa 26 nchini. Aidha, zoezi la uhamasishaji uogeshaji wa mifugo limefanyika katika mikoa 26 nchini. Jumla ya michovyo ya mifugo **40,352,228** imeogeshwa, kati ya michovyo ya mifugo hiyo, ng'ombe ni **22,400,170,** mbuzi **12,836,389,** na kondoo ni **5,115,669** katika majosho **1,486** kati ya majosho **2,533** yaliyopo nchini. Ukarabati wa majosho **1,129** unaendelea. |
| 528. | | Kudhibiti kupe na magonjwa wayaenezayo kwa kuogesha mifugo na kutoa chanjo dhidi ya Ndigana Kali. | | | Ujenzi wa jengo la kuzalisha chanjo za mifugo na ukuta kuzunguka jengo la uzalishaji umefikia **asilimia 45.** Kazi zilizokamilika ni ujenzi wa boma la jengo la kuzalisha chanjo na ukuta kuzunguka jengo. |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| 529. | | Kuwezesha Wakala wa Maabara ya Veterinari Tanzania (Tanzania Veterinary Laboratory Agency-TVLA) kuzalisha chanjo. | | | Ujenzi wa jengo la kuzalisha chanjo za mifugo na ukuta kuzunguka jengo la uzalishaji umefikia **asilimia 45.** Kazi zilizokamilika ni ujenzi wa boma la jengo la kuzalisha chanjo na ukuta kuzunguka jengo. |
| 530. | | Ujenzi wa minada miwili (2) ya mpakani (Longido na Kirumi) na kukarabati minada ya upili (Nyamatala na Kasesya). | | | • Ukarabati wa mazizi katika mnada wa Kirumi umefanyika na ujenzi wa ofisi katika mnada wa Kirumi na ujenzi wa sakafu katika mnada wa Longido unaendelea. Pia, ujenzi wa uzio katika mnada wa Kasesya, Buhigwe na Nyamatala inaendelea.<br>• Tathmini ya ukarabati wa minada ya Nyamatala na Kasesya inaendelea.<br>• Kazi ya minada ya Longido, Nyamatala na Kasesya imetengewa shilingi 600,000,000 na shilingi 112,500,000 zimelipwa kwa ajili ya mnada wa Longido ikiwa ni **asilimia 75** ya kazi ambazo zimefanyika. |
| **JUMLA NDOGO** | | | **2,260,020,000.00** | **-** | |
| | | **WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI (UVUVI)** | | | |
| 531. | SWIOFish | • Kuimarisha sera, sheria na kanuni za uvuvi kwa ajili ya usimamizi wa rasilimali za | | 4,486,540,291.53 | • Wizara imefanya mapitio ya Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya Mwaka 2003 na Kanuni zake za mwaka 2009. Hadi |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | uvuvi;<br>• Kufanya tafiti mbalimbali za aina za samaki;<br>• Kujenga uwezo wa watumishi kwa kuwapatia mafunzo;<br>• Kuimarisha mfumo wa taarifa zinazohusu uvuvi kulingana na matakwa ya kikanda;<br>• Kuimarisha ulinzi wa Rasilimali za Uvuvi kwa ajili ya ushirikishwaji wa jamii za uvuvi;<br>• Kuimarisha doria katika ulinzi wa rasilimali za uvuvi katika mavuvi ya kipaumbele;<br>• Kazi mbalimbali za ushauri;<br>• Kuwezesha kitengo cha Marine Parks and Reserve Unit;<br>• FETA; TAFIRI na Idara za Uvuvi.<br>• Kuwezesha ujenzi wa | | | sasa maoni kutoka kwa wadau ya kuhusu Sheria hizo yamekusanywa na kuchambuliwa. Kutokana na Mapitio hayo Wizara imewasilisha barua Ofisi ya Mwanasheria wa Serikali kuomba Mwongozo wa kufanya marekebisho ya sheria iliyopo au kutunga sheria mpya.<br>• Vile vile, Wizara imeendelea kufanya mapitio ya Sheria ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu Na. 29 ya Mwaka 1994 na Sheria ya Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi Bahari Kuu Na. 1 ya Mwaka 1998 na marekebisho yake ya Mwaka 2007.<br>• Pia, Wizara imefanya marekebisho ya Kanuni nne (4) za Uvuvi ambazo ni (i) kuruhusu matumizi ya nyavu za milimita nane (8) badala ya kumi (10) kwa uvuvi wa dagaa katika ukanda wa bahari; (ii) matumizi ya nyavu za makila zenye ukubwa wa macho ya kuanzia inchi saba (7) badala ya inchi sita (6) kwa uvuvi wa sangara na (iii) kuondoa ukomo wa urefu wa sentimita 85 kwa samaki aina ya |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | nyumba, Maabara na Jengo la Utawala | | | Sangara, (iv) matumizi ya leseni moja kwa kila eneo la maji ya uvuvi badala ya kila Halmashauri kutoa leseni yake ili kuongeza tija katika uvuvi na biashara ya mazao ya uvuvi. Mapitio haya yamefanyika ili kuliwezesha Taifa kunufaika na rasilimali za uvuvi.<br>• Tafiti mbalimbali za samaki aina ya Pweza, Jodari na jamii zake, samaki wanaoelea, samaki wanaopatikana katika matumbawe na kambamiti zinaendelea kufanyika katika maeneo ya Bahari ya Hindi; Mafia, Tanga na Mtwara.<br>• Watumishi 24 kutoka Serikali Kuu, Halmashauri na Taasisi zilizo chini ya Wizara wamejiunga na masomo ya Shahada za Uzamili (18) na Shahada za Uzamivu (6) katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (22), Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (1) na Chuo cha Mipango Dodoma (1); Pia, Kuwezesha watumishi wane (4) kufanya mitihani ya NBAA na mafunzo ya muda mfupi ESAMI kuhusu manunuzi na ugavi. |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | • Kufanyika kwa sensa ya uvuvi mwaka 2018 ambapo taarifa yake inaendelea kuandaliwa. Aidha, Kanzidata ya Mazao ya Uvuvi imefanyiwa marekebisho ili kuendana na mahitaji. Vile vile, ufuatiliaji na uboreshaji wa ukusanyaji takwimu za uvuvi umefanyika katika wilaya ya Kibiti<br>• Kuainisha maeneo ya mavuvi ili kutayarisha fish patterns katika wilaya za Lindi, Bagamoyo, Mkinga, Pangani na Tanga ili kubaini na kuanzisha maeneo ya mavuvi ya pamoja.<br>• Kununuliwa na kuwekwa kwa GIS software mbili (2) katika Komputa za Kitengo cha kuendeleza rasilimali za uvuvi. Aidha, maafisa uvuvi (32) na wanachama 106 wa BMUs wamepatiwa mafunzo ya ukusanyaji takwimu za uvuvi katika BMUs 49 na halmashauri 16 za ukanda wa pwani ya bahari ya Hindi;<br>• Mwongozo wa Kitaifa wa Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi ulitayarishwa na kuidhinishwa. Kwa kutumia mwongozo huo, BMU 49 |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | ziliimarishwa katika wilaya (5) za Tanga, Mkinga, Pangani, Bagamoyo na Lindi. Vilevile vikundi 50 vya BMUs vilipatiwa mafunzo ya uongozi na utawala bora, wajibu na majukumu yao, kuandaa Mpango wa Usimamizi wa Uvuvi katika maeneo yao;<br>• Vifaa vya kufanyia usafi kwa ajili ya BMUs na kazi za ufuatiliaji wa kazi za mradi katika wilaya za Lindi, Bagamoyo, Pangani, Mkinga na Tanga vilinunuliwa.<br>• Vifaa kwa ajili ya kulinda maeneo ya bahari kwa kutumia vessel monitoring system vimenunuliwa na watumishi 4 wamepatiwa mafunzo kutoka kwa mtaalam aliyefunga mitambo hiyo DSFA. Jumla ya doria za baharini na nchi kavu 106 zimefanyika na kukamata watuhumiwa (260) na vifaa haramu vya kutengeneza milipuko kama mbolea kilo 1775, vipande 3221 vya milipuko, tambi 3258, milipuko 1831, regulators 20, injini 86 za boti, mitungi 345 ya gesi, Kompresa 18, kilo 5,895 za samaki waliovuliwa kwa |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | mabomu na Kesi 73 za watuhumiwa wa uvuvi haramu zimefunguliwa. Vilevile, Semina kuhusu madhara ya uvuvi haramu ilifanyika kwa mahakimu, waendesha mashtaka, madiwani na viongozi wa dini katika halmashauri 16 za mwambao wa pwani ambapo watu 138 walipatiwa mafunzo;<br>• Kazi mbalimbali za ushauri zilifanyika kama ifuatavyo kwa uchache ni:<br>*i. Consultancy Services for External Institutional Support for Fisheries Research Activities;*<br>*ii. Consultancy Services Technical Advise on Fisheries Information System;*<br>*iii. Consultancy Services to Review and Improve The Current Design of Fisheries Catch Database;*<br>*iv. Consultancy Services to Provide Technical Advise on Coral Reef Benthic Monitoring in Marine Parks;*<br>*v. Consultancy Services to Develop Business Plan for Marine Parks and Reserve Unit;*<br>*vi. Consultancy Services to Train and* |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | *Provide Technical Backstopping Services an Fisheries Co-Management;*<br>vii. *Consultancy Services for Designing of TAFIRI DSM Centre Wet Lab Building and TACMP Staff Housing Compound;*<br>viii. *Consultancy Services to Conduct Training Needs Assessment for Pius and Local Government Officials in Management Of Safegurds, Environmental And Social Issues;*<br>ix. *Consultancy Services To Develop Communication, Education and Awareness Raising Strategy to Match Planned Activities;*<br>x. *Consultancy Services to Develop Business Plan for Kilindoni, Nyamisati and Masoko Pwani Landing Sites;*<br>xi. *Consultancy Services to Develop and Customize MIS Software for Project Management and Provide Training;*<br>xii. *Consultancy Services to Conduct Baseline Survey of Community Household; and*<br>xiii. *Consultancy Services to Conduct Project Monitoring and Evaluation* |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | • Mradi umewezesha kitengo cha Marine Park kufanya kazi za tathmini ya Matumbawe, tathmini ya mazao ya uvuvi, na kununua vifaa vya doria katika Hifadhi ya Bahari ya Siliokanti – Tanga;<br>• Mradi umewezesha FETA kutayarisha mitaala ya elimu na kununua vifaa mbalimbali.<br>• Mradi umenunua magari 12 ambayo yamegawiwa katika idara za maendeleo ya uvuvi, ufugaji viumbe maji, TAFIRI na MPRU. Vilevile, pikipiki 17 zimenunuliwa kwa ajili ya kusaidia ukusanyaji wa takwimu na ushirikishwaji wa jamii katika Halmashauri 5 (BMUs), vituo vya MCS/QC Kilwa na Mafia , TAFIRI na FETA pamoja na boti za doria.<br>• Ujenzi wa nyumba za watumishi katika Hifadhi ya Bahari ya Silikanti Tanga na Maabara ya TAFIRI Dar es Salaam unaendelea. Aidha, michoro na BOQs kwa ajili ya jengo la Utawala la Hifadhi ya Bahari ya Kisiwa cha Mafi imekamilika. |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| 532. | Ujenzi wa bandari ya uvuvi | • Kuwezesha meli zinazovua katika Bahari Kuu kutia nanga na kuhaulisha samaki, kuuza samaki, kutoa takwimu sahihi na huduma nyingine | 1,421,041,703.08 | | • Mradi upo kwenye hatua ya upembuzi yakinifu. Kufikia mwezi Septemba 2019, Mtaalam mwelekezi wa Kampuni ya Sering Ingegneria ya Italia alikuwa amekamilisha na kuwasilisha taarifa ya awali (Inception Report) na rasimu ya taarifa ya kina (Interim report). Malipo ya asilimia 20, sawa na Shilingi 284,208,340.62 ya gharama za mradi yalilipwa kwa Mkandarasi baada ya kukamilika hatua ya awali *(Inception report).* Matayarisho ya malipo ya asilimia 30 sawa na Shilingi 426,312,510.92 ya gharama za mradi yanaendelea baada ya mkandarasi kuwasilisha rasimu ya taarifa ya kina *(Draft Interm Report),* Septemba 2019. |
| **JUMLA NDOGO** | | | **1,421,041,703.08** | **4,486,540,291.53** | |
| **WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** | | | | | |
| 533. | *Defence Scheme* | • Kuboresha huduma ya makazi kwa Wanajeshi kwa kukarabati miundo mbinu;<br>• Kuendelea na ujenzi wa nyumba za makazi 10,000 | 5,567,475,218.00 | | • Kujengwa na kukamilisha miundombinu kwa nyumba 6,064.<br>• Kuendeleza ujenzi wa miundombinu ya maji safi na maji taka, Ngerengere.<br>• Kujengwa kwa Ofisi za Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa katika Mji wa Serikali eneo la |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | Mtumba, Dodoma. |
| | | • Kuendeleza programu za utafiti na kukuza uzalishaji katika viwanda vya kijeshi | 10,000,000,000.00 | | • Kufanyika kwa tafiti na uhawilishaji wa teknolojia za magari (NYUMBU na Zimamoto).<br>• Kufanyika kwa ununuzi wa malighafi kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa mazao ya kijeshi |
| | | • Kuliongezea Jeshi uwezo kiutendaji kwa kulinunulia zana na vifaa vya kisasa | 488,216,086,294.00 | | • Kufanyika kwa malipo ya kimkataba kufuatia ununuzi wa zana na vifaa kwa matumizi ya Jeshi, ugharamiaji mafunzo kwa Wanajeshi na ujenzi wa mahanga. |
| | | • Kuimarisha na kusambaza Mtandao wa Mawasiliano salama kwenye vikosi; kuweka umeme na kusimika minara ya Mtandao wa Mawasiliano Salama Jeshini | 150,000,000.00 | | • Kuingiza umeme katika minara ya mawasiliano na kufanyika tathmini ya kuunganisha umeme katika minara hiyo kwa kushirikiana na Wakala wa Kusambaza Umeme Vijijini (REA).<br>• Utekelezaji wa mradi umefika katika Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Tanga, Morogoro, Dodoma na Zanzibar. |
| | | • Kulipatia Jeshi ardhi ya kutekeleza shughuli zake kwa kupima na kumiliki ardhi kisheria | 11,343,742,819.66 | | • Kulipwa fidia katika maeneo ya Ras Mishindo (Kilwa), Ilemela(Mwanza), Mlangarini na Moshono – Arusha, Makoko Mara, Kihangaiko Bagamoyo na Kakonko Kigoma ambayo yatatumika na Jeshi |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | • Kuboresha huduma ya makazi kwa Wanajeshi kwa kukarabati miundo mbinu;<br>• Kuendelea na ujenzi wa nyumba za makazi 10,000 | 5,567,475,218.00 | | • Kujengwa na kukamilisha miundombinu kwa nyumba 6,064.<br>• Kuendeleza ujenzi wa miundombinu ya maji safi na maji taka, Ngerengere.<br>• Kujengwa kwa Ofisi za Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa katika Mji wa Serikali eneo la Mtumba, Dodoma. |
| 534. | Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu | • Kujenga na kukarabati majengo, miundombinu na mifumo ya ulinzi, makazi na ofisi | 24,534,091,935.23 | 301,438,631,000.00 | • Kuboresha mfumo wa ulinzi wa anga<br>• Kukamilisha ujenzi wa mahanga ya Askari<br>• Kuweka mfumo wa ulinzi wa Kamera za CCTV kwenye maghala ya milipuko na risasi<br>• Ununuzi wa "server" ya mfumo wa malipo na usimikaji wake.<br>• Ujenzi na ukarabati wa makambi, maghala na miundombinu<br>• Ukarabati na upanuzi wa uwanja wa ndege vita Ngerengere<br>• Ujenzi wa Chuo cha Mafunzo Maalum ya Kijeshi (Comprehensive Training Centre – CTC) Mapinga Bagamoyo<br>• Ujenzi Awamu ya Pili National Defence College (NDC)<br>• Ujenzi Makao Makuu ya Ulinzi ya muda Msalato na miundombinu Makao Makuu ya kudumu Kikombo, |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | Dodoma<br>• Ununuzi wa eneo la kimkakati Kakonko, Kigoma.<br>• Ujenzi wa Karakana ya magari ya Kisasa 521 KJ<br>• Ujenzi wa hospitali mpya ya Kijeshi, Arusha |
| **JUMLA NDOGO** | | | 547,811,396,266.89 | 301,438,631,000.00 | |
| **OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA (MENEJIMENT YA UTUMISHI WA UMMA)** | | | | | |
| 535. | *Public Service reform Programme* | • Ujenzi wa nyumba za Viongozi Wastaafu wa Kitaifa (Mh. Ally Hassani Mwinyi na Mh. Jakaya M. Kikwete) | 5,994,709,224.00 | | • Ujenziwa nyumba za Viongozi wa Kitaifa Wastaafu ambao ni Mhe Ali H. Mwinyi na Mhe Jakaya M. Kikwete ni miradi inayoendelea. Nyumba ya Mwinyi ipo katika hatua za umaliziaji na nyumba ya Kikwete, ujenzi wake upo katika umaliziaji wa majengo madogo madogo lakini jengo kubwa msingi na nguzo vimekamilika hatua nyingine bado.<br>• Miradi hiyo ilistahili kutengewa sh. Bilioni 4.65 kwa mwaka 2019/20 kwa mjibu wa Mkataba itakamilika Oktoba, 2019 na malipo yanatakiwa kufanyika, hivyo inatakiwa kujiandaa kulipa nje ya bajeti kwa kuwa mwaka 2019/20 zimetengwa sh. Bilioni 0.5 |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | tu |
| | | • Mradi wa Usanifu wa Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS) – OR-MUU | 3,990,526,775.00 | | • Katika mwaka 2018/19 shughuli zifuatazo zilifanyika: Usanifu; utengenezaji; Majaribibio ya Mfumo; Kusafisha taarifa za Watumishi tayari kwa kuingizwa kwenye mfumo mpya; na Ununuzi wa Vifaa vya mfumo.<br>• Katika mwaka 2019/20, mradi ulitakiwa kuwekewa ukomo wa Shilingi bilioni 4.0 ili kufanikisha kujenga Uelewa wa watumiaji na wataalamu wasaidizi kwenye ngazi ya waajiri. Mwaka huu umetengewa sh. Bilioni 1.0 tu, hivyo Mfumo wa Taarifa za Utumishi na Mishahara utatekelezwa kwa asilimia 25 ya lengo. |
| | | Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Kuhifadhi Mifumo ya TEHAMA - eGA | 12,059,364,572.00 | | • Ujenziwa Kituo cha Kuhifadhi Mifumo ya TEHAMA kwa ajili ya Taasisi za Umma umeendelea kukamilika. Vituo vya kuhifadhi Mifumo na Taarifa za Serikali Mtandao vipo na vinatoa huduma kwa Serikali na Taasisi zake kupitia Wakala ya Serikali Mtandao.<br>• Mradi huu umekuwa ukitengewa kiasi |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | cha Shilingi bilioni 4.0 kwa ajili ya kuongeza uwezo wa Vituo vya kuhifadhia mifumo na Taarifa za Serikali mtandao, eneo ambalo linaendelea kukua siku kwa siku kutokana na msisitizo wa Serikali wa kujitegemea katika uhifadhi ili kuepukana na kutumia kwa maeneo hatarishi ya nje ya Serikali ambayo yanatishia usalama wa mifumo na Taarifa za Serikali. Mwaka 2019/20 zimetengwa Sh. Bilioni 2.5 tu, fedha hizi zitatekeleza mradi kwa asilimia 62.5 ya lengo la mwaka. |
| | | Mradi wa ujenzi wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma - Mtumba | 1,000,000,000.00 | | • Ujenzi wa Jengo la Ofisi umekamilika na tayari limeanza kutumika.<br>• Fedha hizi zilitolewa moja kwa moja hazikupitia katika Bajeti iliyoidhinishwa kwa Fungu 32. |
| | | Mradi wa ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Serikali Mtandao (eGA) - Mtumba | 1,000,000,000.00 | | • Ujenzi wa Jengo la Ofisi umekamilika na tayari limeanza kutumika.<br>• Fedha hizi zilitolewa moja kwa moja hazikupitia katika Bajeti iliyoidhinishwa kwa Fungu 32. |
| **JUMLA NDOGO** | | | 24,044,600,571.00 | | |
| | | | **OFISI YA RAIS, IKULU** | | |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| 536. | Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) | (i) Program ya Uhawilishaji Fedha kwa Walengwa kwa masharti ya lishe, elimu na afya | 4,759,470,400.00 | 338,294,857,455.18 | Shughuli zilizofanyika katika mradi huu ni pamoja na:<br>• Kuwezesha kaya maskini zisizo na nguvu kazi zikiwemo kaya zinazoongozwa na wazee, watoto na walemavu kupata ruzuku ya kujikimu ambapo Tanzania Bara ruzuku ilihawilishwa kwa kaya maskini 1,067,041 na Zanzibar kwa kaya maskini 32,248;<br>• Watoto katika kaya maskini kuhudhuria masomo shuleni na watoto walio chini ya miaka 5 kupelekwa kliniki;<br>• Kuboreshwa kwa lishe katika kaya maskini ili kuleta ufanisi wa watoto katika masomo na watu wazima kuweza kushiriki kikamilifu, na kwa ufanisi katika shughuli za kujiendeleza kiuchumi; na<br>• Kufidia gharama za kuwatunza kaya zenye watu walemavu. |
| | | (ii) Miradi ya kutoa ajira za muda kwa walengwa katika kutekeleza miradi | | 89,955,347,645 | • Kutolewa fursa kwa walengwa kupitia uanzishwaji wa miradi ambapo Tanzania Bara jumla ya miradi 8,384 |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | ya miundombinu hususan kwenye sekta ya elimu, afya, maji, barabara za vijijini na miradi ya utunzaji wa mazingira | | | imetekelezwa na kutoa ajira ya muda kwa kaya 230,738 katika Halmashauri 42, kwa upande wa Zanzibar jumla ya miradi 251 imetekelezwa na ilitoa ajira ya muda kwa kaya 14,555 Unguja na Pemba; na<br>• Kuongezeka kwa kipato kwa ajili ya kujikimu na kuwekeza katika shughuli za uzalishaji. |
| | | (iii) Miradi ya kukuza na Kuendeleza Uchumi wa Kaya | | 10,946,497,328.64 | • Kuundwa kwa vikundi vya kuweka akiba na kuwekeza ili kuwezesha kaya maskini kupata mitaji ya kuanzisha au kuendeleza shughuli za kiuchumi ambapo Tanzania Bara jumla ya vikundi 16,366 vyenye wanachama 226,050 vimeundwa na kuweza kuweka akiba ya shilingi milioni 2,491,993,261, kwa upande wa Zanzibar vikundi vya kuweka akiba 1,957 yenye wanachama 27,398 vimeundwa na kuweka akiba ya shilingi milioni 1,086,411,690;<br>• Walengwa wameunganishwa na huduma za ugani na kupata utaalam katika shughuli za kiuchumi katika sekta zote ili waweze kuzalisha kwa |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | tija; na<br>• Kaya maskini zenye nguvu kazi zimepatiwa mafunzo ya masuala ya kuendeleza uchumi wa kaya na wenye mahitaji wanatarajiwa kupata mitaji kuendeleza miradi yao. |
| | | (iv) Miradi ya Miundombinu | | 17,342,059,098.51 | • Kuendelea kuboreshwa kwa miundombinu ambapo Tanzania Bara jumla ya miradi 47 ya kuendeleza miundombinu katika sekta ya Elimu, Afya na Maji imetekelezwa na Zanzibar miradi 8 katika sekta ya Elimu na Afya imetekelezwa;<br>• Kutolewa kwa ujuzi na maarifa mbalimbali kwa walengwa wakati wa utekelezaji wa miradi kwa ajili ya kutastawisha maendeleo endelevu ya jamii husika; na<br>• Kustawishwa kwa maendeleo ya kilimo na mifugo na upatikanaji wa maji katika maeneo ya utekelezaji. Vile vile miradi itajenga uelewa katika matumizi bora ya ardhi na kupunguza mmomonyoko wa udongo kupitia utekelezaji wa miradi ya kulinda mazingira. |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| JUMLA NDOGO | | | 4,759,470,400.00 | 456,538,7619,527.32 | |
| **OFISI YA RAIS, TAMISEMI** | | | | | |
| 537. | Elimumsingi bila ada | Kuendelea kuratibu utoaji wa elimu msingi bila ada | 794,128,,495,243.90 | | Kuendelea kusimamia utoaji elimu msingi bila ada kwa shule za msingi na sekondari kwa kugharamia:<br>• Ruzuku ya uendeshaji kwa kila mwanafunzi;<br>• Chakula kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum wa shule za msingi na wanafunzi wa bweni kwa shule za sekondari kidato cha 1 hadi cha 4;<br>• Fidia ya ada kwa wanafunzi wa kutwa na bweni kidato cha 1 hadi cha 4; na<br>• Posho ya madaraka kwa walimu wakuu, wakuu wa shule na waratibu elimu Kata. |
| 538. | Ujenzi wa Hospitali za Halmashauri | Kujenga Hospitali 71 katika halmashauri ambazo hazina hospitali za Halmashauriza wilaya | 100,500,000,000.00 | | • Utekelezaji wa mradi unaendelea katika halmashauri 71 ambapo ujenzi wa Hospitali za Wilaya 68 unaendelea katika hatua mbalimbali kati ya asilimia 50 – 90 na maandalizi ya ujenzi yanaendelea katika Halmashauri 4 za Manispaa ya Ubungo (Dar es Salaam), Wilaya ya Tunduma (Songwe) na Hospitali ya Uhuru (Dodoma). Ujenzi wa hospitali |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | za halmashauri unahusisha majengo 7 kwa kila halmashauri ambayo ni jengo la utawala, jengo la wagonjwa wa nje, stoo ya dawa; maabara, jengo la vipimo vya mionzi, jengo la kufulia nguo na jengo la wazazi, ambapo:<br>• Ujenzi katika halmashauri 2 za Uvinza na Siha umefikia hatua ya kuinua kuta za msingi;<br>• Halmashauri 15 zipo katika hatua ya kuchimba msingi;<br>• Halmashauri 42 zipo katika hatua ya kusafisha eneo la mradi; na<br>• Halmashauri 6 za Mbarali, Buhigwe, Kilolo, Buchosa, Namtumbo na Ileje ujenzi umefikia kati ya asilimia 38 na asilimia 79 ambapo baadhi ya majengo yamekamilika yakiwemo jengo la wagonjwa wa nje na jengo la utawala katika Halmashauri ya Namtumbo. |
| 539. | Ujenzi na Ukarabati wa Vituo vya Afya | • Kukarabati na kuimarisha majengo na miundombinu katika vituo vya afya 518 vilivyokuwepo ngazi ya msingi na ujenzi wa | | 184,668,499,567.24 | • Vituo 352 vya kutolea huduma za afya vimekarabatiwa ambapo vituo 44 vimekamilika na kuanza kutoa huduma za upasuaji, na ukarabati wa vituo 306 umefikia kati ya asilimia 80 |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | nyumba za watumishi ifikapo 2020,<br>• Kujenga na kumalizia maboma yaliyopo 1,845 yanayohusu zahanati, vituo vya afya, Hospitali za Halmashauri, na nyumba za watumishi. | | | na 98,<br>• Nyumba 320 za watumishi zimejengwa, na<br>• Dawa na vifa tiba zimeagizwa kutoka Bohari ya Dawa (MSD). |
| 540. | Mradi wa kuendeleza Jiji la Dar es Salaam (DMDP) | Kujenga km 210 za barabara za lami, Mifereji ya Maji ya Mvua, Masoko, Zahanati, na Stendi katika Halmashauri za mkoa wa Dar es Salaam | | 84,965,590,046.00 | • Ujezi wa barabara zenye urefu wa km 114 unaoendelea ambapo jumla ya km 108 zimekamilika,<br>• Ujenzi wa madaraja mawili (2) umekamilika,<br>• Ujenzi wa masoko tisa (9) ya kimkakati unaendelea ambapo mawili yamekamilika,<br>• Ujenzi wa zahanati ya Buza katika Halmashauri ya Manispa ya Temeke yenye ukubwa wa ghorofa 2 na uwezo wa kuhudumia wagonjwa 100 kwa wakati mmoja,<br>• Ujenzi wa stendi mbili unaendelea katika Manispa ya Temeke.<br>• Ujenzi wa mifereji ya Maji ya Mvua km 40 unaendelea,<br>• Ujenzi wa Ofisi tatu za mradi zenye |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | maabara ya kisasa umekamilika. |
| 541. | Mradi wa Miji ya kimkakati (TSCP) | • Kujenga km 80.96 za barabara kwa kiwango cha lami katika Jiji la Dodoma, Arusha, Mbeya, Tanga na Mwanza na Katika Manispaa za Ilemela Kigoma Ujiji na Mtwara Mikindani,<br>• Kujenga mifereji mikubwa ya Mvua yenye km 16.47 ili kudhibiti mafuriko,<br>• Ujezi wa stendi mbili za kisasa katika Jiji la Dodoma na Manispaa ya Mtwara Mikindani,<br>• Ujenzi wa dampo (Jiji la Tanga na Mwanza)<br>• Ujenzi wa Masoko ya Kisasa mawili (2)<br>• Ujenzi wa vivuko 6 vya waenda kwa miguu | | **83,453,393,707.65** | • Ujenzi wa km 21.82 za barabara kwa kiwango cha lami umekamilika na ujenzi unaendelea,<br>• Ujenzi wa masoko mawili ya kisasa umefikia asilimia 60 katika jiji la Dodoma na katika Manispaa ya Mtwara mikindani,<br>• Ujenzi wa Stendi mbili za mabasi, Magari ya mizigo unaendelea,<br>• Ujenzi wa Mifereji ya mvua na madampo unaendelea.<br>• Ujenzi wa Vivuko vya waenda kwa miguu umekamilika. |
| 542. | Programu ya kujengea uwezo mamlaka za Serikali za miji (ULGSP) | • Kujenga km 161.4 za barabara kwa kiwango cha lami katika Halmashauri za miji 18 na kuweka taa za | | 335,549,214,007.61 | • Ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami zenye jumla ya km 116.60 umekamilika na km 44.80 unaendelea. |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | barabarani.<br>• Kujenga machinjio, stendi na masoko | | | • Ujenzi wa stendi tisa za Mabasi zinaendelea kujengwa pamoja na ujenzi wa stendi ya magari ya Mizigo unaendelea, kati ya hizo stendi 6 ujenzi zimekamilika na tatu unaendelea.<br>• Ujenzi wa machinjio 4 za kisasa unaendelea,<br>• Ujenzi wa masoko 4 unaendelea kati ya hayo moja limekamilika,<br>• Uandaaji wa Mipango ya Uendelezaji wa Miji 18 unaendelea, kati ya Mipango hiyo, Mipango ya miji 15 imeidhinishwa na Wizara ya Ardhi kwa ajili ya kuanza kutumika,<br>• Ununuzi wa Vifaa vya takajumla ya Magari 24,Hevy trucks 8 na Skip Bucket 178 zimenunuliwa.<br>• Ukarabati wa Madampo matatu unaendelea. |
| 543. | Matengenezo ya Barabara | • Matengenezo ya kawaida, maalumu na maeneo korofi yenye urefu wa km 63,463.89<br>• Kujenga barabara kwa kiwango cha Changarawe | 799,376,665,380.18 | | • Matengenezo ya kawaida, matengenezo maalum na sehemu korofi km 63,446.05.<br>• Kujenga kwa kiwango cha changarawe km 1,538.12 |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | km 1750.62<br>• Kujenga barabaa za Lami km 857.2.<br>• Kukarabati Madaraja 520<br>• Kujenga Madaraja madogo 370<br>• Kujenga Mdaraja Makubwa 21 | | | • Kujenga kwa kiwango cha lami km 485<br>• Kujenga madaraja makubwa yenye urefu wa mita 20 yapatayo 7.<br>• Kujenga madaraja madogo 225.<br>• Kujenga makalavati 7,168. |
| 544. | Ujenzi wa Majengo ya Utawala ya Halmashauri | • Ujenzi wa Majengo ya Utawala ya Halmashauri 23 | 118,473,914510 | | Ujenzi wa majengo 76 ya utawala unaendelea. Utekelezaji ulikuwa katika hatua ifuatayo:-<br>Majengo 5 yapo katika hatua ya ujenzi wa nguzo; Majengo 6 yapo katika hatua ya upandishaji wa kuta; jingo 1 lipo hatua ya Plasta; Majengo 2 ya po hatua ya upauaji na Majengo 9 yapo katika hatua ya umaliziaji ikiwemo upakaji wa rangi, kuweka marumaru, milango na mifumo ya umeme. |
| 545. | Mradi wa biashara na Uwekezaji wa Viwanda | • Ujenzi wa viwanda 100 kwa kila mkoa, sawa na viwanda 2,600 kwa mikoa 26<br>• Kutenga hekari 228,54 kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vidogo, vya kati na vikubwa | | | • Viwanda vidogo na vya kati 4,876 vimeanzishwa, sawa na asilimia 187.5 ya lengo la viwanda 2,600<br>• Kujenga viwanda vikubwa 108, vya kati 236, vidogo 2,522 na vidogo sana 2,010.<br>• Kutenga hekari 777,110.48, ambapo |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | hekari 367,077.21 ni kwa ajili ya viwanda vikubwa, vya kati na vidogo; hekari 41,119.4 ni kwa ajili ya minada, masoko na stendi; hekari 204,488.28 kwa ajili ya kilimo na skimu za umwagiliaji; hekari 21,425.6 kwa ajili ya machimbo ya dhahabu, shaba, chuma, gesi na mafuta; na hekari 143,000 kwa ajili ya malisho ya mifugo. |
| 546. | Ujenzi wa miundombinu ya elimu ya msingi na sekondari | Ukamilishaji wa maboma, na ujenzi wa miundombinu ya shule za msingi na sekondari | | 98,864,360,902 | • Ujenzi wa vyumba vya madarasa 5,192 katika shule za sekondari;<br>• Ujenzi wa matundu ya vyoo 11,888 katika shule za sekondari;<br>• Ujenzi wa mabweni 293 katika shule za sekondari;<br>• Ujenzi wa nyumba 155 za walimu katika shule za sekondari ;<br>• Ununuzi wa magari 40 kwa ajili ya usimamizi wa elimu;<br>• Ujenzi wa mabwalo 19 katika shule za Sekondari<br>• Ujenzi wa vyumba vya madarasa 4,023 katika shule za Msingi;<br>• Ujenzi wa matundu ya vyoo 11,888 katika shule za msingi; |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | • Ujenzi wa nyumba za walimu 1761 katika shule za msingi;<br>• ukarabati wa shule 138 za msingi;<br>• Ufuatiliaji na tathmini umefanyika katika Shule 502 katika shule za msingi na sekondari. |
| 547. | Ununuzi wa Boti | Kununua Boti 7 katika Halmashauri za Ludewa, Kibiti, Rufiji, Mafia, Ukerewe, Kigoma na Nyasa | 1,400,000,000 | | • Boti imenunuliwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti;<br>• Boti imenunuliwa katika Halmashauri ya Ludewa;<br>• Boti imenunuliwa katika Halmashauri ya Ukerewe;<br>• Boti imenunuliwa katika Halmashauri ya Rufiji;<br>• Boti imenunuliwa katika Halmashauri ya Nyasa;<br>• Boti imenunuliwa katika Halmashauri ya Kigoma; na<br>• Boti imenunuliwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Mafia. |
| 548. | Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo | Kutekeleza miradi ya kuchochea maendeleo ambayo ni kipaumbele cha wananchi | 42,024,276,000 | | • Ukamilishaji wa miradi ya miundombinu ya elimu katika shule za msingi na sekondari;<br>• Ujenzi na ukarabati wa zahanati na vituo vya Afya; |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | • Ujenzi wa miradi ya Maji;<br>• Miradi ya Uwezeshaji wananchi kiuchumi; na<br>• Uwekezaji wa viwanda vidogo |
| 549. | Miradi ya Kimkakati | Kutekeleza miradi ya kimkakati iliyokidhi vigezo vya utekelezaji | 132,923,923,817 | | • Ujenzi wa kiwanda cha vifungashio katika Halmashauri ya Maswa;<br>• Ujenzi wa kiwanda cha chaki katika Halmashauri ya Wilaya Maswa;<br>• Ujenzi wa Stendi ya Mabasi katika Halmashauri ya Wilaya ya Chato;<br>• Ujenzi wa Soko la Kisasa katika Halmashauri ya Mji wa Kibaha;<br>• Ujenzi wa soko la Kagunda katika Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma;<br>• Ujenzi wa Stendi ya Mabasi katika Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko;<br>• Ujenzi wa mradi wa Soko Muhange katika Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko;<br>• Ujenzi wa Soko la Mnanila katika Halmashauri Buhigwe;<br>• Ujenzi wa Stendi ya Mabasi katika Halmashauri ya Manispaa ya Moshi;<br>• Ujenzi wa Soko la Kisasa katika Halmashauri ya Manispaa ya |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | Morogoro;<br>• Ujenzi wa Ghala la kisasa katika Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa;<br>• Ujenzi wa Stendi ya Mabasi katika Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu;<br>• Ujenzi wa soko la kisasa Kisutu katika Halmashauri ya Manispaa ya Ilala;<br>• Ujenzi wa Soko la Mzimuni katika Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni;<br>• Ujenzi wa soko la Mburahati katika Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo;<br>• Ujenzi wa Stendi ya Mbezi Luiz katika Jiji la Dar es Salaam;<br>• Ujenzi wa kituo cha kuegesha malori Chapwa katika Halmashauri ya Mji wa Tunduma: na<br>• Ujenzi wa kiwanda cha Chumvi Itumbula katika Halmashauri ya Wilaya ya Momba;<br>• Ujenzi wa Mchinjio ya kisasa Vingunguti;<br>• Ujenzi wa Stendi ya Mabasi |

| Na. | Jina la Mradi | Malengo ya Mradi | Fedha Zilizotumika | | Hatua Iliyofikiwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha za Ndani (Tshs) | Fedha za Nje (Tshs) | |
| | | | | | Likongowele;' <br>• Ujenzi wa Stendi ya Mabasi Mpemba; na <br>• Ujenzi wa soko la Kimataifa katika Kijiji cha Kakozi. |
| 550. | Ujenzi wa Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Wilaya na Makazi ya Viongozi katika Mkoa na Wilaya | Ujenzi wa Ofisi ya Makazi ya Viongozi katika Mikoa na Wilaya | 23,800,000,000 | | • Ujenzi wa Ofisi na Makazi ya viongozi katika Mikoa katika Mikoa ya Katavi, Geita, Njombe, Simiyu, Songwe na Mbeya; <br>• Ujenzi wa Ofisi na Makazi ya Wakuu wa Wilaya katika Wilaya 19 zilizoanzishwa mwaka 2012/13; <br>• Ujenzi nyumba za Maafisa Waandamizi wa Mikoa na Wilaya. |
| **JUMLA NDOGO** | | | 2,012,627,274,951.08 | 787,501,058,230.50 | |
| **JUMLA KUU** | | | **24,629,849,730,363.80** | **13,183,357,322,993.90** | |